




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



RIPOTI YA  
MIRADI



MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU  
RIPOTI KUU YA MWAKA YA MIRADI YA MAENDELEO

MWAKA WA FEDHA 2021/22

MACHI 2023







JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' Simu: 255(026)2161200, Nukushi: 255(026)2117527, Barua pepe:ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Kumb.Na.CGA.319/421/01B

29 Machi 2023

Mheshimiwa. Samia Suluhu Hassan,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Ikulu,  
S.L.P. 1102,  
Chamwino,  
**40400 DODOMA.**

**RE: KUWASILISHA TAARIFA KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA MWAKA 2021/22 KUHSU MIRADI YA MAENDELEO**

Ninayo furaha kuwasilisha taarifa yangu kuu ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2021/22, kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, kifungu 418 (iliyorekebishwa 2020).

Kwa unyenyekevu, natoa shukrani za dhati kwa msaada ninaopata katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

Nawasilisha,

Charles E. Kichere


**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



# Kuhusu Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

## Uanzishwaji

Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 pamoja na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009.



### Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyu na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyu na upendeleo.

### Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

### Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihii na utumizi stahiki.



### Kufanya kazi kwa utaalim

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

### Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

### Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

## YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI	VI
ORODHA YA VIELELEZO	IX
ORODHA YA VIAMBATISHO	IX
ORODHA YA VIFUPISHO	X
MUHTASARI	2
SURA YA KWANZA	9
UTANGULIZI NA MUHTASARI WA MIRADI ILIYOKAGULIWA.....	9
SURA YA PILI	15
HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAGUZI ZILIZOPITA .....	15
SURA YA TATU	19
UTENDAJI WA KIFEDHA NA USIMAMIZI WA MATUMIZI.....	19
SURA YA NNE	50
USIMAMIZI WA UNUNUZI.....	50
SURA YA TANO	58
USIMAMIZI WA MIKATABA NA HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI.	58
SURA YA SITA	77
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA UJENZI WA KUFUA UMEME WA BWAWA LA JULIUS NYERERE .....	77
SURA YA SABA	90
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA UJENZI WA USAMBAZAJI WA MAJI .....	90
SURA YA NANE	99
UKAGUZI WA KIUFUNDI KWENYE UJENZI NA UKARABATI WA MELI .....	99
SURA YA TISA	114
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA KUBORESHA UBORA WA ELIMU YA SEKONDARI .....	114
SURA YA KUMI	129
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MABASI YA MWENDOKASI DAR-ES-SALAAM.....	129
SURA YA KUMI NA MOJA	141
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA UJENZI WA BARABARA KATIKA MIKOYA YA NJOMBE, MOROGORO NA KIGOMA .....	141
SURA YA KUMI NA MBILI	158
UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UDHIBITI WA UBORA WA MIRADI YA BARABARA INAYOENDELEA NA ILIYOKAMILIKA ILI KUZUIA UCHAKAVU KABLA YA MUDA WAKE.....	158
SURA YA KUMI NA TATU	169

UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA ....	169
SURA YA KUMI NA NNE	182
UKAGUZI WA KIUFUNDI KUHUSU GHARAMA KATIKA UJENZI WA MAJENGO YANAYOMILIKIWA NA SERIKALI .....	182
SURA YA KUMI NA TANO	198
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	198
VIAMBATISHO	202



## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Idadi ya miradi iliyokaguliwa kwa sekta katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 .....	11
Jedwali Na. 2: Majina na sura za ukaguzi wa kiufundi uliofanyika 2021/22 .....	12
Jedwali Na. 3: Utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa za kaguzi zilizopita .....	16
Jedwali Na. 4: Fedha ambazo hazijatumika .....	17
Jedwali Na. 5: Mwenendo wa ununuzi bila idhini ya bodi ya zabuni .....	18
Jedwali Na. 6: Miradi Iliyotekelawa na fedha zilizotumika -sekta ya kilimo .....	21
Jedwali Na. 7: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Elimu .....	22
Jedwali Na. 8: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Nishati na Madini .....	24
Jedwali Na. 9: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Afya .....	26
Jedwali Na. 10: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Uchukuzi na Mawasiliano .....	28
Jedwali Na. 11: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Maji .....	30
Jedwali Na. 12: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika - Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa .....	31
Jedwali Na. 13: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika - sekta mbalimbali .....	32
Jedwali Na. 14: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika ya Ofisi ya Makamu wa Rais .....	34
Jedwali Na. 15: Muhtasari wa Hati ya Ukaguzi zilizotolewa .....	35
Jedwali Na. 16: Mwenendo wa hati ya ukaguzi zilizotolewa .....	36
Jedwali Na. 17: Fedha zilizokopwa pasipo kurejeshwa .....	42
Jedwali Na. 18: Madai ya tozo .....	47
Jedwali Na. 19: Maoni katika kuzingatia sheria za ununuzi .....	51
Jedwali Na. 20: Maelezo yanayoonesha mikataba ambayo haijapitiwa ...	52
Jedwali Na. 21: Manunuzi ambayo hayajariotiwa kwa Bodi za Zabuni ...	53
Jedwali Na. 22: Manunuzi yaliyofanyika nje ya TANePS .....	54
Jedwali Na. 23: Miradi iliyoanza kutekelezwa bila ya kuwepo kwenye mpango wa manunuzi .....	57
Jedwali Na. 24: Maelezo yanayoonesha magari yaliyolipiwa lakini hayajapokelewa .....	59

Jedwali Na. 25: Mikataba ilioisha muda bila ya kuhuishwa .....	60
Jedwali Na. 26: Mwelekeo wa ukusanyaji mapato kutoka mwaka 2017/18-2021/22 .....	70
Jedwali Na. 27: Muhtasari wa fedha zilizopokelewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na TVETs .....	71
Jedwali Na. 28: Utendaji wa kifedha wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na TVETs .....	72
Jedwali Na. 29: Utekelezaji wa bajeti kwenye TVETs .....	72
Jedwali Na. 30: Muda wa wastani wa ujenzi wa miradi ya mabwawa ya umeme .....	79
Jedwali Na. 31: Taarifa ya kuchelewa kumlipa mkandarasi.....	98
Jedwali Na. 32 Uwandaaji usiojitosheleza wa usanifu wa michoro na kukosekana kwa michoro.....	116
Jedwali Na. 33: Mapungufu yaliyobainika katika usanifu wa miundombinu ya shule ngazi ya kata .....	117
Jedwali Na. 34: Mikataba iliyokosa ufanuzi wa mawanda ya kazi na utaratibu wa malipo.....	120
Jedwali Na. 35: Salio la fedha dhidi ya ukamilishaji wa kazi hadi kufikia tarehe 25 Septemba 2022 .....	121
Jedwali Na. 36: Kasoro zilizobainika katika shule zilizojengwa na kutembelewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa .....	124
Jedwali Na. 37: Mabadiliko ya usanifu na vigezo katika shule zilizotembelewa bila idhini .....	125
Jedwali Na. 38: Hali ya vifaa vya ujenzi vilivyopimwa katika shule zilizotembelewa .....	126
Jedwali Na. 39: Mapungufu ya usimikaji wa huduma kulikotokana na kuwatumia mafundi wasio na sifa.....	127
Jedwali Na. 40: Ongezeko la kipande cha kwanza .....	135
Jedwali Na. 41: Wafanyakazi wa kigeni wasiokuwa na vibali vya kazi ...	137
Jedwali Na. 42: Wafanyakazi wa kigeni walioajiriwa bila usajili wa bodi za kitaalamu za ndani .....	138
Jedwali Na. 43: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa kila hatua ya ununu .....	139
Jedwali Na. 44: Hali ya utekelezaji kwa taasisi.....	139
Jedwali Na. 45: Maelezo ya kina ya usanifu .....	143
Jedwali Na. 46: Mapungufu katika miundo iliyotengenezwa .....	149
Jedwali Na. 47: Hali ya umiliki wa vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni .....	152
Jedwali Na. 48: Mchanganuo wa ada za wahandisi .....	154
Jedwali Na. 49: Riba iliyolipwa kwenye malipo yaliyocheleweshwa kwa mkandarasi .....	156

Jedwali Na. 50: Hali ya kifedha ya mradi .....	157
Jedwali Na. 51: Miradi iliyotekelizwa.....	159
Jedwali Na. 52: Masuala ya sifa yaliyobainishwa katika miradi .....	166
Jedwali Na. 53: Taasisi na miradi iliyokaguliwa .....	183
Jedwali Na. 54: Miradi yenyе upembuzi yakinifu usiojitoesheleza.....	184
Jedwali Na. 55: Miradi ya ujenzi ambayo haikuwa imepangiwa bajeti...	185
Jedwali Na. 56: Miradi isiyokuwa na makadirio ya gharama za awali ....	186
Jedwali Na. 57: Kutokuwa na uhakika wa gharama zilizokadiriwa za mradi .....	186
Jedwali Na. 58: Uchambuzi wa riba iliyodaiwa .....	191
Jedwali Na. 59: Malipo yaliyolipwa zaidi kwa huduma maalum kwa mkandarasi mkuu .....	192
Jedwali Na. 60: Gharama zilizotumiwa kwa nguzo za kusimikwa ardhini	194
Jedwali Na. 61: Malipo ya Awali yalilipwa kwa wakandarasi wasaidizi bila makubaliano ya Mkataba .....	196



---

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa bidhaa zilizonunuliwa pasipo kupokelewa .....	18
Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka mitano mfululizo.....	36
Kielelezo Na. 3: Ugawaji usiofaa wa milango kwenye staha ya gari.....	106
Kielelezo Na. 4: Ukarabati usio sahihi wa sehemu zilizoharibika na zenyematundu .....	107
Kielelezo Na. 5: Mbao za boti za uokoaji zilizoharibika .....	110
Kielelezo Na. 6: Utupaji wa taka usiofaa kwenye eneo la mradi .....	113

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Muhtasari wa samani na vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano ...	202
Kiambatisho II: Kutokuanza kwa ujenzi na kutonunuliwa kwa vifaa vya shule mpya za sekondari.....	203
Kiambatisho III: Shule mpya za sekondari zilizojengwa bila hati miliki za ardhi.....	204
Kiambatisho IV: Taarifa za mkataba wa mhandisi mshauri .....	207
Kiambatisho V: Taarifa za mkataba wa mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya BRT..	208
Kiambatisho VI: Hati za Malipo pamoja na tozo za riba katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Lusitu - Mawengi kipande cha 2 kwa kiwango cha zege .....	209

## ORODHA YA VIFUPISHO

ADF	Mfuko wa Maendeleo ya Afrika
AfDB	Benki ya Maendeleo Afrika
AGTF	Mfuko wa Afrika wa Ustawi wa Pamoja
AQRB	Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi
ARU	Chuo Kikuu cha Ardhi
BADEA	Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika
BMGF	Mfuko wa Bill na Melinda Gates
BMU	Kikundi cha Usimamizi wa Mazingira ya Fukwe za Bahari
BRT	Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka
BSAAT	Mradi Endelevu wa Kuwezesha Kuzuia na Kupambana na Rushwa - Tanzania
BTIP	Uwekezaji wa Miundombinu ya Msingi ya Kusafirisha Umeme awamu ya pili
C1	Safu/tabaka la msingi wa barabara liliimashwa lenye kiwango cha 1 Mega paskali
C2	Safu/tabaka la msingi wa barabara liliimashwa lenye kiwango cha 2 Mega paskali
CBR	Kipimo Cha nguvu ya ardhi ya chini ya barabara
CDC	Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani
COEHME	Mradi wa Kituo Mahiri cha Ufuatiliaji na Tathmini ya masuala ya Afya
COSTECH	Tume ya Sayansi na Teknolojia
CREATE5	Kituo cha Umahiri cha Utafiti wa Kilimo, Sayansi ya Chakula na Usalama wa Lishe
CRR	Mwamba uliopondwa kwa ajili ya tabaka la kokoto la msingi wa barabara
CSR	Uwajibikaji kwa jamii
DANIDA	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denmarki
DAWASA)	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam
DFATD	Shirika la Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo
DFID	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza
DLLs	Viashiria vya Ugawaji wa Fedha
DMGP	Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam
DTP	Mradi wa Kidijitali Tanzania
DUTP	Programu ya Uboreshaji wa Miundombinu ya Usafirishaji Jijini Dar es Salaam
E&ME	Mtambo ya Umeme na Vifaa

EAC	Jumuiya ya Afrika Mashariki
EASTRIP	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki
EBARR	Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini
EcoRodMan	Usimamizi wa Kiikolojia na Kilimo Endelevu cha Panya na Usalama wa Chakula barani Afrika
EMA	Mradi wa Kuongeza Uwezo Kitaifa kwa ajili ya Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira
EP4R	Programu ya Lipa Kulingga na Matokeo kwenye Elimu
EPC	Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi
ERB	Usajili wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi
ERB	Bodi ya Usajili wa Wahandisi
ESIA	Taarifa ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii
ESPJ	Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji
EU	Jumuiya ya Ulaya
FSDT	Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa na Serikali ya Tanzania na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania
FTI	Taasisi ya Mafunzo ya Misitu
FYDP III	Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu
GAFSP	Programu ya Kimataifa wa Kilimo na Usalama wa Chakula
GAVI	Shirika la Dunia linalohusika na utaratibu wa Kutoa Chanjo
GEF	Kituo cha masuala ya Mazingira Duniani
GPSA	Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali
HEET	Mradi wa Kuchochea Mageuzi ya Kiuchumi kuititia Elimu ya Juu
HQ	Makao Makuu
HSPS	Mradi wa Kusaidia Sekta ya Afya
HSS	Miundo ya vyuma kwa ajili ya kuzamisha majini
IDA	Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza
IFAD	Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo
IJC	Vituo Jumuishi vya Haki
ILO	Shirika la Kazi Duniani
JICA	Shirika la Maendeleo la Japani
JNHP	Mradi wa Bwawa la Umeme Julius Nyerere
KfW	Shirika la Misaada la Ujerumani
KOICA	Kanada, Ireland, Shirika la Uhusiano wa Kimataifa la Korea Kusini
KTPIP	Mradi wa Kuunganisha Umeme Kenya na Tanzania
LANES	Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu

LDFS	Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na Kuongeza Uhakika wa Chakula katika Maeneo Kame Tanzania
LV WATSAN	Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira - Ziwa Viktoria
LVBC	Tume ya Bonde la Ziwa Victoria
m	mita
MLVMCT	Mradi wa Kimataifa wa Usafirishaji na Mawasiliano wa Ziwa Viktoria
MLYMCT	Mradi wa Kimataifa wa Usafiri na Mawasiliano wa Ziwa Victoria
mm	Milimita
MoU	Hati ya Makubaliano
MoW	Ministry of Water
MRCC	Kituo cha Utafutaji na Uokoaji cha Ziwa Victoria
MRCC	Kituo cha Utafutaji na Uokoaji cha Ziwa Victoria
MSCL	Kampuni ya Huduma za Meli
NACTE	Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundı
NCMC	Kituo cha Kudhibiti Hewa ya ukaa Nchini
NEMC	Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira
NFAST	Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia
NIT	Chuo cha Taifa cha Usafirishaji
NM-AIST	Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela
NORAD	Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norwei
OFID	Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani
OPEC	Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta
OR-TAMISEMI	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PAPs	Waathirika wa Miradi
PFMRP	Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma
PPRA	Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma
PSSN	Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini
RAP	Mpango wa Hatua za Uhamishaji
REGROW	Mradi wa Maliasili Endelevu kwa Ukuaji
RGDM	Mwongozo wa Usanifu wa Kijiometri wa Barabara
RIF	Mfuko wa Miundombinu ya Reli
RISE	Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Barabara katika Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi
RRFHP	Mradi wa Umeme wa Kikanda wa Maporomoko ya Maji wa Rusumo
RUWASA	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
SDF	Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi

SE4ALL	Mradi Endelevu wa Nishati kwa Wote
SEQUIP	Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari
SGR	Reli ya Kisasa
Sh.	Shilingi za Kitanzania
SIDA	Shirika la Ushirkiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi
SPARCO	Utafiti katika Kujenga Uwezo wa Kupambana na Maradhi ya Selimundu
SRWSSP	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijijini
SWASH	Usafi wa Maji Shulenii
SWIOFish	Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Ukuaji wa Pamoja Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi
SWRSSP	Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
TACAIDS	Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania
TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TANePS	Mfumo wa Ununuzi wa Kieletroniki Tanzania
TANESCO	Shilika la Umeme Tanzania
TANIPAC	Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu
TANROADS	Wakala wa Barabara nchini Tanzania
TARURA	Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini
TASAC	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania
TASAF	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii
TATO	Chama cha Watoa Huduma za Utalii Tanzania
TAZA	Mradi wa Kuunganisha Umeme Tanzania na Zambia
TBA	Wakala wa Majengo Tanzania
TCU	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania
TEA	Mamlaka ya Elimu Tanzania
TEAGEP	Mradi wa Kuimarisha Uwajibikaji na Utawala Bora katika Tasnia ya Uziduaaji
TECU	Kitengo cha Ushauri wa Kihandisi cha Wakala wa Barabara Tanzania
TEITI	Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia
TESP	Mradi wa Kusaidia Elimu kwa Walimu
TIRDP	Mradi wa Maendeleo ya Reli ya Kimataifa Tanzania
TMP	Mradi wa Kisasa wa Kuboresha Mfumo wa Kodi
TPA	Mamlaka ya Bandari ya Tanzania
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
TRC	Shirika la Reli Tanzania
TSDP	Mradi wa Maendeleo wa Nishati ya Jua - Shirika la Umeme Tanzania

TSSP	Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji
TTGRUP	Mradi wa Kuboresha na Kukarabati Gridi ya Umeme
TVETs	Vituo vya Juu vya Mafunzo ya Elimu ya Ufundis
UDSM	Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam
UNDP	Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
UNEP	Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa
UNICEF	Uswisi na Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto
UNOPS	Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Huduma za Miradi
USAID	Shirika la Misaada la Watu wa Marekani
UTC	Mradi wa Kuboresha Vyuo vya Ualimu
UVIKO	Ugonjwa wa Virusi vya Korona
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
WSDP	Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji





# STATEMENT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

Ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Jumla ya Mwaka ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Taarifa hii inatoa uchambuzi wa kina wa miradi mingi inayofadhiliwa na serikali na washirika wa maendeleo, inayojumuisha vipengele kama vile utendaji wa kifedha na kimwili, ununuzi, usimamizi wa mikataba, mipango na muundo.

Taarifa inabainisha mapungufu makubwa katika miradi mingi na inatoa mapendekewe ya kuboresha, ikisisitiza haja ya washikadau kuchukua hatua za kurekebisha. Miradi mashuhuri iliyojadiliwa ni pamoja na Mradi wa Umeme wa Maji wa Julius Nyerere, Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya 2, Ujenzi wa Reli ya Kimataifa (Standard Gauge), na Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP). Taarifa hii pia ilipitia udhibiti wa gharama katika majengo yanayomilikiwa na serikali na udhibiti wa ubora katika miradi ya ujenzi wa barabara.

Matokeo yanahimiza uwazi, uwajibikaji, na utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo. Tunatumai washikadau watatumia taarifa hii kukabiliana na changamoto zilizobainishwa na kuimarisha utendaji wa mradi kwa ujumla.

Kwa kumalizia, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, taarifa hii ni nyenzo muhimu ya kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa miradi katika sekta ya umma, na kuchangia katika uboreshaji unaoendelea na kufikia mafanikio ya malengo ya maendeleo nchini.



Charles E. Kichere

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

## MUHTASARI

### (i) Utendaji wa Kifedha

Zaidi ya asilimia 90 ya miradi ilipata hati zinazoridhisha kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2017/18, hii ikiwa ni ishara nzuri kwenye matumizi ya fedha na uandaaji wa taarifa za fedha zinazoaminika. Hata hivyo, utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za nyuma kwa kipindi hicho cha miaka mitano haufiki 50% ikiambatana na uwepo kwa hoja zinazojirudia kama inavyoonekana katika sura ya pili ya ripoti hii.

Zaidi ya hayo nilibaini mapungufu kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoidhinishwa kwa Hati ya Makubalino kati ya Tanzania na Uganda inayohusu utekelezaji wa mradi ya Kimataifa wa Usafiri na Mawasiliano wa Ziwa Viktoria (MLVMCT) na uendeshwaji shughuli za Tume ya Bonde la Ziwa Victoria nje ya nchi washiriki wa mradi. Pia nilibaini kuwa mkataba kati ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) haujafanyiwa mapitio ili kujumuisha mafunzo ya ubunifu na mafunzo kwa njia ya mtandao, pia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ilishindwa kuunda kitengo kanachojitosheleza cha utekelezaji wa mradi wa Maendeleo ya Barabara na Ufunguaji Fursa za Kiuchumi Vijijini (RISE).

Nimebaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa matumizi na bajeti ikiwa ni pamoja na fedha za miradi kiasi cha Sh. bilioni 8.99 kukopwa bila kurejeshwa; hati za malipo zenye thamani ya Sh. 632.5 milioni hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi katika Chuo cha Walimu Sumbawanga kilichopokea fedha za Programu ya Elimu kwa Matokeo (EP4R) zenye thamani ya Sh. bilioni 3 kwa ajili ya ujenzi wa chuo kipyaa, baadhi ya hati za malipo na nyaraka zinazohusiana na mradi huo hazikuhakikiwa kutokana na kuteketea kwa moto tarehe 25 Disemba 2021.

Mengine niliyoyabaini ni kushindwa kwa Serikali kuchangia sehemu yake ya fedha iliyopaswa kuchangia kwenye miradi kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 6.24 (Sh. bilioni 14.3) katika Mradi Endelevu wa Utoaji Maji Safi na Usafi wa Mazingira wa Mjini Arusha (ASUWSDP); malipo ya fidia kwa watu walioathirika na mradi ambayo hayajalipwa yenye thamani ya Sh. bilioni 11.37 yanayohusiana na Mradi wa Horohoro Bagamoyo Lunga na Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato inayotekelze wa Wakala wa Barabara

Tanzania (TANROADS), pia riba iliyotozwa na wakandarasi ya Sh. bilioni 2.57 kutokana na kutolipa kwa wakati hati za malipo za wakandarasi (IPCs).

#### **(ii) Usimamizi wa ununuzi**

Nilibaini kuwa kati ya watekelezaji wa miradi 290, watekelezaji 208 walizingatia sheria za ununuzi wakati watekelezaji 82 walizingatia sheria lakini walikuwa na mapungufu. Nilibaini mikataba yenyе thamani ya Sh. bilioni 2.51 haikupitiwa na kuhakikiwa na wanasheria wa taasisi husika, ununuzi mdogo wa Sh. milioni 506.76 kutowasilishwa kwenye Bodi za Zabuni, ununuzi wa Sh. 14.92 bilioni kufanyika nje ya Mfumo wa Ununuzi wa Kieletroniki Tanzania (TANePS). Pia nilibaini MoEST ilianzisha utekelezaji wa shughuli za miradi by EPforR yenyе thamani ya Sh. bilioni 3.82 bila kuhusisha mpango wa ununuzi na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (PO-RALG) kuitia Programu ya Kusaidia Sekta ya Afya (HSSP) kuchelewa kununua dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.66 kwa takribani miezi 20.

#### **(iii) Usimamizi wa mikataba na hali halisi ya utekelezaji wa miradi**

Katika usimamizi wa mikataba, nilibaini magari yaliyolipiwa lakini hayakupokelewa yenyе thamani ya Sh. bilioni 26.28, mikataba iliyo fikia ukomo bila kuhuhishwa yenyе thamani ya Sh. milioni 421.75 na malipo ya awali yaliyo cheleweshwa kulipwa ambayo yalisababisha malipo ya riba ya Sh. milioni 879.26. Pia nilibaini utekelezaji wa miradi inayohusiana na usafi wa mazingira inayotekelawa na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) kabla ya kupata idhini ya taarifa ya kina ya mradi kutoka kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Katika hali ya utekelezaji wa miradi, nilibaini mapungufu mbali mbali ikiwa ni pamoja na ujenzi uliotelekezwa wa maghala 14 na miundombinu saidizi ya nje wilayani Babati, kushindwa kwa mkandarasi kuweka mfumo wa udhibiti wa garimoshi kwa zaidi ya miaka minne kwenye reli ya Dar-es-salaam-Isaka wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2.04 wakati kazi za kuimarishe na kuongeza kina cha Gati Na. 8-11 katika bandari ya Dar es salaam hazi jaanza kwa zaidi ya miaka mitano. Pia kutokuanza kwa ujenzi na ununuzi wa vifaa katika shule 35 za awali za mfano kutokana na kukosekana kwa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze bado haijakabidhi

majengo yaliyokamilika, vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Kikundi cha Usimamizi wa Mazingira ya Fukwe za Bahari (BMU) cha Saadan na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kutokupeleka kiasi cha Sh. milioni 651.85 kwenda kwenye miradi tisa ya jamii iliyoidhinishwa.

#### **(iv) Mradi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere**

Nilibaini makadirio ya muda wa kukamilisha mradi usio halisi kwani mradi ulipangwa kukamilika katika kipindi cha miaka mitatu huku miradi ya ukubwa kama huo iliyojengwa duniani kote ilichukua kati ya miaka 4 hadi 10 kukamilika, hii inaonesha kuwa makadirio ya muda ya awali hayakuwa halisi. Pia nilibaini kuwa hakukuwa na makubaliano ya pande zote kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na mkandarasi kuhusu muda ulioongezwa wa kukamilisha mradi. Zaidi, nilibaini viashiria vya hatari ya uhaba wa maji kutokana na shughuli za kibinadamu zisizodhibitiwa katika vyanzo vya maji.

Nilibaini majoribio ya turubini ya mfano yalifanyika bila kushuhudiwa na mwajiri; TANESCO kutotoza gharama za ukiukaji wa mashariti ya mkataba kiasi cha Sh. bilioni 327.93; kutokuwa na ufanisi katika kushughulikia madai ya mkandarasi, kucheleva kufanya maombi ya marekebisho ya bei, ununuzi wa mitambo ya umeme kwa miaka miwili pamoja na kutotekelizwa kwa majukumu ya kijamii ya kampuni (CSR) kwa miaka mitatu na miezi 11.

#### **(v) Ujenzi wa miradi teule ya maji**

Nilibaini dosari mbali mbali ikiwa ni pamoja na takwimu za haidrolojia zilizotumika kusanifu kibanio cha mradi wa Kigoma hazikuwa za kutosha ili kuwezesha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na utabiri wa hali ya hewa huku mradi wa Tinde Shelui ukitekelezwa bila kuzingatia hitaji la mtandao wa usambazaji maji na hivyo kupelekea matangi mapya na mabomba ya kuitisha maji kutoka kwenye chanzo, na tangi lenye ujazo mita 1,150 lililojengwa katika kijiji cha Buchama kutotumika.

Aidha, nilibaini kuwa uwezo wa sasa wa mtambo wa kusafisha maji wa Ihelele kwenye mradi wa Tinde Shelui ni mita za ujazo 80,000 kwa siku, ambazo zitakidhi mahitaji ya maji yaliyotarajiwa kwa takribani miaka mitatu, hii itasababisha uwepo wa mgao wa maji kabla ya kufikia mwaka

2025 na kutakuwa na upungufu wa mita za ujazo 91,569.83 kwa siku ifikapo mwaka 2035.

**(vi) Ujenzi na ukarabati wa meli**

Nilibaini mapungufu kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa miundombinu duni, uwekaji usiofaa wa milango na uwekaji usiojitosheleza wa boti za kuokoa maisha katika usanifu wa msingi wa meli mpya. Pia nilibaini kuwa ujenzi wa meli mpya ulianza bila andiko la dhamira na kabla ya kukamilika kwa njia ya maegesho ya meli na hivyo kusababisha ucheleweshaji na gharama za ziada za zaidi ya dola za Kimarekani milioni 3 sawa na Sh. bilioni 7.8. Nilibaini kuwa injini zilizowekwa kwenye MV Victoria zilikuwa na vipimo tofauti.

**(vii) Utekelezaji wa mpango wa kuboresha elimu ya sekondari**

Nilibaini mapungufu katika uandaaji wa michoro ya usanifu na idhini zake, kuchelewa kuajiliwa kwa mhakiki wa kujitegemea, uandaaji usiojitosheleza wa mikataba ya mafundi na bajeti isiyo na uhalisia katika ujenzi. Aidha, nilibaini kuchelewa uhamishaji kwa fedha kwa ajili ya shughuli za usimamizi katika shule 232 katika ngazi ya kanda, mkoa, na halmashauri vilevile uhaba wa wafanyakazi wenyewe ujuzi katika kazi za ufundi umeme, keknolojia ya habari na mawasiliano, usanifu wa maji na ufungaji wa gesi katika ngazi ya kata.

**(viii) Mradi wa mabasi yaendayo haraka awamu ya pili Dar es Salaam**

Nilibaini usimamizi duni wa muda na kutokuhuisha kwa wakati dhamana ya malipo ya awali. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa baadhi ya ujenzi wa zege uliofanyiwa vipimo haukidhi ubora wa viwango vya uimara wa zege vinavyotakiwa, Kwa mfano, uimara wa ngazi upande wa kulia wa Daraja la Mbagala la watembea kwa miguu ulikuwa 22 kati ya  $40 \text{ N/mm}^2$ , na uimara wa vizuizi vya ajali upande wa kushoto na kulia wa Barabara ya Kilwa/Mandela katika makutano ya daraja la juu ulikuwa 28 na 23 matawaliwa kati ya  $40 \text{ N/mm}^2$  zinazohitajika. Zaidi ya hayo, vifusi vilivyohifadhiwa havikuwekwa kwenye mpangilio unaoendana na matakwa ya mkataba na viwango maalumu vinavyohitajika.

Aidha, nilibaini utozaji wa riba ya Sh. milioni 904.78 kutokana na kuchelewa kuwalipa wakandarasi na kuongezeka kwa gharama ya Sh. bilioni 7.67 kutokana na marekebisho ya usanifu.

**(ix) Miradi ya ujenzi wa barabara kwenye Mikoa ya Njombe, Morogoro na Kigoma**

Ukaguzi wangu wa miradi ya ujenzi wa barabara kwenye mikoa ya Njombe, Morogoro na Kigoma ulibaini upana wa usanifu wa barabara kuwa chini ya mita 7.5, gharama za ziada za kudhibiti mchwa Sh. bilioni 4.41 zilizotokea bila idhini ya mwajiri kwenye kipande cha 3, Makutano ya barabara ya Mvugwe - Nduta. Kuwepo kwa ongezeko la bei ya mkataba kwa Sh. bilioni 10.23 na Sh. milioni 980 kwa chuma na polyethylini, mtawalia katika mradi wa Lusitu-Mawengi kipande cha pili kutokana na kutojumuishwa kwa vitu hivi muhimu kwenye nyaraka za zabuni.

Aidha, usimamizi duni wa masuala ya uhamiaji kwa wafanyakazi wa kigeni kumepelekea wafanyakazi 26 kutoka nje ya nchi kufanya kazi bila vibali vyta kazi na wafanyakazi 27 bila kuwa na vibali vyta makazi na hivyo kupelekea upotetu wa mapato ya serikali ambayo yangetokana na makusanyo ya ada za vibali vyta kazi na ukaazi kiasi cha Sh. milioni 232.27.

**(x) Udhhibiti ubora wa miradi ya barabara ili kuzuia uchakavu na uharibifu wa mapema**

Miongoni mwa mapungufu niliyoyabaini kwenye udhibiti ubora wa miradi ya barabara ili kuzuia uchakavu na uharibifu wa mapema ni pamoja na usanifu duni wa barabara, kutohuishwa kwa kanuni za viwango vyta kazi za barabara kwa takribani miaka 22 iliyopita na kutofanyiwa marekebisho kwa mwongozo wa usanifu wa lami na vifaa wa mwaka 1999 kwa takribani miaka 23. Pia nilibaini, ucheleweshwaji katika kuajiri mhandisi mshauri na msimamizi wa miradi ya barabara ambapo, miradi mitano kati ya nane iliyokaguliwa ilishirikisha na wahandisi washauri baada ya wakandarasi kuanza kufanya kazi. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwepo kwa migongano ya kimaslahi na kutokuwepo na usawa kwenye michakato ya kuingia mikataba kati ya Kitengo cha Ushauri wa Kihandisi TANROADS (TECU) na TANROADS. Usimamizi duni wa mradi na mikataba unaofanywa na washauri, kwani wataalamu muhimu wanaohusika na kazi za uhandisi katika miradi ya

barabara hawakuwa wamesajiliwa kama wahandisi wataalamu, kinyume na kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi.

#### **(xi) Ujenzi wa reli ya kisasa**

Nilibaini ukosefu wa viwango maalum kwa kazi ya mfumo wa umeme kwa ajili ya makandarasi kufanya nukuu za bei na makadirio ya gharama za mradi wa umeme hayakuzingatia sanifu na tafiti za awali. Zaidi ya hayo hakukuwa na muda uliopangwa wa kukamilisha ujenzi wa karakana ya kuunganisha treni za umeme za kisasa.

Shirika la Reli Tanzania (TRC) halikutumia njia ya ununuzi ya ushindani katika ujenzi wa reli ya kisasa kwa kipande cha tatu na cha nne na kusababisha kuongezeka kwa Dola za Kimarekani milioni 1.3 na milioni 1.6 kwa kilomita mtawalia ikilinganishwa na mikataba ya awali.

Kuongezeka kwa gharama ya ununuzi wa treni na mabehewa ya abiria kwa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 215.05 (Sh. bilioni 492.46), na Euro milioni 4.53 (Sh. bilioni 11.59) mtawaliwa kutokana na usimamizi duni wa mikataba. Vile vile mkataba ulitekelezwa bila kuwepo kwa dhamana ya utendaji, hali iliyosababisha hasara ya kiasi cha Euro milioni 5.32 (Sh. bilioni 13.6), na kutotoza gharama za uchelewashaji wa kazi kwa mujibu wa mkataba.

Pia, nilibaini viashiria vya kutumia Dola za Kimarekani milioni 11.19 (Sh. bilioni 25.62) zaidi ya kiwango kilichopangwa kutoka fungu la fedha za dharura katika ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha kwanza kutokana na kuongezeka kwa muda wa ujenzi wa reli kwa zaidi ya siku 1441, hii imepelekea kuongezeka kwa gharama ya Mhandisi Mshauri wa mradi kwa Dola za Kimarekani milioni 11.32. Vile vile nilibaini mapungufu katika usimamizi wa vibali vya raia wa kigeni.

#### **(xii) Usimamizi wa gharama katika ujenzi wa majengo yanayomilikiwa na Serikali**

Nilibaini mapungufu mbali mbali katika tathmini ya usimamizi wa gharama katika ujenzi wa majengo yanayomilikiwa na Serikali. Mapungufu hayo ni pamoja upembuzi yakinifu usiojitosheleza, maandalizi ya viwango maalumu yasiyojitosheleza na utumiaji wa njia za ununuzi zisizo za ushindani.

Zaidi ya hayo, kutokuwepo kwa nyaraka za mikataba kwa baadhi ya miradi. Kushindwa kudai msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani Sh. bilioni 4.27 na madai ya riba ya Sh. bilioni 12.12 iliyotokana na kuchelewa kulipa wakandarasi. Malipo zaidi ya Sh. milioni 562.68 na Sh. milioni 584.68 mtawalia yaliyotokana na makadirio ya gharama yasiyojitosheleza kwa nguzo za kusimikwa ardhini.

Malipo ya awali Sh. milioni 857.21 na Sh. bilioni 4.83 hayakurejeshwa na yalilipwa bila kuwepo kwa matakwa ya kimkataba.



# SURA YA KWANZA



UTANGULIZI NA MUHTASARI WA MIRADI  
ILIYOKAGULIWA

## **1.0 Utangulizi**

Serikali ya Tanzania inatekeleza kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano Awamu ya Tatu 2021/22-2025/26, unaolenga kuongeza uwezo wa uzalishaji, kujenga uchumi shindani, na kuboresha maendeleo ya watu. Mpango huo unalenga kufikia malengo haya kwa kuboresha miundombinu, kuimarisha sera za biashara na uwekezaji, na kurekebisha mifumo ya elimu na mafunzo. Sura hii inaainisha bajeti na aina za miradi ya maendeleo iliyotekelizwa, historia yake na majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Maafisa Masuuli.

### **1.1 Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/22**

Serikali iliandaa bajeti ya kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia afua zilizopitishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano Awamu ya Tatu, ikijumuisha miradi mikuu kama Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili, Mradi wa Bwawa la Umeme Julius Nyerere (JNHPP). Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Barabara katika Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE), Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam (DMGP) na mingineyo.

### **1.2 Aina za kaguzi zilizofanyika**

Katika mwaka wa fedha 2020/21, nilifanya kaguzi za aina tatu kwenye miradi ya maendeleo ambayo ni ukaguzi wa fedha, ukaguzi wa uzingatiaji kama sheria na taratibu zimefuatwa na ukaguzi wa kiufundi.

#### **1.2.1 Ukaguzi wa fedha**

Ukaguzi wangu wa fedha unazingatia zaidi tathmini ya mfumo wa uhasibu, udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa fedha na kufuata sheria na kanuni. Nimetoa maoni ya ukaguzi kupitia taarifa zangu za ukaguzi 293 katika mwaka wa fedha 2020/21.

## 1.2.2 Ukaguzi wa Kiufundi

Nimefanya kaguzi tisa za kiufundi kwenye miradi ya ujenzi katika sekta za usafirishaji, nishati, maji na kilimo. Kaguzi zilijikita katika mipango, usanifu na ununuzi; afya, usalama na mazingira; na usimamizi wa mikataba.

## 1.2.3 Ukaguzi wa uzingatiaji kama sheria na taratibu zimefuatwa

Katika mwaka wa fedha 2021/22, nimekagua taasisi 290 kwa lengo la kutathmini kama sheria na taratibu za ununuzi zimefuatwa kwa mujibu wa kifungu 48(3) cha Sheria ya Ununuzi ya 2021.

## 1.2.4 Mawanda ya ukaguzi

Katika mwaka wa fedha 2020/21, nilikagua miradi 105 iliyotekelizwa na taasisi 248 ikijumuisha taarifa za ukaguzi 300 kama zinavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 1 na 2**.

**Jedwali Na. 1: Idadi ya miradi iliyokaguliwa kwa sekti katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21**

Na.	Sekta	Idadi ya taarifa za ukaguzi wa kiufundi	Idadi ya taarifa za ukaguzi wa fedha <sup>1</sup>	Idadi ya miradi iliyokaguliwa	Idadi ya watekelezaji wa miradi <sup>2</sup>	Jumla ya taarifa za ukaguzi
1	Kilimo	-	7	7	4	7
2	Elimu	1	14	9	6	15
3	Nishati na Madini	1	17	18	3	18
4	Afyah	0	195	10	188	195
5	Usafirishaji	7	14	20	10	21
6	Maji	1	9	7	8	10
7	Jamii	-	10	10	10	10
8	Miradi mingineyo	0	24	24	19	24
Jumla		10	290	105	248	300

**Chanzo:** Taarifa za kaguzi za fedha, kiufundi na uzingatiaji kama sheria na taratibu zimefuatwa kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2022

<sup>1</sup> Matokeo ya ukaguzi wa kufuata sheria za manunuzi yalijumuishwa katika taarifa 290 za fedha

<sup>2</sup> Idadi ya watekelezaji wa mradi ni kwa idadi ya miradi iliyokaguliwa

## Jedwali Na. 2: Majina na sura za ukaguzi wa kiufundi uliofanyika 2021/22

Na.	Sekta	Majina ya kaguzi za kiufundi	Marejeo ya sura
1	Nishati na Madini	Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Bwala la Umeme la Julius Nyerere (JNHPP)	6
2	Maji	Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Miradi Teule ya Ugavi wa Maji	7
3	Usafirishaji	Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi/Utgenezaji wa Meli na Vivuko	8
4	Elimu	Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	9
5	Usafirishaji	Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT)	10
6	Usafirishaji	Ukaguzi wa Kitaalam wa Ujenzi wa Miradi ya Barabara katika Mikoa ya Njombe, Morogoro na Kigoma	11
7	Usafirishaji	Ukaguzi wa Kiufundi wa Udhibiti wa Ubora wa Miradi ya Barabara Zilizojengwa Katika Kuzuia Kushindwa kwa Mapema	12
8	Usafirishaji	Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR)	13
9	Usafirishaji	Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu Udhibiti wa Gharama katika Ujenzi wa Majengo Yanayomilikiwa na Serikali	14

**Chanzo:** Taarifa za kaguzi za kiufundi na tathmini kama sheria na taratibu zimefuatwa kwa mwaka wa fedha ulioiishia 30 Juni 2022

### Sekta ya kilimo

Katika kuwezesha na kuboresha maendeleo kwa utumiaji wa fursa za kilimo zinazotolewa na matumizi ya njia janja za kilimo endelevu kwa mabadiliko ya tabianchi, kuititia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano Awamu ya Tatu, juhudhi zimeelekezwa katika sekta hii. Katika mwaka wa fedha 2021/22, nimetoa taarifa saba za ukaguzi chini ya sekta hii ambazo zinahusiana na ukaguzi wa kifedha kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 6**.

### Sekta ya elimu

Katika mwaka wa fedha 2021/22, nimetoa taarifa za ukaguzi 14 chini ya sekta hii zilizolenga kuboresha mifumo ya elimu na ujifunzaji ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 7**.

## Sekta ya nishati na madini

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano Awamu ya Tatu unalenga kukuza uchumi wa viwanda unaozingatia maliasili katika sekta ya madini nchini kwa kutekeleza afua muhimu kama vile kuimarisha usimamizi na udhibiti wa uchimbaji madini wakubwa na wa kati, kuwawezesha wachimbaji wadogo, kukuza uongezaji thamani na kunufaisha madini kutambua na kuwawezesha uchimbaji wa madini adimu. Serikali pia imedhamiria kuboresha upatikanaji na uhakika wa nishati ya umeme katika maeneo ya vijijini na mijini. Katika mwaka wa fedha 2021/22, taarifa 17 za ukaguzi zimetolewa chini ya sekta ya nishati kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 8.**

## Sekta ya afya

Sekta ya afya ni muhimu kwa maendeleo ya watu, ikijumuisha miundombinu, wataalamu wa matibabu, vifaa na vifaa, huduma za tiba na kinga na bima ya afya. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano Awamu ya Tatu unaweka kipaumbele katika kuimarisha mifumo ya usimamizi wa afya, upatikanaji wa huduma, na utoaji na kushughulikia changamoto za ubora kwa kuanzisha afua muhimu kama vile kujenga na kukarabati vituo vya afya, kukuza miradi ya bima ya afya na kuboresha huduma za jadi za afya. Katika mwaka wa fedha 2021/22, nimetoa ripoti 195 za ukaguzi zinazohusiana na sekta ya afya kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 9.**

## Sekta ya usafirishaji

Serikali imejikita katika kuboresha miundombinu ya usafirishaji nchini chini ya sekta ya uchukuzi, kwa kuzingatia Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usafiri 2011-2025. Hii ni pamoja na kuboresha viwanja vya ndege, barabara, reli na bandari ili kuwawezesha shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka wa fedha 2021/22, taarifa 14 za ukaguzi zimetolewa chini ya sekta hii kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 10**

## Sekta ya maji

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano Awamu ya Tatu unalenga katika kuboresha upatikanaji na usambazaji wa huduma za

maji na usafi wa mazingira na kulinda vyanzo vya maji na mazingira. Wizara ya Maji inatekeleza mageuzi ya kisekta, ikiwa ni pamoja na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), ili kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji na huduma za usafi wa mazingira vijijini na mijini. Katika mwaka wa fedha 2021/22, taarifa 9 za ukaguzi zimetolewa chini ya sekta hii kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 11**.

### **Sekta ya jamii**

Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania Awamu ya Tatu (TASAF III)/Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN) na Miradi inayofadhiliwa na UNDP ni mipango muhimu katika sekta ya ustawi wa jamii inayolenga kuwezesha jamii na kutoa fursa za maisha bora inayoendana na Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Umaskini. na Malengo ya Maendeleo ya Milenia. TASAF III inalenga katika kuimarisha upatikanaji wa fursa za mapato na huduma za kijamii na kiuchumi kwa kaya zinazolengwa, wakati PSSN inatoa uhamisho wa fedha wenye tija, kazi za umma, na msaada wa kimsingi wa maisha kwa kaya maskini zaidi na zilizo hatarini zaidi kote Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2021/22, nimetoa taarifa 10 za ukaguzi chini ya sekta hii kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 12**.

### **Miradi mingine**

Katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali ilitekeleza miradi mtambuka katika sekta mbalimbali, kama vile mazingira, utalii, uvuvi, sheria, kujenga uwezo, ulinzi wa mtoto na afua za maisha na kutokomeza umaskini. Miradi hii ilifadhiliwa na anuwai ya pande mbili na zaidi. Nimetoa ripoti 24 za ukaguzi chini ya sekta hii kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 21 and 22**.



# SURA YA PILI



**HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO  
YA KAGUZI ZILIZOPITA**

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji na hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli katika kutekeleza na mapendekezo ya ukaguzi. Kulikuwa na mapendekezo 2,938 kutoka taarifa za ukaguzi 290 zinazohusiana na miradi ya maendeleo. Mlipaji Mkuu wa Serikali alitoa mpango kazi wa kina wa kutekeleza mapendekezo hayo, ambayo inaoonesha dhamira thabiti ya kuboresha usimamizi wa fedha na udhibiti wa ndani. Mapendekezo yanalenga kushughulikia hitilafu zilizobainishwa wakati wa ukaguzi na kutoa suluhu kwa maboresho ya siku zijazo.

### 2.1 Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita

Katika **Jedwali Na. 3**, inaoneshwa kwamba kati ya mapendekezo 2,938 kutoka kwenye taarifa za ukaguzi zinazohusiana na miradi ya maendeleo, 37% yametekelezwa, 25% yanatekelezwa kwa sasa, 24% hayajatekelezwa, 10% yamejirudia, na 4% yamepitwa na wakati. Barua ya Menejimenti kwa kila mtekelezaji wa mradi zinatoa muhtasari zaidi wa hali ya utekelezaji na maendeleo yaliyofanyika kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi.

#### Jedwali Na. 3: Utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa za kaguzi zilizopita

Sekta	Jumla ya mapendekezo ya Miaka ya Nyuma	Mapendekezo yaliyo tekelezwa	Mapendekezo yanayօe ndelea kutekelezwa	Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa	Mapendekezo yaliyojirudia	Mapendek ezo yaliyopitwa na wakati
Kilimo	29	19	5	0	4	1
Elimu	299	117	105	25	35	17
Nishati na Madini	74	19	38	7	8	2
Afya	2,116	772	413	637	217	77
Usafirishaji	79	36	35	7	0	1
Maji	114	34	48	10	20	2
Jamii	99	30	36	16	11	6
Miradi Mchangane	128	57	34	10	6	21
Jumla	<b>2,938</b>	<b>1084</b>	<b>714</b>	<b>712</b>	<b>301</b>	<b>127</b>
Asilimia		37	25	24	10	4

Chanzo: Taarifa za ukaguzi za mwaka 2021/22

## 2.2 Hoja za ukaguzi zinazojirudia

Nimebaini hoja 12 za ukaguzi zinazojirudia katika sekta zote kwa miaka mitatu iliyopita (2019/20 hadi 2021/22) zinazohusiana na utoaji na matumizi ya fedha, usimamizi wa matumizi na ununuzi. Maelezo zaidi yanatolewa katika aya zifuatazo.

### 2.2.1 Matumizi ya fedha za miradi yasiyoridhisha

Nilibaini baadhi ya watekelezaji wa miradi walishindwa kutumia kiasi cha fedha ndani ya mwaka wa fedha, angalia **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Fedha ambazo hazijatumika**

Mwaka wa fedha	Watekelezaji wa Mradi	Fedha zilizosalia (Sh)	Asilimia ya fedha zilizosalia
2021/22	45	867,787,000,000	58%
2020/21	287	1,377,029,559,731	37%
2019/20	267	1,156,889,698,990.4	32%


**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi

Kutotumia fedha za miradi kwa kiwango kinachohitajika ndani ya muda uliokubaliwa kunapunguza juhudzi za serikali katika kutoa huduma na kufanya maendeleo kwa wananchi kwa kiwango kilichotarajiwa.

### 2.2.2 Bidhaa na huduma zilizonunuliwa pasipokupokelewa

Nilibaini kuwa watekelezaji wa mradi waliwalipa wazabuni mbalimbali wa bidhaa na huduma bila kupokelewa kwa bidhaa husika. **Kielelezo Na. 1** kinaonesha mwenendo wa miaka mitatu.

## Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa bidhaa zilizonunuliwa pasipo kupokelewa



Kielelezo hapo juu kinaonesha ongezeko la 1274% la bidhaa ambazo hazijapokelewa kutoka 2020/21. Hii inaonesha watekelezaji wa miradi kutokuwa na uangalizi mzuri na usimamizi wa miamala ya ununuzi. Hii inaweza kusababisha hasara ya kifedha na kudhoofisha utekelezaji wa malengo ya miradi.

### 2.2.3 Ununuzi wa bidhaa na huduma ambazo hazikupitishwa na bodi ya zabuni

Watekelezaji wa mradi walinunua bidhaa na huduma mbalimbali bila idhini ya bodi za zabuni, kinyume na Kifungu cha 35(2) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011, hivyo kupunguza ukomo wa uwazi na kusababisha hatari ya kutoa kandarasi kwa watoa huduma wasio na uwezo. **Jedwali Na. 5** linaonesha mwelekeo wa miaka mitatu.

#### Jedwali Na. 5: Mwenendo wa ununuzi bila idhini ya bodi ya zabuni

Mwaka wa fedha	Idadi ya Watekelezaji wa Mradi	Thamani ya bidhaa na huduma zilizonunuliwa(Sh.)	% Ongezeko/punguzo
2021/22	6	1,677,359,759	▲ 339.50% from 2020/21
2020/21	6	381,654,221	▼ 13.49% from 2019/20
2019/20	6	441,166,183	

Chanzo: Taarifa za ukaguzi

Napendekeza Serikali iandae mkakati wa kukabiliana na hoja zinazojirudia mara kwa mara kwa kuhuishwa taratibu, kutoa mafunzo na uelewa, kuimarisha mifumo ya udhibiti na kuwawajibisha watumishi wanaokiuka taratibu.

# SURA YA TATU



**UTENDAJI WA KIFEDHA NA USIMAMIZI WA  
MATUMIZI**

### **3.0 Utangulizi**

Sura hii inahusu ufadhili wa miradi, hati za ukaguzi zilizotolewa na matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa fedha, udhibiti wa ndani na masuala ya utawala katika kaguzi 290 za fedha zilizofanyika.

Kwa ujumla, sura hii inatoa taarifa muhimu ambazo serikali inaweza kutumia kufanya maamuzi sahihi kuhusu usimamizi wa kifedha, udhibiti wa ndani, na utawala ili kuboresha utendaji wa kifedha, kukuza uwajibikaji, na kuhakikisha uwazi katika kuripoti masuala ya kifedha.

#### **3.1 Ufadhili wa miradi**

Wafadhili wa miradi ya maendeleo ni Serikali ya Jumhuri ya Tanzania, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Programu ya Kimataifa wa Kilimo na Usalama wa Chakula (GAFSP), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA), Shirika la Maendeleo la Japani (JICA), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF), Mfuko wa Afrika wa Ustawi wa Pamoja (AGTF), Mfuko wa Maendeleo ya Afrika (ADF), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD), Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani (CDC), Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (OPEC), Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na UKIMWI (PERFAR), Shirika la Kimataifa la Upatikanaji wa Chanjo Dunia (GAVI), Serikali ya ufalme wa Norway na washirka wengine wa maendeleo.

Fedha zilizotolewa kwa kiasi kikubwa zilikuwa kwa mfumo wa misaada na mikopo, na sehemu hii inatoa maeleo kuhusu fedha zilizotolewa na kutumiwa na watendaji wa sekta zilizokaguliwa.

Uchambuzi wangu wa taarifa za kifedha 290 zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 unaonyesha kuwa miradi ilikuwa na jumla ya fedha inayopatikana ya Sh. trilioni 5.5. Sh. trilioni 3.0 zilitumiwa kwenye

kiasi hicho, na kusababisha salio la Sh. trilioni 2.5 mpaka ilipofika tarehe 30 Juni 2022.

### 3.1.1 Sekta ya kilimo

Katika mwaka 2021/22 miradi iliyokaguliwa ilifadhiliwa kwa kiasi kikubwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Programu ya Kimataifa ya Kilimo na Usalama wa Chakula (GAFSP), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Serikali ya Tanzania. **Jedwali Na. 6** linaonesha miradi iliyotekelizwa na kiasi cha fedha kilichotumika ukilinganisha na fedha zilizokuwepo katika sekta ya kilimo kama ilivyowasilishwa katika taarifa za fedha.

#### **Jedwali Na. 6: Miradi Iliyotekelizwa na fedha zilizotumika -sekta ya kilimo**

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Mradi wa Kituo Mahiri Afrika cha Teknolojia Bunifu za Udhibiti wa Panya na Uendelezaji wa wa Teknolojia za Unusaji [ACE IRPM&BTI]	Chuo /Kikuu cha Kilimo cha Sokoine	5,462.12	2,216.18	3,245.94
2	Kituo cha Umahiri cha Utafiti wa Kiimo, Sayansi ya Chakula na Usalama wa Lishe (CREATE)	Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST)	5,169.37	2,968.07	2,201.30
	Kuimarisha Ujuzi na Uwezo wa Mafunzo katika Mradi wa Sekta ya Kilimo cha Bustani	Baraza la Taifa la Elimu Ufundi (NACTE)	227.84	214.66	13.17
4	Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (TANIPAC)	Wizara ya Kilimo	16,092.09	15,473.99	618.10
5	Kituo cha Ubora cha Afrika kwa Magonjwa ya Kuambukiza ya Wanadamu na Wanyama Kusini naMashariki (SACIDS-ACE)	Chuo /Kikuu cha Kilimo cha Sokoine	4,744.02	2,514.49	2,229.52
6	Mradi wa kupambana na athari za UVICO 19 unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) - Tanzania	Wizara ya Kilimo	4474.23	4301.35	172.89
Jumla			36,169.67	27,688.74	8,480.92

**Chanzo:** Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoshishwa tarehe 30 Juni 2022

Moja ya mradi ya sekta ya kilimo wa Usimamizi wa Kiikolojia na Kilimo Endelevu cha Panya na Usalama wa Chakula barani Afrika (EcoRodMan), unaotekelawa na Chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine, ulikaguliwa kwa kipindi kinachoanzia tarehe 1 Februari 2021 hadi 31 Januari 2022. Hivyo, nimekutana na mafundisho wa kifedha wa mradi huu kutoka kwenye jedwali hapo juu. Kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Januari 2022, mradi ulikuwa na Sh. 829,754,675 ambapo kiasi cha Sh. 168,729,349 kilitumika na kubakiwa na salio la Sh. 661,025,326 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi zilizosalia.

### 3.1.2 Sekta ya Elimu

Katika Sekta ya Elimu, fedha zilipokelewa kutoka Benki ya Dunia, Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD) Kanada na Serikali ya Tanzania. **Jedwali Na. 7** linaonesha miradi iliyotekelawa na fedha zilizotumika ukilinganisha na fedha zilizokuwepo kulingana na taarifa za fedha zilizowasilishwa.

#### **Jedwali Na. 7: Miradi iliyotekelawa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Elimu**

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumi ka (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika Elimu ( EPforR)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	144,941.65	82,836.68	62,104.98
2	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - Chuo cha (EASTRIP) - DIT Dar es Salaam	Chuo cha Teknolojia - Dar es Salaam	8,880.62	1,733.86	7,146.76
3	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - (EASTRIP) - DIT Mwanza Campus	- DIT Mwanza Kampasi	10,471.40	1,853.61	8,617.78
4	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano	Chuo cha Taifa cha	10,403.04	5,314.62	5,088.41

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumi ka (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
	wa Kikanda wa Afrika Mashariki t Africa Skills for Transformation and Regional Integration (EASTRIP) - Chuo cha Taifa cha Usafirishaji	Usafirishaji			
5	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - (EASTRIP) - Chuo cha Ufundi Arusha	Chuo cha Ufundi Arusha	9,817.14	1,988.36	7,828.78
6	Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	70,840.81	26,624.84	44,215.97
7	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki (EASTRIP) - Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Makao Makuu - Dodoma	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	2,018.95	1,500.24	518.71
8	Ushirikiano wa Kimataifa Sekta ya Elimu - Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu awamu ya pili (GPE LANES II)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	45,162.10	45,162.10	0
9	Mradi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Afrika - Nelson Mandela (NM-AIST)	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Afrika - Nelson	898.37	872.12	26.26
10	Mradi wa Kusaidia Elimu kwa Walimu (TESP)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	25,339.69	15,960.37	9,379.32
11	Mradi wa Kuboresha Vyuo vyya Ualimu (UTC)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	4,452.89	4,446.89	6.00
12	Mradi wa Kuchochea Mageuzi ya Kiuchumi kupitia Elimu ya Juu (HEET)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	12,207.27	88.48	12,118.80
13	Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	Wizara ya Elimu Sayansi na	84,654.17	78,357.29	6,296.87

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
		Teknolojia			
14	Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	85,100	78,987	6,113
Jumla			515,188.10	345,726.46	169,461.64

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022

### 3.1.3 Sekta ya nishati na madini

Katika mwaka wa fedha 2021/22, miradi iliyo chini ya sekta ya nishati na madini ilipokea fedha kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD), Benki ya Maendeleo ya Ujeruman (KFW), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA), Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani (OFID), Jumuiya ya Ulaya (EU), na Serikali ya Tanzania. **Jedwali Na. 8** linaonesha miradi iliyotekelzwa, kiasi cha fedha kilichokuwepo ukilinganisha na kiasi cha fedha kilichotumika kama inavyoonekana kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa.

#### Jedwali Na. 8: Miradi iliyotekelzwa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Nishati na Madini

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Uwekezaji wa Miundombinu ya Msingi ya Kusafirisha Umeme awamu ya pili (BTIP)	Shirika la Umeme Tanzania	16,507.43	16,507.43	0
2	Mradi wa kusafirisha umeme na Uwekaji umeme Vijijini Bulyanhulu- Geita 220kv	Shirika la Umeme Tanzania	2,903.47	2,903.46	0.01
3	Mradi wa Kusafirisha Umeme Mkubwa na Uwekaji Umeme Vijijini - Geita- Nyakanazi 220kv	Shirika la Umeme Tanzania	30,181.27	29,290.13	891.15

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
4	Mradi wa Kuunganisha Umeme Kenya na Tanzania (KTPIP)	Shirika la Umeme Tanzania	82,824.73	80,574.17	2,250.55
5	Upembuzi Yakinifu wa Mradi wa Bwawa la Kikonge	Shirika la Umeme Tanzania	2,059.15	2,059.15	0
6	Mradi wa Kusafirisha Umeme Mkubwa na Uwekaji Umeme Vijijini - Geita- Nyakanazi 220kv	Shirika la Umeme Tanzania	29,928.53	29,357.78	570.75
7	Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo	Shirika la Umeme Tanzania	16,036.72	14,785.45	1,251.27
8	Mradi wa Ukarabati wa Kituo cha Umeme wa Nguvu ya Maji - Hale	Shirika la Umeme Tanzania	19,832.92	456.90	19,376.02
9	Wakala wa Nishati Vijijini - Mradi unaofadhliliwa na Benki ya Dunia	Wizara ya Nishati	331,461.41	4,724.51	326,736.90
10	Mradi Endelevu wa Nishati kwa Wote (SE4ALL)	Wizara ya Nishati	121.75	116.50	5.25
11	Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini - (SMMRP) II	Wizara ya Madini	563.98	522.88	41.10
12	Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia - Umoja wa Ulaya (TEITI) - EU	Wizara ya Madini	70.92	0.24	70.68
13	Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (Serikali ya Tanzania na CIDA) - (TEITI)	Wizara ya Madini	430.43	415.56	14.87
14	Mradi wa Kuunganisha Umeme Zambia na Tanzania (TAZA)	Shirika la Umeme Tanzania	271,752.76	7,739.78	264,012.97
15	Mradi wa Kuboresha na Kukarabati Gridi ya Umeme (TTGRUP)	Shirika la Umeme Tanzania	27,627.26	24.74	27,602.52
16	Mradi wa Maendeleo wa Nishati ya Jua - Shirika la Umeme Tanzania (TSDP)	Shirika la Umeme Tanzania	22,082.02	-	22,082.02
<b>Jumla</b>			<b>854,385</b>	<b>189,479</b>	<b>664,906</b>

**Chanzo:** Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoshishia tarehe 30 Juni 2022

Mradi wa Kuimarisha Uwajibikaji na Utawala Bora katika Tasnia ya Uziduaji (TEAGEP), ulikuwa na taarifa za fedha zinazojumuisha

kipindi cha takribani miezi sita kuanzia tarehe 18 Oktoba 2021 hadi tarehe 31 Marchi 2022. Hivyo utendaji wa kifedha wa miradi huu haukujumuishwa kwenye Jedwali hapo juu. Katika kipindi kilichoishia tarehe 31 Machi, 2022 mradi ulikuwa na jumla ya Sh. 856,960,387. Kati ya fedha hizo, Sh. 118,006,194 zilitumika, na kubaki na salio la Sh. 738,954,193.

### 3.1.4 Sekta ya afya

Katika mwaka wa fedha 2021/22, miradi iliyotekelwa chini ya sekta ya Afya ilipokea fedha kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denmaki (DANIDA), Benki ya Dunia, Kanada, Ireland, Shirika la Uhusiano wa Kimataifa la Korea Kusini (KOICA), Uswisi na Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norwei (NORAD), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani (CDC), Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Mradi wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI unaofadhiliwa na Mfuko wa Afya wa Kimataifa (Global Fund), Shirika la Kimataifa la Upatikanaji wa Chanjo Dunia na Serikali ya Tanzania. Fedha zilizotumika kutekeleza miradi kama inavyoonekana kwenye taarifa za fedha zinaoneshwa kwenye Jedwali Na. 9.

#### Jedwali Na. 9: Miradi iliyotekelwa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Afya

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Mfuko wa Afya -	Wizara ya Afya	6,329.29	6,133.54	195.75
2	Mradi wa Kusaidia Sekta ya Afya (HSPS)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	4,012.61	2,034.93	1,977.68
3	Mradi wa Kituo Mahiri cha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kwa Ajili ya Sayansi ya Matibabu ya Mishipya ya Moyo	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	133.80	113.57	20.22
4	Programu ya Kuimarisha Afya ya Msingi kwa Matokeo	Wizara ya Afya	12,908.13	12,908.13	-

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
5	Shirika la Dunia linalohusika na utaratibu wa Kutoa Chanjo (GAVI) - Msaada wa utoaji wa Chanjo ya UVIKO 19	Wizara ya Afya	26,809.55	13,482.43	13,327.12
6	Shirika la Dunia linalohusika na utaratibu wa Kutoa Chanjo (GAVI) - Programu ya Uimarishaji Mfumo wa Afya Awamu II (HSS2)	Wizara ya Afya	11,337.91	3,129.82	8,208.09
7	Mradi wa Ushirikiano katika Tafiti za Afya, Mafunzo na Uvumbuzi kwa ajili ya Programu ya Maendeleo Endelevu.	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	4,306.73	2,043.56	2,263.17
8	Mradi wa Kituo Mahiri cha Ufuatilajji na Tathmini ya masuala ya Afya (COEHME)	Chuo Kikuu cha Mzumbe	4,903.69	4,830.98	72.71
9	Mwitikio wa wagonjwa wa VVU chini ya Mfuko wa Dharura wa Kupambana na UKIMWI ((PEPFAR) - Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani	Wizara ya Afya	5799.15	4947.53	851.62
10	Programu ya Kuimarisha Afya ya Msingi kwa Matokeo (SPHC4R)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	3,234.17	3,017.68	216.49
11	Mfuko wa Afya	Mmlaka ya Serikali za Mitaa	90,124	75,063	15,061
Jumla			79,775.03	52,642.17	169,899

**Chanzo:** Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoshia tarehe 30 Juni 2022

Pia, nimekagua taarifa ya fedha ya programu inayojulikana kama “Utafiti katika Kujenga Uwezo wa Kupambana na Maradhi ya Selimundu (SPARCO)” unaotekelizwa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili chini ya mkataba wa ushirikiano Na. 2U24HL135881-05 kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Mei 2021 hadi 31 Aprili, 2022. Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Aprili 2022, jumla ya Sh. 1,858,821,410 zilikuwepo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za

mradi, kati ya hizo Sh. 826,681,289 zilitumika na kubaki Sh. 1,032,140,120 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi.

### 3.1.5 Sekta ya uchukuzi na mawasiliano

Katika mwaka wa fedha 2021/22, sekta ya uchukuzi na mawasiliano ilipokea fedha kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, Jumuia ya Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Japoni (JICA), Tume ya Umoja wa Afrika, Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DFID) na Serikali ya Tanzania. **Jedwali Na. 10** linaonesha miradi iliyotekelizwa; kiasi cha fedha kilichokuwepo ukilinganisha na kiasi cha fedha kilichotumika kama inavyoonekana kwenye taarfia za fedha zilizowasilishwa.

#### **Jedwali Na. 10: Miradi iliyotekelizwa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Uchukuzi na Mawasiliano**

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka(BRT) Awamu ya pili	Wakala wa Barabara	98,429.81	97,289.88	1,139.94
2	Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam (DMGP)	Mamlaka ya Bandari Tanzania	297,406.00	131,146.49	166,259.50
3	Programu ya Uboreshaji wa Miundombinu ya Usafirishaji Jijini Dar es Salaam (DUTP)	Wakala wa Barabara	140,553.16	55,559.09	84,994.07
4	Mradi wa Kimataifa wa Usafiri na Mawasiliano wa Ziwa Victoria (MLYMCT)	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)	275.29	262.84	12.45
5	Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa :Rumonge - Gitaza (45km) and Kabingo - Kasulu - Manyovu (260km)	Wakala wa Barabara	68,656.20	66,047.53	2,608.67
6	Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa: Bagamoyo - Horohoro /Lunga - Lunga Malindi Awamu ya Kwanza	Wakala wa Barabara	28,251.33	27,644.44	606.89

7	Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma kwa Kiwango cha Lami (112.3 KM)	Wakala wa Barabara	54,423.98	53,260.73	1,163.25
8	Maradi wa Tanzania wa Kidijitali (DTP)	Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknologia ya Habari	6,279.44	3,974.08	2,305.36
9	Maradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Awamu ya Kwanza	Wakala wa Barabara	32,637.80	31,194.60	1,443.20
10	Mradi wa Maendeleo wa Uboreshaji wa Njia ya Reli ya Kati (TIRDP)	Shirika la Reli Tanzania	92,792.53	37,815.02	54,977.51
11	Mfuko wa Miundombinu ya Reli (RIF)	Shirika la Reli Tanzania	854,020.88	388,481.72	465,539.16
12	Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji (TSSP)	Wakala wa Barabara	162,917.99	160,265.44	2,652.55
13	Mradi wa Maendeleo ya Jiji Kuu la Dar es Salaam (DMDP)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	114,643.58	112,965.56	1,678.02
14	Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Barabara katika Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE)	Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini	10,094.66	623.87	9,470.79
Jumla			961,382.65	1,166,531.29	794,851.36

**Chanzo:** Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoshia tarehe 30 Juni 2022

### 3.1.6 Sekta ya Maji

Katika mwaka 2021/22 , Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Misaada la Ujerumani (KfW) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na wafadhili wengine wa miradi ya maji nchini. **Jedwali Na. 11** linaonesha miradi iliyotekelizwa; kiasi cha fedha kilichokuwepo ukilinganisha na kiasi kilichotumika kama inavyoonekana kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa.

**Jedwali Na. 11: Miradi iliyotekelizwa na kiasi cha fedha kilichotumika - Sekta ya Maji**

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Mradi Endelevu wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Arusha (ASUWSDP).	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha	97,070.49	85,613.14	11,457.34
2	Kituo cha Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu kwa Matumizi ya Baadaye (WISE - FUTURES)	Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST)	8,122.50	4,343.78	3,778.72
3	Usafi wa Maji Shuleni (SWASH)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	8,593.68	8,378.78	214.91
4	Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji II - (WSSP II)	MoW and DAWASA	162,378.53	51,101.23	111,277.31
5	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijijini (SRWSSP)	Wizara ya Afya	28,520.90	28,377.77	143.13
6	Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) - Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira	Wizara ya Afya	140.12	70.51	69.60
7	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijijini -	Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini	195,816.24	114,663.28	81,152.96
8	Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira - Ziwa Viktoria (LV WATSAN)	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza	76,617.92	22,704.40	53,913.52
9	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijijini (SRWSSP) - Kitengo cha Uratibu	Wizara ya Maji	503,779.68	226,311.40	277,468.28
Jumla			1,081,040.07	541,564.29	539,475.78

**Chanzo:** Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoshia tarehe 30 Juni 2022

### 3.1.7 Sekta ya jamii

Katika mwaka wa fedha 2021/22, miradi ya sekta ya Jamii iliyokaguliwa ilifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Mfuko wa Bill na Melinda Gates (BMGF), Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Shirika la Kazi Duniani (ILO), Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa na Serikali ya Tanzania na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT). **Jedwali Na. 12** linaonesha miradi iliyotekelizwa; kiasi cha fedha kilichokuwepo ukilinganisha na kiasi kilichotumika kama inavyoonekana kwenye taarfia za fedha zilizowasilishwa:-

#### **Jedwali Na. 12: Miradi iliyotekelizwa na kiasi cha fedha kilichotumika - Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa**

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichot umika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya III - Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN II)	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)	544,929.11	432,436.15	112,492.96
2	Mradi wa Ustawi na Kuinua Sekta ya Utalii Kutokana na Athari za Ugonjwa wa UVIKO	Chama cha Waendeshaji Huduma za Kitalii - Tanzania (TATO)	1,368.64	1,324.97	43.66
3	Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Haki na Kulinda Haki za Binadamu Tanzania	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG)	438.27	412.21	26.06
4	Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Zanzibar	Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Zanzibar	229.59	219.38	10.21
5	Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Makapuni Madogo na ya Kati Kushindana Katika Masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa kwa Kuendana na Mnyororo wa Thamani	Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda	106.34	91.11	15.22
6	Mradi wa Nishati Endelevu kwa Wote	Wizara ya Nishati	128.95	78.25	50.69
7	Mradi wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori Tanzania Kwa Njia Shirikishi	Wizara ya Maliasili na Utalii (MoNRT)	1,021.46	660.63	360.83

		Idara ya Wanyamapori (WD)			
8	Ustawi wenyewe Tija na Ubunifu wa Kidijitali	Tume ya Utalii - Zanzibar	290.17	246.58	43.60
9	Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge Awamu ya Pili	Ofisi ya Bunge	361.22	361.22	-
10	Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Makapuni Madogo na ya Kati Kushindana Katika Masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa kwa Kuendana na Mnyororo wa Thamani	Wizara ya Uwekezaji, Vivanda na Biashara - Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania	0	0	0
Jumla			548,874	435,831	113,043

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaioishia tarehe 31 Desemba 2022

### 3.1.8 Miradi ya sekta mbalimbali

Katika mwaka wa fedha 2021/22, miradi ya sekta mbalimbali ilipokea fedha kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika na wadau wengine wa miradi ya maendeleo. **Jedwali Na. 13** linaonesha miradi iliyotekelizwa; kiasi cha fedha kilichokuwepo ukilinganisha na kiasi kilichotumika kama inavyoonekana kwenye taarifia za fedha zilizowasilishwa.

#### Jedwali Na. 13: Miradi iliyotekelizwa na kiasi cha fedha kilichotumika - sekta mbalimbali

Na.	Jina la Mradi	Mtekezeza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Mradi wa Maboresho wa Huduma za Mahakama na Utoaji wa Haki kwa Wananchi	Mahakama ya Tanzania	49,183.56	35,171.86	14,011.69
2	Msaada wa Maendeleo kwa Ukuaji Wa Takwimu Tanzania	Ofisi ya Takwimu ya Taifa	6,845.72	5,845.26	1,000.46
3	Mradi wa Uhamasishaji wa Raslimali za Ndani na Usimamizi Bora wa Maliasili (ISP DRM&NRG)-TPDC	Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	13,839.25	13,105.98	733.27
4	Mradi wa Maliasili Endelevu kwa Ukuaji (REGROW)- TANAPA	Shirika la Hifadhi za Taifa	62,340.05	3,959.50	58,380.55
5	Mradi wa Maliasili Endelevu kwa Ukuaji	Wizara ya Maliasili na	29,943.93	8,090.90	21,853.03

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
	(REGROW)	Utalii			
6	Kituo cha Kudhibiti Hewa ya ukaa Nchini (NCMC)	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	753.65	460.67	292.99
7	Mifumo ya Majengo bora, na Utafiti Unaofaa Tanzania (SIDA)	Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)	3,667.51	3,582.66	84.86
8	Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na Kuongeza Uhakika wa Chakula katika Maeneo Kame Tanzania (LDFS)	Ofisi ya Makamu wa Rais	5,982.49	2,363.90	3,618.59
9	ARU -SIDA Programu ya Ushirikiano wa Kufanya Tafiti	Chuo Kikuu cha Ardhi,	1,051.44	474.98	576.46
10	UDSM -SIDA Programu ya Ushirikiano wa Kufanya Tafiti	Chuo Kikuu cha Dar-es- salaam	4,544.76	2,946.05	1,598.71
11	Programu ya Usimamizi wa Afya ya Mazingira na Uchafuzi - Afrika	Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)	4,650.35	1,081.48	3,568.87
12	Local Climate Adaptive Living Mechanism (LoCAL) Project  Mradi wa Kuhimili Hali ya Hewa katika Mazingira ya Kawaida	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	70.90	20.95	49.95
13	Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia (NFAST)	Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)	4,645.89	3,408.35	1,237.54
14	Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)	Wizara ya Fedha na Mipango	7,589.43	7,370.52	218.91
15	Mradi wa Mikopo ya Nyumba - Benki Kuu ya Tanzania	Benki Kuu ya Tanzania	68,655.19	2,177.27	66,477.92
16	Mradi wa Kisasa wa Kuboresha Mfumo wa Kodi - Mamlaka ya Mapato Tanzania (TMP)	Mamlaka ya Mapato Tanzania	19,185.21	12,770.50	6,414.71
17	Mradi wa Kuwezesha Jamii Kupitia Mafunzo Kuhusu Usimamizi na Utunzaji wa Misitu	Taasisi ya Mafunzo ya Misitu (FTI)	839.93	833.73	6.19

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
	kwa Ushirikishwaji wa Wadau na Mabadiliko ya Tabaaanchi.				
18	Uwezeshaji wa Taasisi katika Masuala ya Hali ya Hewa na Taarifa za Hali ya Hewa kwa Ajili ya Mipango ya Maendeleo - Kaskazini mwa Tanzania	Ofisi ya Makamu wa Rais	2409.61	2408.56	1.06
19	Mradi Endelevu wa Kuwezesha Kuzuia na Kupambana na Rushwa - Tanzania (BSAAT)	Ofisi ya Makamu wa Rais	2982.67	2962.56	20.11
Jumla			289,181.54	109,035.68	180,145.87

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoshisha tarehe 30 Juni 2022

Miradi minne ya sekta mbalimbali ilitekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, ilikuwa na taarifa za fedha zilizojumuisha kipindi cha kuanzia tarehe 1 Januari 2021 hadi 31 Disemba 2021. Taarifa za utendaji wa kifedha zimeanishwa katika Jedwali Na. 14 hapo chini.

#### Jedwali Na. 14: Miradi iliyotekelze na kiasi cha fedha kilichotumika ya Ofisi ya Makamu wa Rais

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi Kilichopo (Sh. Milioni)	Kiasi Kilichotumika (Sh. Milioni)	Bakaa (Sh. Milioni)
1	Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR)	Ofisi ya Makamu wa Rais	3,779.77	3,757.64	22.13
2	Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa - Tanzania	Ofisi ya Makamu wa Rais	115.06	115.04	0.03
3	Mradi wa Kuongeza Uwezo Kitaifa kwa ajili ya Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA)	Ofisi ya Makamu wa Rais	2,641.79	14.31	2,627.48
4	Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Ikolojia kwa Ajili ya Kurejesha Mandhari ya Uhifadhi wa Bioanuwai nchini - Tanzania	Ofisi ya Makamu wa Rais	920.35	747.30	173.06
Jumla			7,457	4,634	2,823

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoshisha tarehe 31 Disemba 2021

Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Ukuaji wa Pamoja Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) unaosimamiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ulikaguliwa kwa kipindi cha miezi 15 kilichoishia tarehe 30 Septemba 2022. Kufikia tarehe 30 Septemba 2022, mradi ulikuwa na Sh. 6,753,426,900, kati ya kiasi kilichokuwepo, Sh. 6,752,710,174 zilitumika, na hivyo kubakiwa na kiasi cha Sh. 716,726.

### 3.2 Hati za ukaguzi

Hati ya ukaguzi inatolewa kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho inayotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, kama taarifa za fedha kwa ujumla wake zimeandalika kwa kuzingatia viwango vya taarifa za kifedha vinavyotumika (kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji Hesabu katika Sekta ya Umma IPSAS na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Kifedha). Hati hiyo imetolewa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI 1200).

Katika kufanya ukaguzi wa fedha za miradi ya maendeleo, ninatoa hati kulingana na mifumo ya taarifa za fedha inayotumika katika utayarishaji wa taarifa za fedha za hesabu za mwisho. Maeneo haya yanajumuisha uhakiki wa taarifa za fedha, udhibiti wa ndani na kuzingatia utekelezaji wa sheria na kanuni.

#### 3.2.1 Maoni ya ukaguzi yaliyotolewa juu ya taarifa za fedha

Katika mwaka wa fedha 2021/22, nilitoa nilitoa hati zinazoridhisha 287 na hati zenye mashaka tatu kama inavyooneshwaa katika **Jedwali Na. 15**.

**Jedwali Na. 15: Muhtasari wa Hati ya Ukaguzi zilizotolewa**

Sekta	Hati zilizotolewa				
	Hati inayoridhisha	Hati yenye mashaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya	Jumla
Kilimo	7	0	0	0	7
Elimu	13	1	0	0	14
Nishati na Madini	17	0	0	0	17
Afya	193	2	0	0	195
Jamii	10	0	0	0	10
Uchukuzi na Mawasiliano	14	0	0	0	14

Sekta	Hati zilizotolewa				
	Hati inayoridhisha	Hati yenye mashaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya	Jumla
Maji	9	0	0	0	9
Miradi Mingine	24	0	0	0	24
Jumla	287	3	0	0	290

Chanzo: Taarifa za fedha za mwaka wa fedha 2021/22


Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miaka mitano mfululizo yanaonesha mwelekeo unaoridhisha kuhusu miradi ya maendeleo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 16.**

#### Jedwali Na. 16: Mwenendo wa hati ya ukaguzi zilizotolewa

Mwaka wa Fedha	Hati zilizotolewa						Ju mla	
	Hati inayoridhish a		Hati yenye mashaka		Hati isiyoridhisha			
	Na.	%	Na.	%	Na.	%		
2021/2022	287	99	3	1	0	0	290	
2020/2021	293	100	-	-	-	-	293	
2019/2020	275	95	15	5	-	-	290	
2018/2019	441	97	13	3	1	0.22	455	
2017/2018	455	97	14	3	-	-	469	

Chanzo: Taarifa za ukaguzi za mwaka wa fedha 2021/22 na taarifa kuu ya miradi ya maendeleo yam waka uliopita

#### Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka mitano mfululizo



##### (a) Hati inayoridhisha

Hati inayoridhisha hutolewa pale ambapo taarifa za fedha zilizowasilishwa hazikuwa na upotoshaji pia ziliandaliwa kwa kufuata

mfumo ulioelekezwa, ikiwa ni pamoja na Sheria na Kanuni zinazokubalika. Katika mwaka wa fedha 2021/22 nimetoa hati zinazoridhisha sawa na 99% ya jumla ya hati zote zilizotolewa kwa Watekelezaji wa Miradi. Hati zinazoridhisha zimepungua kwa asilimia moja ukilinganisha na 100% zilizotolewa kwa mwaka wa fedha uliopita.

**(b) Hati yenyenye mashaka**

Hati hii hutolewa wakati nimejiridhisha kuwa kuna makosa kwenye taarifa za mwisho za fedha, ama moja moja au kwa ujumla wake. Hata hivyo, makosa yaliyobainika husababisha athari sehemu maalumu tu na si taarifa nzima ya fedha. Katika mwaka huu wa fedha nimetoa hati tatu zenyenye mashaka sawa na asilimia moja ya hati zote zilizotolewa kwa watekelezaji wa miradi; ikiwemo miradi miwili ya Mfuko wa Afya (inayotekelzeza na Halmashauri ya Kasulu na Shinyanga ) na maradi mmoja ulipo chini ya Wizara ya Elimu na Sayansi na Teknolojia (EPforR). Nimebaini kuwa Watekelezaji wa Miradi walipata hati zenyenye mashaka kutokana na kufanya matumizi yasiyo na viambatisho vinavyojitosheleza hivyo kuathiri mawanda ya ukaguzi kwa kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.

Ni maoni yangu kuwa kuwapo kwa matumizi yasiyo na viambatisho kunathibitisha udhaifu katika udhibiti wa matumizi na utunzaji wa kumbukumbu za hesabu ambapo unapelekea fedha za miradi kutumia kwa malengo yasiyokusudiwa. Hata hivyo, mwenendo wa utoaji wa hati zenyenye mashaka unaonesha ongezeko la asilimia mbili katika mwaka wa fedha 2021/22 ikilinganishwa na 2020/21.

**(c) Hati mbaya**

Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, kulingana na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa na yaliyoathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha hivyo kusababisha taarifa hizo kutokuwa sahihi. Hii inamaanisha kuwa tofauti na hati yenyenye shaka, taarifa za fedha zilizoandaliwa zina makosa makubwa yatokanayo na kutokukubaliana au kushindwa kukidhi mawanda; na makosa hayo hayajajikita sehemu moja bali yameathiri maeneo mengi katika taarifa za fedha na hivyo kuathiri kueleweka kwa taarifa hizo kwa

watumiaji wake kwa ajili ya kufanya maamuzi. Aidha, katika mwaka fedha 2021/22 sijatoa hati mbaya kwa Watekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**(d) Kushindwa kutoa maoni**

Mazingira ya ukaguzi yanaweza kusababisha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi. Hii inatoka pale ambapo nimeshindwa kupata ushahidi wa kutosha au taarifa muhimu ili kufikia malengo ya ukaguzi, na endapo madhara ya kushindwa kupata ushahidi au nyaraka hizo ni makubwa sana. Hivyo, ninaonesha kwenye ripoti yangu ya ukaguzi kuwa kutohana na ukubwa wa madhara yaliyopo au yanayoweza kutokea kutohana na kukosa ushahidi wa kutosha, nimeshindwa kutoa maoni ya ukaguzi. Aidha, katika mwaka fedha 2021/22 sijashindwa kutoa maoni kwenye taarifa za fedha nilizokagua.

**3.3 Tathimini ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi na mifumo ya utawala**

Sehemu hii inaonesha tathmini ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi na mifumo ya utawala uliowekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matokeo ya ukaguzi yameonesha mapungufu ambayo yanatia shaka juu ya uadilifu, uwazi na uwajibikaji ambao unaweza athiri uthibiti wa fedha na utoaji wa huduma.

**3.3.1 Hati ya Makubaliano isiyoidhinishwa inayohusu utekelezaji wa mradi wa MLVMCT**

Ukaguzi wangu wa mradi wa Kimataifa wa Usafiri na Mawasiliano wa Ziwa Viktoria (MLVMCT) unaotekelizwa na TASAC ulibaini kuwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika Mkutano wa kawada wa 14 uliofanyika tarehe 4 Septemba 2009, uliidhinisha ujenzi wa Kituo cha Utafutaji na Uokoaji cha Ziwa Victoria (MRCC) katika mkoa wa Mwanza.

Nilibaini kuwa,muda wa utekelezaji wa mradi huu ulikuwa wa miaka minne kuanzia Mei, 2018 hadi Mei, 2022 na washirka wa mradi huu walipaswa kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) itakayosimamia utekelezaji wa shughuli za mradi za kikanda. Hata hivyo, nilibaini kuwa hadi Novemba 2022 rasimu ya Hati ya Makubaliano kati ya

Tanzania na Uganda haikuidhinishwa licha ya Tume ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) kubaki mtekelezaji wa mradi huo.

Hii ilisababishwa na mchakato mrefu wa uhakiki wa rasimu ya Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya nchi washirika, kuhusiana na hili, malengo yaliyokusudiwa ya mradi hayakufikiwa kama inavyotarajiwa kwani imepelekea kuongezwa kwa muda wa utekelezaji wa mradi kutoka Mei 2022 hadi Aprili 2023.

**Ninapendekeza Serikali ya Tanzania na Uganda kuharakisha uhakiki wa rasimu ya Hati ya Makubaliano ili uidhinishwe kwa ajili ya utekelezaji bora wa mradi huu.**

### **3.3.2 Tume ya Bonde la Ziwa Viktoria inaendesha shughuli zake nje ya Nchi washirika wa Mradi**

Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wake wa kawaida wa 14 uliofanyika tarehe 4 Septemba 2009, likubali ujenzi wa Kituo cha Utafutaji na Uokoaji cha Ziwa Viktoria (MRCC) katika mkoa wa Mwanza. Mradi huu unatekelezwa na nchi ya Uganda na Tanzania tu.

Nilibaini ujenzi wa Kituo cha Utafutaji na Uokoaji cha Ziwa Viktoria haukutekelezwa hadi kufikia tarehe 25 October, 2022 hivyo mikutano inayoandaliwa na Tume ya Bonde la Ziwa Viktoria (LVBC) imekuwa ikifanyikia Kisumu, nchini Kenya.

Wakati huo huo, mradi huu kupitia Tume ya Bonde la Ziwa Viktoria umemwajiri mratibu wa mradi wa kikanda tangu mwaka 2020 ambae amekuwa akifanya kazi akitokea Kisumu, nchini Kenya kinyume na masharti ya mkataba wa ajira Na: LVBC/AFDB/IC/01/2021/22, ambao unaeleza kuwa kituo chake cha kazi ni mkoani Mwanza, Tanzania.

Kwa hivyo, TASAC inalipa gharama zaidi za fedha za kigeni kwa kuhudhuria mikutano Kisumu, nchini Kenya. Kwa upande mwingine, kufanyika kwa shughuli za mradi mbali na nchi washirika kunaweza kuchelewesha utekelezaji wake.

Ninapendekeza TASAC ihakikishe ofisi za Tume ya Bonde la Ziwa Viktoria (LVBC) na Tume pamoja na mratibu wa mradi vinahamia kwenye eneo la mradi kwa utekelezaji wa haraka wa mradi wa MLVMCT. Pia iharakishe ujenzi wa Kituo cha Utafutaji na Uokoaji cha Ziwa Viktoria mkoani Mwanza.

### 3.3.3 Mkataba kati ya TEA na MoEST bado haujafanyiwa mapitio ili kuweza kujumuisha mafunzo ya ubunifu na mafunzo ya mtandaoni (DLI 10.2)

Tarehe 17 Oktoba 2021, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (MoEST) walingia mkataba wa kutoa huduma na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) (Msimamizi wa fedha) kwa ajili ya usimamizi wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) ambao upo chini ya Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ).

Nimebaini kwamba mkataba wa kutoa huduma kati ya TEA na MoEST haujajumuisha kipengele cha programu na mafunzo ya Ubunifu na Mafunzo ya Mtandaoni (DLI 10.2), licha ya fedha kiasi cha Shilingi 1,160,575,895 kupokelewa na TEA tarehe 19 Januari 2022 ambayo ni sawa na asilimia 50 ya fedha za utekelezaji wa (DLI 10.2).

Hii ilisababishwa na mapitio ya mkataba wa kutoa huduma kutozingatiwa na MoEST na TEA. Pande zote mbili haziwezi kusimamia ipasavyo masuala ya utawala wa uendeshaji wa Mafunzo ya Ubunifu na Mafunzo ya Mtandaoni.

**Ninapendekeza TEA kushirikiana na MoEST kuititia upya mkataba wa huduma wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi ili kuweza kujumuisha Mafunzo ya Ubunifu na Mafunzo ya Mtandaoni (DLI 10.2).**

### 3.3.4 Kushindwa Kuunda Kitengo Kamili cha Utekelezaji wa Mradi

Kifungu cha IV, Sehemu ya 4.01(c) ya Mkataba wa Fedha wa Mwaka 2021 na Sehemu ya I.A.1(a) ya Ratiba ya Mkataba wa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Barabara katika Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE) ya Mwaka 2021 inahitaji ifikapo 19 Novemba 2021 baada ya siku 90 tangu tarehe ya kusaini mkataba ambayo ilikuwa 18 Agosti 2021, TARURA kuwa na Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi

("PIU") ambacho kitaongozwa na Mratibu wa Programu wa RISE wa kudumu akisaidiwa na wafanyakazi wenyewe sifa,uzoefu na ujuzi wa kutosha.

Nimebaini kwamba Mratibu wa mradi wa RISE aliyeeteuliwa hasimamii mradi huu kwa sababu pia anasimamia Mradi wa Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam (DMDP) na Mradi wa Kupendezesha Miji (TACTICS<sup>3</sup>) ambao ofisi yake iko mkoani Dar es Salaam. Kwa upande mwingine, nimebaini kuwa hadi kufikia Novemba 2022,wataalamu waliohitajika hawakuweza kuajiriwa ambao ni maafisa ugavi wawili,wataalamu wawili wa usalama barabarani, Mtaalam mmoja wa Jinsia, Mtaalam wa Mazingira na Jamii mmoja, Mtaalam wa Usimamizi wa Fedha mmoja, na msaidizi wa kiufundi mmoja.

Ukosefu wa wafanyakazi wenyewe ujuzi unaohitajika, wataalamu na mratibu wa mradi wa kudumu kunaweza kusababisha ufanisi duni katika utekelezaji wa mradi.

**Ninashauri mnejimenti ya TARURA kuhakikisha kuwa inaajiri mratibu wa mradi wa kudumu na wataalamu wanaohitajika katika mradi wa RISE.**

### **3.4 Usimamizi wa matumizi na bajeti**

Usimamizi wa matumizi ya umma unalenga kudhibiti usimamizi wa kifedha kwa watekelezaji wa miradi ili kuhakikisha ufanisi wa matumizi wa rasilimali za umma, kuimarisha uwajibikaji, na udhibiti kwa maslahi ya umma. Licha ya kuzingatia miongozo ya bajeti, sera, kanuni, waraka, sheria na kanuni. Nimebaini mapungufu katika udhibiti wa matumizi mbalimbali kama vile fedha za miradi zilizokopwa pasipo kurejeshwa, Kutowasilishwa kwa hati za malipo, uchangiaji usioridhisha wa Serikali kwenye miradi pamoja na riba iliyotozwa kwa ucheleweshaji wa malipo ya madai ya wakandarasi.Ninawasilisha mapendekezo yaliyotokana na mapugufu yaliyojitekeza katika mwaka wa fedha 2021/22.

---

<sup>3</sup> Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC) project.

### 3.4.1 Fedha za miradi zilizokopwa hazijarejeshwa Sh. bilioni 8.99

Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinaogozwa na makubaliano ya ufadhili wa kifedha ambayo inawataka watekelezaji wa mradi kuhakikisha fedha zinazotolewa zinatumika kikamilifu katika shughuli za mradi zilizopangwa.

Nilibaini kuwa kiasi cha Sh. 8,987,992,160.44 kutoka miradi mitano zilikopwa katika mwaka wa fedha 2021/22 bila kurudishwa kwenye miradi husika.Hii ni kinyume na matakwa yaliyopo kwenye hati za mradi husika, kama vile Mkataba wa Fedha, Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi, Hati ya Makubaliano (MoU) na miongozo mingine inayosimamia uendeshaji wa miradi. Sekta zilizohusika ni Elimu na Uchukuzi na Mawasiliano. Maelezo ya fedha zilizokopwa yanaonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 17** hapo chini.

**Jedwali Na. 17: Fedha zilizokopwa pasipo kurejeshwa**

Na.	Jina la Mradi	Sekta	Mtekeleza Mradi	Maelezo	Kiasi (Shs.)
1	Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma kwa Kiwango cha Lami (112.3 KM)	Uchukuzi na Mawasili ano	Wakala wa Barabara	Malipo ya fidia na ufunguzi wa mradi	594,386,100
2	Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	Elimu	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	Kufadhili miradi mingine kama ESPJ	80,782,102
3	Matokeo Makubwa Sasa katika Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (BRN (EPforR))	Elimu	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	Kufadhili mradi wa LANES	6,294,162,925
4	Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	Elimu	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	Matumizi mbalimbali ya Wizara ya Elimu	1,130,488,503
5	Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ)	Elimu	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	Kufadhili matumizi mbalimbali ya Wizara ya Elimu	888,172,530
<b>Jumla</b>					<b>8,987,992,160</b>

**Chanzo:** Hati za malipo

Hii ilitokana na mapungufu katika udhibiti wa ndani ukwenye usimamizi wa wa fedha za miradi. Kutokurejeshwa kwa fedha zilizokopwa kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za miradi hiyo.

Ninawashauri watekelezaji wa miradi kuhakikisha fedha zilizokopwa zinarejeshwa mara moja kwenye miradi husika ili kukwepa madhara ya kutotekelzeza kwa shughuli zilizopangwa.

### **3.4.2 Hati za malipo zenyenye thamani ya Sh. milioni 632.5 kutowasilishwa kwa ukaguzi**

Kanuni Na. 95(2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (zilizorekebishwa mwaka 2004) inataka kwamba, "taarifa ya hati za Malipo zilizoharibiwa au kupotea iripotiwe kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali ambae naye ataripoti kwa katibu Mkuu Kiongozi na kumpatia nakala ya taarifa hiyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali".

Katika Mwaka wa fedha 2021/22, Chuo cha Ualimu cha Sumbawanga kilipokea Sh. 3,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa chuo kipyakupitia mradi wa EP4R unaotekelzeza na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Mapitio ya taarifa za kibenki yalibaini kuwa kati ya fedha zilizopokelewa, Sh. 2,514,864,040 zilitumika. Aidha niliweza kuthibitisha matumizi yenye thamani ya Sh. 1,882,360,776 huku hati za Malipo zenyenye thamani ya Sh. 632,503,264 hazikuwasilishwa kwa Ukaguzi.

Nilibaini, hati za Malipo na viambatanisho vyake viliungua moto mnamo tarehe 25 Disemba 2021 hivyo kuzuia kufanyika kwa Ukaguzi kwenye Malipo hayo yaliyofanyika.

**Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Elimu kutoa taarifa rasmi kwa Mhasibu Mkuu wa Serkali pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya upotevu wa hati za Malipo na viambatanisho vyake na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa ikiwemo na kuwasilisha kwa taarifa ya uchunguzi wa tukio hili kwa Ukaguzi.**

### **3.4.3 Serikali kushindwa kuchangia sehemu yake ya fedha za miradi Dola za Kimarekani milioni 6.24 (Sh. bilioni 14.3)**

Makubaliano ya mkopo yaliyosainiwa tarehe 23 Mei 2015 kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika yanahitaji Serikali kuchangia sehemu yake ya fedha za kigeni na fedha za kitanzania kwenye mradi Endelevu wa Usambazi Maji Safi na Usafi wa Mazingira wa Mjini Arusha (ASUWSDP).

Nilibaini gharama jumla ya mradi ilikuwa Dola za Kimarekani 233,915,581 ambapo Serikali ya Tanzania ilihitajika kuchangia sehemu yake ya kifedha Dola za Kimarekani 22,953,000 (Sh. 52,565,893,285.50) kwa Kipindi chote cha mradi. Ukaguzi zaidi ulibaini kwamba hadi tarehe 30 Juni, 2022, mchango wa Serikali ya Tanzania ulipaswa kufikia asilimia 80 sawa na Dola za Kimarekani 18,499,783.32 (Sh. 42,367,343,519.54), hadi kufikia wakati wa Ukaguzi mwezi September, 2022 Serikali ya Tanzania iliweza kuchangia Dola za Kimarekani 12,256,106.45 (Sh. 28,068,365,082.84). Hivyo kulikuwa na deni la mchango wa Serikali lenye thamani ya Dola za Kimarekani 6,243,676.87 (Sh. 14,298,978,437) licha ya kwamba mradi unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2023.

Ucheleweshaji wa Serikali kutoa mchango wake kunaweza kusababisha mkwamo katika utekelezaji shighuli za mradi na hivyo kutofikiwa kwa malengo yake.

**Ninapendekeza menejimenti ya ASUWSDP ifuatilie upatikanaji wa kiasi cha fedha kilichosalia kutoka kwa Serikali, pamoja na kuikumbusha Serikali mara kwa mara juu ya wajibu wake katika utekelezaji wa mradi kulingana na matakwa ya makubaliano ya mkopo.**

### **3.4.4 Kuchelewa kulipa fidia kwa waathirika wa miradi Sh. bilioni 11.37**

Kifungu Na. 52(8) cha Sheria ya Upimaji na Usajili wa Wapima Ardhi ya mwaka 2016 kinahitaji malipo ya fidia kwa waathirika wa miradi kufanyika kwa haraka ndani ya miezi sita tangu kuthibitishwa kwa taarifa ya tathmini ya fidia. Kinyume na hivyo fidia italipwa na riba

kwa kiwango kinacholipwa na benki za kibashara kwa amana za kudumu. Aidha, Kifungu Na. 52(2) kinabainisha kwamba ripoti ya tathmini kwa ajili ya fidia inaruhusiwa kutumika katika muda wa miaka miwili tangu tarehe ya kuthibitishwa kwa ripoti hiyo.

Mapitio yangu ya ripoti za tathmini zilizotolewa tarehe 07 Septemba 2021 kwenye mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa: Bagamoyo - Horohoro /Lunga - Lunga Malindi unaotekelawa na Wakala wa Barabara yalibaini kuwa fidia ya Sh. 512,341,000 haikulipwa kwa waathirika wa mradi 422. Hii ilitokana mchakato mrefu wa Malipo ya fidia kwa waathirika wa miradi.Kushindwa kulipa fidia kwa waathirika wa mradi ndani ya miezi sita, Serikali inaweza kulipa riba ikiwa kiasi hicho kitabaki bila kulipwa.

Nilibaini,mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka(BRT) Awamu ya pili unaotekelawa na Wakala wa Barabara ulikuwa na madai ya fidia yenye thamani ya Sh. 4,630,330,823 kwa waathirika 15 wa mradi kwa zaidi ya miaka miwili.

Mapitio zaidi ya ripoti za tathmini za mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Msalato unaotekelawa na Wakala wa Barabara yalibaini madai ya fidia kwa waathirika 1,039 wa miradi yenye thamani ya Sh. 6,227,732,598.11 ikijumuisha madai halisi Sh. 3,927,262,940 na riba ya madai yenye thamani ya Sh. 2,300,469,659.Kuchlewesha malipo ya fidia kwa waathirika wa miradi kunasababisha Serikali kulipa riba isiyostahili ya ucheleweshaji ambayo ingeweza kupeukwa kwa kulipa fidia kwa wakati kulingana na ripoti ya tathmini ya mwaka 2011.

**Ninapendekeza Wakala wa Barabara kuharakisha Malipo ya fidia kwa waathirika wa miradi yenye thamani ya Sh. 11,370,404,421 kwa waathirika wa miradi 1,476.**

### **3.4.5 Hundu zilizotolewa kwa waathirika wa miradi kutowasilishwa benki Sh. milioni 352.12**

Kifungu cha 162(1) cha Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (Zilizorekebishwa 2004) kinahitaji kulinganishwa kwa taarifa za kibenki na daftari la fedha husika kila mwezi. Aidha, hundi iliyochacha hutambuliwa ikiwa haijawasilishwa benki kwa Malipo

kwa siku zinazozidi 180 au miezi sita. Hundi iliyochacha huwa haiwezi kulipwa na benki.

Ukaguzi wangu ulibaini hundi zilizochachacha zilizotolewa kwa waathirika wa miradi zenyet thamani ya Sh. 352,128,273.60 katika miradi miwili ambayo ni mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Msalato na mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma kwa Kiwango cha Lami (112.3 km). Hii ilisababishwa na uwepo wa malalamiko na migogoro baina ya waathirika wa miradi ambayo ilisababisha kutochukua hundi hizo zilizoandikwa kwao kwa ajili ya Malipo. Kwa upande mwingine, kulikuwa na mawasiliano yasioyordhisha kati ya watendaji wa mradi na waathirika wa miradi kuhusu kuhamasisha uchukuaji wa hundi hizo za Malipo.

Ninaamini kuwa hundi zilizochachacha zilisababisha fedha kurerejeshwa kwenye akaunti za benki za miradi hivyo zinaweza kusababisha matumizi ya fedha hizo kwenye shughuli zisizopangwa.

**Ninapendekeza Wakala wa Barabara kuwasiliana na waathirika wa miradi na kuwapatia hundi zao kwa wakati bila kuchelewa zaidi.**

### **3.4.6 Kutolipwa kwa fedha za washiriki wamiradi ya ajira za muda Sh. bilioni 2.42**

Katika Mamlaka tano za maeneo ya utekelezaji (PAAs) zilizopo ndani ya mikoa mitano, washiriki katika Miradi ya Ajira za Muda (PWP) hawakulipwa haki zao kiasi cha Sh. 2,421,930,900 kwa mwezi Oktoba na Novemba 2021 kutokana na kutoolewa kwa fedha hizo kutoka Makao Makuu ya TASAF. Hii ni ukiukwaji wa kifungu 2.2 cha Mwongozo wa Uendeshaji wa TASAF III, 2019, ambao unataka watu wanaoshiriki katika kazi za miradi ya ajira za muda kwa miezi minne kulipwa kwa wakati.

Kutowasilishwa kwa fedha kumezuia walengwa wa mradi kunufaika na faida ya mradi kwa wakati.

**Ninapendekeza TASAF kuhakikisha fedha zilizobaki zinatolewa kwa walengwa husika bila kucheleweshwa zaidi.**

### 3.4.7 Riba iliyotozwa kwa Ucheleweshaji wa Malipo ya madai ya wakandarasi Sh. bilioni 2.84

Kifungu Na. 14.7 (c) na 14.8.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinabainisha kuwa "ikiwa mkandarasi hatolipwa ndani ya siku 56 baada ya Mhandisi kupokea hati za madai za kuthibitisha, atastahili kulipwa riba ambayo inazidishwa kila mwezi kwa kiasi kilichocheleweshwa kulipwa.

Mapitio yangu yalibaini miradi saba ya Sekta ya Maji na Sekta ya Uchukuzi na Mawasiliano ilikuwa na madai ya riba Kiasi cha Sh. bilioni 2.84 kutohana na kucheleweshwa kwa malipo ya Hati za Malipo ya Wakandarasi (IPCs). Maelezo zaidi yanapatikana kwenye **Jedwali Na. 18** hapo chini:

#### **Jedwali Na. 18: Madai ya tozo**

Na.	Jina la Mradi	Sekta	Watekelezaj i wa mradi	Kiasi (Shs.)
1	Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka(BRT) Awamu ya pili	Uchukuzi	Wakala wa Barabara Tanzania	649,549,367
2	Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji (TSSP)	Uchukuzi	Wakala wa Barabara Tanzania	201,350,096.96
3	Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa :Rumonge - Gitaza (45km) and Kabingo - Kasulu - Manyovu (260km)	Uchukuzi	Wakala wa Barabara Tanzania	129,759,425.10
4	Programu ya Uboreshaji wa Miundombinu ya Usafirishaji Jijini Dar es Salaam (DUTP)	Uchukuzi	Wakala wa Barabara Tanzania	141,844,115.49
5	Mradi wa Maendeleo ya Jiji Kuu la Dar es Salaam (DMDP)	Uchukuzi	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	277,431,909.40
6	Mradi Endelevu wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Arusha (ASUWSDP).	Maji	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha	564,816,794.21
7	Barabara ya Mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma kwa Kiwango cha Lami (112.3 km).	Uchukuzi	Wakala wa Barabara Tanzania	879,261,914
<b>Jumla</b>				<b>2,844,013,622.16</b>

**Chanzo:** Hati za malipo

Kuchelewa kulipa madeni ya Wakandarasi kulitokana na mchakato mrefu wa kuidhinisha Malipo kutohana na mfumo wa malipo wa "D-

Fund” ulioanzishwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Malipo ya Riba kwa mfadhili wa mradi huu (AfDB) anayatambua kama Malipo yasiyostahili hivyo inaleta mzigo kwa Serikali ya Tanzania kulipa fedha hizo kwa mfadhili. Kwa upande mwingine, kuchelewesha kulipa wakandarasi kumeathiri utekelezaji wa mradi kwa kwa wakati.

Ninashauri Wakala wa Barabara kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia upya mchakato wa malipo kwa wakandarasi ili kupata njia nzuri na yenye ufanisi ya kulipa wakandarasi ili kuepuka uchumi wa riba kutokana na kuchelewesha kulipa madai yaliyosalia.

### **3.4.8 Kushindwa Kurejesha Fedha zilizosalia kwenda Benki ya Dunia Sh. milioni 724.71**

Mapitio yangu ya Mradi wa Kuimarishe Uwajibikaji na Utawala Bora katika Tasnia ya Uziduaji (TEAGEP), uliotekelawa na Wizara ya Madini yalibaini kwamba mradi huo ulipangwa kufungwa tarehe 31 Machi 2022 na kiasi cha Sh. 724,714,193 kilibaki bila kutumika. Licha ya mchakato wa urejeshaji fedha kuanza tarehe 15 Julai, 2022 lakini hadi wakati wa Utaguzi hii tarehe 31 Julai 2022 kiasi hiki hakikurejeshwa kwa Benki ya Dunia licha ya mchakato wa urejeshaji kuanzishwa 15 Julai 2022. Hii ni kinyume na Kifungu 5.4.3 cha Mwongozo wa Utekelezaji wa Mradi wa Mwaka 2020 ambacho kinahitaji kiasi kilichosalia mwishoni mwa mradi kurejeswa kwenda Benki ya Dunia.

Hii ilisababishwa na kucheleweshwa kufikia makubaliano juu ya kuongezwa kwa muda wa utekelezaji wa mradi. Kushindwa kutekeleza masharti yaliyokubaliwa kunaweza kuiharibia sifa Serikali.

**Ninapendekeza menejimenti ya TEAGEP kuharakisha mchakato wa kurejesha kiasi kilichosalia kwa Benki ya Dunia.**

### **3.4.9 Kushindwa kurejesha kiasi cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) iliyolipwa na mkandarasi Sh. milioni 562.74**

Kanuni Na. 4(1-8) ya Kanuni ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) (Taratibu za Ufuatiliaji wa Msamaha) ya mwaka 2018 inataka maombi ya msamaha wa Kodi kufanywa na Taasisi Nunuzi ndani ya siku 30 kabla ya kunza kwa Utekelezaji wa mradi. Aidha, kifungu Na. 6.04 cha Makubaliano ya Mkopo kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mfuko wa Kuongeza Ukuaji Barani Afrika (AGTF) kinahitaji Serikali ya Tanzania kutoa msamaha wa kodi, ushuru wote na tozo zinazohusiana na uagizaji wa bidhaa nje ya nchi na ununuzi wa bidhaa na huduma zinazonunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.


Ukaguzi wangu wa Mradi wa Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) (Awamu ya pili) unaotekelizwa na Wakal wa Barabara umebaini kuwa kati ya Januari 2021 na Aprili 2021 kodi ya ongezeko la thamani yenye thamani ya Sh. 562,743,931.79 ililipwa na mkandarasi wakati wa Ununuzi wa bidhaa. Licha ya kuahidiwa kurejeshewa kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa, mkandarasi huyo alikuwa hajarejeshewa kiasi hicho hadi kufikia Oktoba 2022, licha ya kuongeza madai ya kurejeshewa fedha hizo ambazo aliomba kurejeshewa kupitia barua yenye kumbukumbu namba SHC/BRT/BT&AP/2022/1365 iliyotumwa tarehe 31 Januari 2022.

Kuchelewa kuomba msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kuathiri utekelezaji wa mradi kwa upande wa gharama na muda.

**Ninapendekeza Wakala wa Barabara kuhakikisha maombi yanafanyaika mapema ili kupata tangazo la Serikali ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani ndani ya wakati unaofaa.**



**SURA YA NNE**



**USIMAMIZI WA UNUNUZI**

---

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea mapungufu yaliyobainika katika usimamizi wa manunuzi katika miradi ya maendeleo.

### 4.1 Maoni ya ukaguzi kuhusu uzingatiaji wa sheria

Kifungu cha 48(3) cha Sheria za Ununuzi ya Umma ya 2011 kinanitaka nieleze katika ripoti yangu ya mwaka kama Taasisi iliyokaguliwa imefuata au kutofuata taratibu zilizowekwa katika Sheria ya Ununuzi ya Umma na Kanuni zake. Ninazingatia hitaji hili katika kila ripoti ya ukaguzi wa taarifa za fedha za hesabu za mwisho za taasisi iliyokaguliwa. Kwa hiyo, katika mwaka wa fedha wa ukaguzi, nimefanya kaguzi za fedha 290 ambapo nimetoa maoni kama watekeleza miradi wamefuata Sheria ya ununuzi na kanuni zake. Nimebaini watekeleza miradi 208 walizingatia sheria ilhali watekeleza miradi 82 walikutwa na mapungufu kwenye kuzingatia sheria kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 19** hapo chini.

**Jedwali Na. 19: Maoni katika kuzingatia sheria za ununuzi**

Sekta	Taasisi zilizozingatia (idadi)	Idadi ya taasisi zilizobainika na mapungufu	Jumla
Kilimo	6	1	7
Elimu	5	9	14
Nishati na Madini	15	2	17
Afyah	140	55	195
Uchukuzi na Mawasiliano	10	4	14
Maji	5	4	9
Jamii	8	2	10
Miradi Mingine	19	5	24
Jumla	208	82	290

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi 2021/22

Muhtasari wa matokeo muhimu yaliyopatikana wakati wa ukaguzi ni kama inavyoiezwa hapo chini.

#### **4.2 Mikataba yenyе thamani ya Sh. bilioni 2.51 kutopitiwa na Maafisa Sheria**

Kanuni ya 60 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama kilivorekebishwa na Kanuni ya 3 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma zilizorekebishwa mwaka 2016 (Tangazo la Serikali 121), inataka mwanasheria wa taasisi nunuzi kupitia mikataba yoyote rasmi inayotokana na kukubali zabuni yenyе thamani chini ya Sh. Bilioni 1 kabla ya kusainiwa na pande husika.

Nimebaini kwamba mtekelezaji mmoja wa miradi katika miradi minne alisaini mikataba na mafundi yenyе thamani ya Sh. bilioni 2.51 kabla ya kuhakikiwa na Wanasheria, kama ilivyoinishwa katika **Jedwali Na. 20** hapa chini.

#### **Jedwali Na. 20: Maelezo yanayoonesha mikataba ambayo haijapitiwa**

Mtekelezaji	Mradi	Kiasi (Sh.)
Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	Matokeo Makubwa Sasa katika Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (EPforR)	695,532,356
Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	Programu ya Elimu na Uujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ)	996,707,689
Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia	Usafi wa Maji Shulen (SWASH)	80,820,606
Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	736,620,000
Jumla		2,509,680,651

**Chanzo:** Kulingana na taarifa iliyopatikana katika faili za miradi

Udhibiti wa ndani usioridhisha katika usimamizi wa mikataba umepelekea kusaini mikataba na mafundi (local artisans) yenyе thamani ya Sh. bilioni 2.51 bila kupitiwa na wanasheria, hali inayopelekea kuongezeka kwa hatari za kisheria kwa watekelezaji wa miradi.

**Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha** kuwa wanasheria wanapitia mikataba yote kabla ya kusainiwa ili kuepuka migogoro ya kisheria inayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa miradi.

#### **4.3 Manunuzi ya Sh. milioni 506.76 yalifanyika bila kuiarifu bodi za zabuni**

Kanuni ya 166(7) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inataka manunuzi yote madogo yatolewe taarifa kwenye bodi za zabuni kila mwezi na mwenye mamlaka ya kuteua, kwa kutumia fomu sahihi ya utaratibu iliyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi (PPRA).

Nilibaini kuwa watekelezaji nane walifanya manunuzi madogo yenye thamani ya Sh. milioni 506.76 bila ya kuripoti kila mwezi katika bodi zao za zabuni husika kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 21** hapa chini.

#### **Jedwali Na. 21: Manunuzi ambayo hayajariptiwa kwa Bodi za Zabuni**

Mtekelezaji	Mradi	Kiasi(Sh.)
Chuo cha Taifa cha Usafirishaji(NIT)	Mradi wa kujenga ujuzi kwa maendeleo na uingiliano wa kikanda katika Afrika Mashariki (EASTRIP)	110,356,368
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Matokeo Makubwa Sasa katika Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (EPforR)	61,428,887
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Programu ya Elimu na Uujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji(ESPJ)	48,133,500
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (LANES II)	53,909,092
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Mradi wa Kusaidia Elimu kwa Walimu (TESP)	69,806,768
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	28,754,500
Halamshauri ya Wilaya ya Ilaje	Mfuko wa Uchangiaji wa Afya(HBF)	37,564,632
Halamshauri ya Mji Tunduma	Mfuko wa Uchangiaji wa Afya(HBF)	31,316,244
Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)	Mradi wa Kuwezesha Barabara na Fursa za Kiuchumi na Kijamii (RISE)	65,498,120
Jumla		506,768,111

**Chanzo:** Hati za malipo zikilinganishwa na mihtasari ya vikao vya Bodi za Zabuni

Uwepo wa uelewa usiojitosheleza wa Kanuni za manunuzi madogo ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (Iliyorekebishwa 2016) kama kisingizio cha kufanya manunuzi kwa njia ya fedha taslimu ili kuepuka kufuata taratibu za kawaida za manunuzi kwa ushindanishi. Kutoripoti manunuzi madogo kunakiuka uadilifu, uwazi na uwajibikaji wa kanuni za manunuzi na kuzuia bodi ya zabuni kufanya kazi ya kupitia na kuchunguza.

Ninapendekeza kuwa taasisi nunuzi ziripoti manunuzi madogo yote kwa bodi za zabuni kila mwezi kwa ajili ya kupitiwa.

#### 4.4 Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mfumo wa Ununuzi wa Kieletroniki Tanzania (TANePS) Sh. bilioni 14.92

Kanuni ya 342 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 na Waraka Na. 4 wa Wizara ya Fedha na Mipango wa mwaka 2019 inataka taasisi nunuzi kutumia mfumo wa ununuzi wa kieletroniki Tanzania (TANePS) katika manunuzi ya bidhaa na huduma kuanzia tarehe 1 Januari 2020.

Nimebaini manunuzi ya bidhaa na huduma yenyeye thamani ya Sh. bilioni 14.92 yaliyofanyika nje ya mfumo wa ununuzi wa Kieletroniki Tanzania (TANePS) kama ifuatavyo; watekelezaji watatu katika Sekta ya Elimu (Sh. bilioni 10.95), mmoja katika Sekta ya Kilimo (Sh. bilioni 3.16), mmoja katika Sekta ya Jamii (Sh. milioni 635.17) na wanne katika Sekta ya Afya (Sh. milioni 173.41). Maelezo yameoneshwa katika **Jedwali Na. 22** hapo chini.

**Jedwali Na. 22: Manunuzi yaliyofanyika nje ya TANePS**

Sekta	Mtekelezaji	Mradi	Kiasi (Sh.)
Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Mradi wa kujenda ujuzi kwa maendeleo na uingiliano wa kikanda katika Afrika Mashariki (EASTRIP)	35,430,450
Elimu	NACTE	Mradi wa kujenda ujuzi kwa maendeleo na uingiliano wa kikanda katika Afrika Mashariki (EASTRIP)	32,490,000
Elimu	NIT	Mradi wa kujenda ujuzi kwa maendeleo na uingiliano wa kikanda katika Afrika Mashariki (EASTRIP)	102,328,804
Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Matokeo Makubwa Sasa katika Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (EPforR)	412,338,604
Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Programu ya Elimu na Uujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ)	1,618,076,821
Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Mpango wa Kukuzza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (LANES II)	882,154,200
Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP)	7,330,996,113
Elimu	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Mradi wa Kusaidia Elimu kwa Walimu (TESP)	540,274,099

Sekta	Mtekelezaji	Mradi	Kiasi (Sh.)
Kilimo	Wizara ya Kilimo	Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD)	3,159,481,975
Jamii	Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)	Msaada wa Maendeleo kwa Takwimu za Tanzania (DSTS)	635,170,400
Afya	OR-TAMISEMI	Programu ya Sekta ya Afya ya Msaada (HSPS)	39,625,077
Afya	Halmashauri ya Wilaya ya Handeni	Mfuko wa Uchangiaji wa Afya (HBF)	70,563,860
Afya	Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi	Mfuko wa Uchangiaji wa Afya (HBF)	25,932,713
Afya	Halmahsuri ya Wilaya ya Mkinga	Mfuko wa Uchangiaji wa Afya (HBF)	37,286,444
Jumla			14,922,149,560

**Chanzo:** Daftari la Fedha na Mfumo wa Ununuzi wa Kieletroniki Tanzania

Hali hii ilitokana na ukosefu wa mafunzo ya kutumia mfumo wa ununuzi wa kieletroniki Tanzania (TANePS) na muitikio wa mfumo usioridhisha wakati wa kuingiza nyaraka na matangazo. Kutoweza kutumia TANePS kunapunguza ufanisi, uwazi, na usawa na hivyo kurefusha taratibu za mchakato wa manunu.

Napendekeza watekelezaji wa mradi husika, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kuwapa mafunzo watumishi jinsi ya kutumia mfumo na kuboresha uingizaji wa nyaraka na matangazo kwa wakati.

#### 4.5 Ucheleweshaji wa ununuzi wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.66 kwa kipindi cha miezi 20

Tarehe 14 Aprili 2021 OR-TAMISEMI ilipokea kiasi cha Sh. 4,860,000,000 kupitia mradi wa Mpango wa Kuimarisha Sekta ya Afya (HSPS) ambapo kiasi cha Sh. 3,200,000,000 kilipangwa kutumika kwa ajili ya mafunzo ya Anastasia na kiasi cha Sh. 1,660,000,000 kilipangwa kutumika kwa ajili ya kununua mashine za usingizi “CEmONC Facility” na vifaa tiba vingine.

Tarehe 21 Juni 2022, OR-TAMISEMI ilisaini mkataba Na. ME/022/2021/2022/HQ/G/27 na M/s Lab Equipment Limited kwa bei ya Sh.4, 305,974,966 bila ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa ajili ya manunu ya vifaa tiba na vifaa vingine kwa ajili ya vituo vya afya na zahanati. Kati ya bei ya mkataba wa Sh.4,305,974,966, kiasi cha Sh.1,660,000,000 kilijumuishwa kwenye bei ya mkataba kwa ajili ya ununuzi wa mashine 32 za usingizi (Universal Anesthesia machines

AM 834 Eternity) na vifaa tiba vingine kwa fedha za mradi Mpango wa Kuimarisha Sekta ya Afya (HSPS). Mkataba ulianza tarehe 21 Juni 2022 na ulipangwa kukamilika tarehe 21 Septemba 2022.

Hadi wakati wa ukaguzi mwezi Novemba 2022, takribani miezi 20 tangu kupokea fedha, mashine za usingizi “CEmONC Facility” na vifaa tiba vingine yenye thamani ya Sh. 1,660,000,000 kwa fedha za mradi wa Mpango wa Kuimarisha Sekta ya Afya (HSPS) zilikuwa bado hazijapokelewa kama ilivyotarajiwa.

Hii ilisababishwa kwa kiasi kikubwa na mchakato mrefu wa manunuzi kwani mchakato ulianza tarehe 1 Januari 2022 wakati fedha zilikuwa zimepokelewa tarehe 14 Aprili 2021 hii inadhihirisha kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa takribani miezi nane tangu fedha zilivyopokelewa. Kuchelewesha kufanya manunuzi ya vifaa tiba kunapelekeja jamii kutopata huduma za matibabu zilizokusudiwa.

**Napendekeza kuwa menejimenti ya OR-TAMISEMI iharakishe upatikanaji wa vifaa tiba ili kupunguza athari ya kuchelewesha kupata faida zilizotarajiwa kwa jamii iliyokusudiwa.**

#### **4.6 Kuanzisha utekelezaji wa shughuli za miradi ya EPforR yenye thamani ya Sh. bilioni 3.82 bila ya kuhusisha mpango wa manunuzi**

Mapitio yangu ya mafaili ya mradi wa Matokeo Makubwa Sasa katika Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (EPforR) umeonesha kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa 17 zilianzisha utekelezaji wa shughuli za mradi wa EPforR yenye thamani ya Sh. 3,820,160,743 kwa njia ya ununuzi ya “force account” bila kuhusisha mipango ya manunuzi kinyume na Aya ya 8.1 ya Mwongozo uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma(PPRA) kwa njia ya ununuzi ya “Force Account” uliotolewa mwezi Mei 2020, ambapo kazi zote za mradi zinapaswa kutekelezwa ikiwa zipo kwenye bajeti na kuingizwa katika Mpango wa manunuzi wa kila mwaka. **Jedwali Na. 23** hapa chini linatoa maelezo zaidi.

## Jedwali Na. 23: Miradi iliyoanza kutekelezwa bila ya kuwepo kwenye mpango wa manunuizi

Na.	Halmashauri	Idadi ya Shule	Jina la Mradi	Kiasi (Sh.)
1	H/W Meru	1	Ujenzi wa maabara na nyumba	187,404,421
2	H/W Kyerwa	1	Ujenzi wa miundo mbinu ya shule	478,530,932
3	H/W Missenyi	1	Ujenzi wa madarasa na vyoo	46,600,000
4	H/W Buhigwe	10	Ujenzi wa madarasa,nyumba na vyoo	549,000,000
5	H/W Kasulu	1	Ujenzi wa mabwenu kwa wenye mahitaji maalum	160,000,000
6	H/M Kasulu	3	Ujenzi wa maabara na vyoo	143,200,000
7	H/W Uvinza	3	Ujenzi wa nyumba na mabweni ya wavulana na wasichana	210,000,000
8	H/W Kyela	4	Ujenzi wa madarasa na vyoo	186,400,000
9	H/W Mbeya	2	Ujenzi wa madarasa na vyoo	93,200,000
10	H/W Rungwe	2	Ujenzi wa madarasa,jingo la utawala na vyoo	136,600,000
11	H/W Nkasi	1	Ujenzi wa madarasa	39,225,390
12	H/W Korogwe	1	Ujenzi wa bweni	100,000,000
13	H/M Korogwe	1	Ukarabati wa mabweni	40,000,000
14	H/W Muheza	1	Ujenzi wa bweni	80,000,000
15	H/W Pangani	1	Ujenzi wa miundombinu ya shule	1,000,000,000
16	H/J Tanga	4	Ujenzi wa madarasa ,nyumba na jengo la utawala	170,000,000
17	H/W Meru	1	Ujenzi wa maabara na nyumba	200,000,000
<b>Jumla</b>				<b>3,820,160,743</b>

**Chanzo:** Nyaraka za miradi

Hii ilitokana na uhusishwaji usioridhisha wa vitengo vya usimamizi wa manunuizi wa halmashauri husika katika utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa na inaweza ikapelekea upangaji wa rasilimali usiojitosheleza kwa miradi iliyotekelzwa.

**Ninapendekeza menejimenti za halmashauri husika kuhusisha ipasavyo vitengo vya manunuizi katika utekelezaji wa miradi. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kujumuisha manunuizi yote**



# SURA YA TANO



**USIMAMIZI WA MIKATABA NA HALI HALISI YA  
UTEKELEZAJI WA MIRADI**

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inaonesha matokeo yanayohusiana na utendaji wa miradi iliyobainishwa wakati wa kufanya kaguzi za fedha za miradi 300 zilizofanyika kwa wa fedha 2021/22 zaidi ya kaguzi za kiufundi na uhakiki wa taasisi katika kuzingatia matakwa ya sheria (Compliance Audit).

Yafuatayo ni matokeo muhimu katika uhakiki wangu wa hali halisi ya utendaji wa miradi.

### 5.1 Udhibiti wa mikataba

#### 5.1.1 Magari yaliyolipiwa lakini hayajapokelewa Sh. bilioni 26.28

Kanuni ya 130(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ilio rekebishwa na Kanuni ya 41 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2016 inataka Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali (GPSA) kununua magari ya umma kwa niaba ya Taasisi za Serikali. Serikali ya Tanzania na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Huduma za Miradi (UNOPS) ziliingia mikataba ya usambazaji wa magari katika utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN) unaotekelizwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Nilibaini kuwa, kati ya kipindi cha mwezi Agosti 2021 na Aprili 2022, watekelezaji wa miradi wanne walilipa kiasi cha Sh. Bilioni 26.28 kwa Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali (GPSA) na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Huduma za Miradi (UNOPS) ili kununua magari 204. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Novemba 2022 (wakati wa ukaguzi wetu), magari hayo hayakuwa yamepokelewa, kama ilivyobainishwa katika Jedwali Na. 24.

#### Jedwali Na. 24: Maelezo yanayoonesha magari yaliyolipiwa lakini hayajapokelewa

Sekta	Mradi	Jina la Mzabuni	Idadi ya magari	Kiasi (Sh.)
Elimu	Matokeo Makubwa Sasa katika Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (EPforR)	Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali (GPSA)	134	14,937,223,172

Sekta	Mradi	Jina la Mzabuni	Idadi ya magari	Kiasi (Sh.)
Afyा	Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiijini (SWRSSP)	Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali (GPSA)	6	505,555,500
Maji	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijiijini (Programu ya Matokeo makubwa)- RUWASA	Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali (GPSA)	24	3,784,009,050
Jamii	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(TASAF)	Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Huduma za Miradi (UNOPS)	40	7,057,498,415
Jumla			204	26,284,286,137

Chanzo: Faili za manunuzi za watekelezaji wa miradi

Mlipuko wa UVIKO 19 ulizua mtengenezaji kutengeneza magari kwa wakati. Hii inazuia utekelezaji wa mradi, hasa katika kuwezesha huduma za usafirishaji.

Ninapendekeza kwamba Menejimenti ya watekelezaji wa miradi husika kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali (GPSA) na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Huduma za Miradi (UNOPS) ili kuhakikisha magari yaliyolipiwa yanapokelewa na kukabidhiwa kwa walengwa waliokusudiwa.

### 5.1.2 Mikataba ilioisha muda bila kuhuisha Sh. milioni 421.75

Aya ya 9 ya Mwongozo wa kufanya kazi za ujenzi kwa kutumia njia ya “force account” uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) mwezi Mei 2020 inataka timu inayotekeliza mradi kuandaa kazi maalum na mikataba ya kazi kwa mafundi.

Katika mwezi Agosti 2022 nilibaini kuwa mikataba yenye thamani ya Sh. 361,100,000 kwa ajili ya shughuli za ujenzi kuitia mradi wa Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ya shule sita za sekondari katika halmashauri nne ilikuwa imeisha muda wake wakati mafundi wanaendelea kufanya kazi mbalimbali bila ya kuhuishwa. Jedwali Na. 25 hapa chini linaonesha maelezo zaidi.

#### Jedwali Na. 25: Mikataba ilioisha muda bila ya kuhuishwa

Halmashauri ya Wilaya	Jina la Shule ya Sekondari	Jumla ya Mkataba (Sh.)
Mpwapwa	Galigali	50,000,000
	Iwondo	61,000

Halmashauri ya Wilaya	Jina la Shule ya Sekondari	Jumla ya Mkataba (Sh.)
Ngorongoro	Ololosokwani	85,600,000
Uvinza	Mpeta	64,200,000
Kakonko	Gwanumpu	100,300,000
<b>Jumla</b>		<b>361,100,000</b>

**Chanzo:** Daftari la fedha na vocha za malipo

Pia nilibaini kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ilinunua dawa, vifaa vya uchunguzi, kemikali za maabara, vifaa vya matibabu na tiba vyenye thamani ya Sh.60, 651,599 kutoka kwa mshitiri (Prime Vendor) (M/s Planet Pharmaceutical Ltd) kuititia Mfuko wa Uchangiaji wa Afya (HBF) baada ya tarehe 15 Oktoba 2021 wakati mkataba kwa mzabuni huyu ulikuwa umeisha muda wake kwani mkataba ulimalizika tarehe 14 Oktoba 2021.

Hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na udhibiti ndani usioridhisha katika usimamizi wa mikataba. Bila kuwepo kwa mkataba halali, uwajibikaji na dhima ya kila upande haiwezi kuwepo.

**Napendekeza kuwa katika siku zijazo usimamizi wa miradi husika, watekelezaji wafuate taratibu za manunuvi na manunuvi yoyote yanayofanywa yanapaswa kuwa na mkataba halali.**

### 5.1.3 Kutowasilisha kwa michoro mara baada ya ujenzi kukamilika

Mapitio ya mkataba Na. AE/059/2018/2019/W/04 wenye thamani ya Sh.2,829,778,143.16 kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya Bodii ya Maji ya Bonde la Wami Ruvu. Mkandarasi aliwasilisha cheti cha kukamilika kwa kazi kuititia kwa mkandarasi mshauri tarehe 24 Februari 2022 bila kuwasilisha michoro mara baada ya ujenzi kukamilika. Hadi tarehe ya ukaguzi mwezi Agosti 2022, Bodii haikuweka akiba ya 0.5% (Sh. 14,148,890.72) ya bei ya mwisho ya mkataba.

Hii ni kinyume cha kipengele 28 cha masharti maalum ya mkataba na kipengele 61.1 cha masharti ya jumla ya mkataba ambacho kinataka mkandarasi kuwasilisha michoro ya ujenzi mara baada ya ujenzi kukamilika siku 14 kabla ya kuwasilisha cheti cha kukamilisha kazi. Ikiwa hawawezi kufanya hivyo, meneja wa mradi atazuia asilimia 0.5 ya bei ya mwisho ya mkataba.

Hii ilisababishwa na jitihada zisizoridhisha za mkandarasi mshauri na menejimenti ya Bonde, ambao zina wajibu kuhakikisha mkandarasi anatimiza wajibu wake wa kimkataba ambayo inaweza kupelekea ugumu katika matengenezo, kufanya mabadiliko, na hivyo kuongeza gharama.

**Napendekeza menejimenti ya Wizara ya Maji ihakikishe kuwa mkandarasi anawasilisha michoro mara baada ya ujenzi kukamilika bila kuchelewa zaidi au kuzuia 0.5% ya bei ya mwisho ya mkataba ambayo ni Sh.14,48,890.72.**

#### **5.1.4 Utekelezaji wa miradi ya nje ya gridi kabla ya kupata idhini inayotokana na taarifa ya kina ya mradi**

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 na Kifungu cha 81(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004, inaitaka taasisi nunuzi kufanya tathmini ya athari ya mazingira katika hatua ya upangaji kabla ya kuanza ketekeleza au kufadhili mradi.

Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) ilisaini mkataba Na. TZS-DAWASA-91652-CS-QCBS wenye thamani ya Dola za Kimarekani 134,950 na kampuni ya Royal Associate Consulting Engineering kwa ajili ya maandalizi ya Ripoti ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIA) na Mpango wa Hatua za Uhamishaji (RAP) kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya usafi nje ya gridi kuanzia tarehe 1 Juni 2020 hadi 30 Novemba 2020. Pia, ilisaini mkataba Na. TZS-DAWASA-91662-CS-QCBS wenye thamani ya Dola za Kimarekani 249,750 na mkandarasi mshauri (WAPCOS) kuanzia tarehe 1 Mei hadi 30 Oktoba 2020 kwa ajili ya utoaji wa huduma za ushauri kwa ajili ya kuiwezesha jamii, kuandaa muundo wa kina (detailed design), nyaraka za zabuni kwa miradi ya usambazaji wa maji nje ya gridi Dar es Salaam.

Ingawa upitiaji wa mafaili ya mradi nilibaini kuwa, taarifa mbili za kina za mradi kutoka kwa washauri ambao ni Royal Associates na WAPCOS hazikuwa zimeidhinishwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lakini utekelezaji wa miradi ulikuwa umeanza tangu mwaka 2021 na 2022 na wakandarasi wa kampuni za Cytun/Kascco JV na Advent Construction Limited na M/s Help Desk Engineering Limited mtawalia. Kushindwa kupata idhini muhimu kutoka NEMC kunaweza

kusababisha kutokufuata sheria na kanuni na hivyo kusababisha adhabu na matokeo mengine kwa wakala na wakandarasi wanaotekeleza mradi.

**Ninapendekeza menejimenti ya Wizara ya Maji na DAWASA ziwasiliane na NEMC ili kupata idhini ya nyuma ya taarifa kina ya mradi.**

## **5.2 Utendaji wa Miradi**

### **5.2.1 Ujenzi uliotelekezwa wa maghala 14 na miundombinu ya nje saidizi katika kijiji cha Endanoga Wilayani Babati**

Wizara ya Kilimo ilisaini mkataba Namba ME 012/2020-2021/TANIPAC/W/37-lot 5 tarehe 9 Julai 2021 na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa maghala 14 na miundombinu ya nje saidizi kwenye kijiji cha Endanoga katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati Mkoani Manyara kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Mpango wa Kuzuia Uchafuzi wa Aflatoxini Tanzania (TANIPAC) ukilenga kuboresha miundombinu, teknolojia na usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno. Thamani ya mkataba ilikuwa Sh. 1,071,799,250 na tarehe ya kukamilika ilirekeblishwa hadi 30 Agosti 2022.

Mapitio yangu ya nyaraka za mradi na kutembelea sehemu ya ujenzi wa mradi mnamo tarehe 31 Agosti 2022 yamebaini kwamba mkandarasi alilipwa kiasi cha Sh. 241,567,481.18 sawa na asilimia 22.5% ya thamani ya mkataba ambapo maendeleo ya hali ya ujenzi ilikua 48% ilhali mkandarasi hakuwepo kwenye eneo la ujenzi tangu alipoondoka mwezi Aprili 2022 pasipo kutoa taarifa kwa Wizara husika kinyume na kifungu 6.7.1 (a) (b) cha Masharti ya Jumla ya Mkataba ambacho kinamuhitaji mkandarasi kumuarifu mwajiri ikiwa ameshindwa kutimiza majukumu yake ya mkataba au kama anataka kusitisha mkataba.

Mapungufu haya yametokana na Menejimenti ya Wizara kushindwa kusimamia vipengele vya mkataba vinavyomtaka mkandarasi kuwepo eneo la ujenzi au kutoa taarifa ya kutokuwepo kwake na hatua zinazopaswa kuchukuliwa endapo hatakekeleza vipengele hivyo. Kitendo cha mkandarasi kutokuwepo eneo la ujenzi kunachelewesha kukamilika kwa ujenzi wa ghala hivyo kuzuia/kuchelewesha huduma

kwa jamii iliyolengwa, aidha kuna hatari ya kuongezeka kwa gharama za mradi kunakoweza kusababishwa na kupanda kwa bei za vifaa hapo mbeleni. Aidha, inaweza kusababisha migogoro ya kisheria kati ya mkandarasi na Wizara.

**Napendekeza Wizara ya Kilimo (a) ichukue hatua za kimkataba dhidi ya mkandarasi kwa kuvunja kifungu 6.7.1 (a) (b) cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (b) iwasiliane na mkandarasi ili arudi kuendelea na ujenzi bila ya kuchelewa zaidi kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maghala 14 na miundombinu ya nje saidizi.**

#### **5.2.2 Baraza la Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze bado halijakabidhi jengo la mradi, vifaa vyta teknolojia ya mawasiliano ya habari na samani kwa Kikundi cha Usimamizi wa Mazingira ya Fukwe za Bahari (BMU) cha Saadan**

Mradi wa Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Uvuvi katika eneo la Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia ulikamilisha ujenzi wa ofisi za Usimamizi wa Mazingira ya Fukwe za Bahari (BMU) katika Manispaa tano za majoribio; Ofisi ya BMU Zingibari katika Wilaya ya Mkinga na Ofisi ya BMU Kipumbwi katika Wilaya ya Pangani Mkoani Tanga; Ofisi ya BMU Saadani katika Wilaya ya Chalinze na Ofisi ya BMU Dunda katika Wilaya ya Bagamoyo Mkoani Pwani; na Ofisi ya BMU Sudi katika Wilaya ya Lindi Mkoani Lindi. Kulingana na makubaliano, baada ya mradi kukamilisha ujenzi wa ofisi hizo chini ya Halmashauri ya Wilaya husika, halmashauri hizo zilipaswa kukabidhi majengo hayo ya ofisi kwa kila BMU kuitia kikao cha Baraza la Halmashauri ya Wilaya husika.

Baada ya kukamilika kwa ujenzi wa ofisi hizo mnamo mwezi Juni 2022, Katibu Mkuu-Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) aliandika barua yenyewe kumbukumbu No. AB.289/401/01/7 ya tarehe 29 Juni 2022 kwenda kwa Mabaraza ya Halmashauri hizo tano akiagiza majengo, vifaa vyta teknolojia ya mawasiliano na habari na samani vikabidhiwe kwa BMU husika kati ya tarehe 5 hadi 8 Julai 2022. Mpaka wakati wa ukaguzi wangu mwezi Novemba 2022 Halmashauri zote tano zilikua zimekamilisha ujenzi wa ofisi za BMU, vifaa vyta teknolojia ya mawasiliano na habari na samani.

Kinyume na agizo la Katibu Mkuu, ukaguzi wangu ulibaini kwamba kati ya Mabaraza ya Halmashauri hizo tano za Wilaya, halmashauri nne zilifanikiwa kukabidhi majengo na vifaa kwa BMU husika isipokuwa Baraza la Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ambalo bado halijakabidhi BMU ya Saadan majengo ya ofisi yaliyokamilika, vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano na samani vyenye thamani Sh. 154,973,235, na Sh. 37,120,000 mtawalia kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. I.**

Nilibaini kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Chalinze alishindwa kusaini hati za kukabidhi jengo hilo na vifaa kwa BMU ya Saadan kutokana na kutopata idhini ya Baraza la Halmashauri ya Wilaya Chalinze ambalo lilikua na mvutano wa kimaamuzi kwamba wakabidhi mali hizo kwa BMU ya Saadan au ziwe chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya Chalinze.

Kuchelewa kukabidhi mali hizo kwa BMU ya Saadan kunanyima jamii husika fursa ya kunufaika na mradi kwa wakati au kutotimia kwa malengo ya mradi yaliyokusudiwa

Ninapendekeza Wizara ya *Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi)* kuhakikisha inawasiliana na Halmashauri ya Wilaya Chalinze ili kukabidhi jengo la ofisi, vifaa vya teknolojia ya mawasiliano na habari, na samani kwa BMU ya Saadan bila kuchelewa zaidi.

#### **5.2.3 Mzabuni kushindwa kuweka mfumo wa kudhibiti ufanyaji kazi wa garimoshi kwa zaidi ya miaka minne kwenye reli ya Dar es salaam - Isaka kwa mkataba wenyе thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2.04**

Shirika la Reli Tanzania (TRC) linatekeleza Mradi wa Maendeleo ya Reli ya Kimataifa Tanzania (TIRDP) kwa kujenga njia ya reli kati ya Dar es Salaam - Isaka yenyе urefu wa kilomita 970. Kupitia ufadhili wa TIRDP, TRC iliingia mkataba namba PA/003/TIRDP-WB/G/012 na CRSC International Co. Ltd mnamo tarehe 22 Juni 2018 wenyе thamani ya Dola za Kimarekani 2,035,232.76 kwa kipindi cha wiki 54 (miezi 13.5) kwa ajili ya kubuni, kuleta, kusakinisha, kufanya majaribio, na kuzindua mfumo wa kudhibiti ufanyaji kazi wa garimoshi.

Ukaguzi wangu umebaini kwamba mpaka mwezi Novemba 2022 mzabuni alishindwa kuleta, kusakinisha, kufanya majaribio, na kuzindua mfumo wa kudhibiti ufanyaji kazi wa garimoshi ikiwa ni zaidi ya miaka minne tangu kusainiwa kwa mkataba, nyongeza ya mabadiliko ya mkataba huu ilitamatika tarehe 14 Januari 2022. Aidha, ilifahamika kuwa kushindwa kwa mzabuni kuweka mfumo huo kulisababishwa na athari za mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 ulioathiri shughuli za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa kimataifa.

Ni maoni yangu kwamba kucheleta kwa mzabuni kufunga mfumo huo kunaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za mradi kutokana na mfumuko wa bei.

Ninapendekeza menejimenti ya TRC (a) imuelekeze mkandarasi kutekeleza matakwa ya mkataba kwa kuhakikisha anasimika mfumo huo wa garimoshi na unafanya kazi bila kucheleta zaidi (b) kufanya upembusi ili kuona kama mkandarasi anaweza kuendelea kutekeleza mkataba, vinginevyo iangaliwe namna ya kuvunja mkataba kwa kuzingatia faida na hasara ili atafutwe mkandarasi mwingine kwa njia ya ununuzi wa dharura ili kuepuka kucheleta zaidi.

#### **5.2.4 Kutokuanza kwa kazi za kuimarishe na kuongeza kina cha Gati Na. 8-11 katika Bandari ya Dar es salaam kwa zaidi ya miaka mitano**

Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam (DMGP) ni mradi wa miaka saba ulio chini ya Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (TPA) kuanzia tarehe 27 Aprili 2018 na unatarajiwu kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni 2024. Moja kati ya maeneo manne ya mradi inataka kuimarishe na kuongezwa kina cha Gati Na. 8-11 katika Bandari ya Dar es salaam. Aidha, kifungu Na. 37 cha Nyaraka ya Tathmini ya Mradi (PAD) kinalekeza kwamba mchakato wa ununuzi na utekelezaji wa kazi katika eneo hilo la mradi kuanza katika robo ya nne ya mwaka 2017 na kukamilika katika robo ya kwanza ya mwaka 2021.

Ukaguzi wangu umebaini kwamba mpaka kufikia mwezi Novemba 2022 mchakato wa ununuzi kwa ajili ya kuimarishe na kuongeza kina cha Gati Na. 8-11 katika Bandari ya Dar es salaam ulikuwa bado haujaanza kutokana na kucheleta kukamilika kwa usanifu wa mradi,

hii ni kinyume na Kifungu Na. 37 cha PAD kinachotaka kukamilika kwa mradi ifikapo mwezi Desemba 2021.

Nina maoni yangu kwamba kucheleva kuanza kwa ujenzi kunaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za mradi na riba katika mkopo kwa serikali.

**Ninapendekeza TPA ihakikishe (a) inaharakisha mchakato wa usanifu wa ujenzi na kuukamilisha pasipo kucheleva zaidi (b) inaananzisha mchakato wa ununuzi na kuanza kazi za kuimarisha na kuongeza kina cha Gati Na. 8-11 (c) inasimamia mradi kwa ukaribu ili kuepuka ucheleweshaji zaidi na kupunguza gharama za mradi.**

#### **5.2.5 Kutokuanza kwa ujenzi na ununuzi wa vifaa katika shule 35 za awali za mfano kutokana na kukosekana kwa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT)**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza mradi wa Kusaidia Elimu ya Alama za Kusoma na Kuandika (LANES) ukilenga kuboresha upatikanaji wa elimu bora kwenye shule za awali, shule za msingi na elimu isiyo rasmi kwa kuzingatia wanafunzi kutoka kundi la watu walio hatarini zaidi ambao wanahitaji fursa kubwa za elimu ya msingi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs). Mradi huu unatekelezwa chini ya Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), aidha Katibu Mkuu TAMISEMI kuititia barua yenye kumbukumbu namba DA.291/297/108C'20 ya tarehe 18 Januari 2022 aliziyagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kukamilisha ujenzi na kununua vifaa kwenye shule hizo ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea fedha kwa kutumia utaratibu wa muongozo wa “force account”.

Nilitembelea shule hizo mnamo mwezi Septemba 2022 na kubaini kwamba Halmashauri 35 zilipokea jumla ya Sh. 1,953,840,000 katika mwezi Juni 2022 kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa vifaa vyaa shule za awali za mfano 35 lakini mpaka wakati wa ukaguzi ujenzi na ununuzi wa vifaa haukuwa umefanyika kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. II**.

Ilibainika kwamba kukosekana kwa hati ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kumepelekea kutokuanza kwa ujenzi na ununuzi wa vifaa hivyo. Ninadhani kwamba kutokuanza kwa ujenzi na ununuzi wa

vifaa si tu kunazuia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutimiza malengo yaliyokusudiwa katika mradi lakini pia kupatikana kwa thamani ya mradi na ongezeko la gharama za mradi kutoptana na kupanda kwa bei za bidhaa.

Ninapendekeza menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa 35 kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufuatilia na kupata hati za Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ili kukamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa katika shule 35 za awali za mfano.

#### 5.2.6 Ujenzi wa shule za sekondari mpya 101 bila hatimiliki za ardhi

Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia inatekeleza Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ukilenga kuboresha ubora wa elimu ya sekondari kwa wasichana na wavulana kwa kujenga mazingira salama, yanayozingatia jinsia na rafiki kwa wanafunzi; kutoa fursa nzuri za elimu mbadala kwa wale walioacha shule za sekondari; kuboresha ujuzi wa walimu, vifaa vyta kufundishia na kupunguza idadi ya wanafunzi darasani; kutumia teknolojia ya kidigitali kuboresha ufundishaji wa hisabati na sayansi; na kuongeza fursa ya elimu ya sekondari kwa kutoa shule nyingi zaidi karibu na makazi ya watoto. Aidha, moja ya malengo ya mradi ni kujenga shule mpya za sekondari 142 katika mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2022.

Mapitio yangu ya nyaraka mbalimbali za ukaguzi yamebaini kuwa jumla ya shule za sekondari 101 zenye thamani ya Sh. 47,470,000,000 zilizojengwa na mradi sawa na 71% ya shule zote zilizojengwa hazikuwa na hatimiliki za ardhi ili kuthibitisha uhalali wa kisheria wa umiliki wa ardhi ambazo shule hizo zimejengwa, muhtasari wa shule hizo unaonyeshwa kwenye **Kiambatisho Na. 3**. Kukosekana kwa hati za umiliki wa ardhi kumesababishwa na ufuatiliaji hafifu wa Maafisa Masuuli wa Halmashauri husika. Endapo kasoro hii haitarekebishwa kwa wakati inaweza kusababisha migogoro ya kisheria kuhusu umiliki wa ardhi hapo baadaye.

Aidha, kasoro hii ni kinyume na maagizo yaliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Msajili wa Hazina kuititia barua zenye kumbukumbu Na.

CAB142/626/01/A/42 na CAN.32/572/01/96 za tarehe 26 Septemba 2014 ambazo ziliagiza Maafisa Masuuli kuhakikisha wanapata hati miliki za ardhi walizonazo.

**Ninapendekeza menejimenti za Halmashauri za Wilaya husika kuongeza juhudzi za kufuatilia hati miliki za ardhi ili kupunguza hatari ya migogoro ya umiliki wa ardhi inayoweza kutokea.**

**5.2.7 Uwezo mdogo wa kuzalisha mapato unahatarisha uendelevu wa shughuli za mradi baada ya ukomo wa ufadhili wa Taasisi ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA)**

Mwaka wa 2016, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela-Afrika (NM-AIST) ilipata mkopo wa IDA ili kufadhili vituo vya elimu ya juu vya ubora katika Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Fedha hizo zililenga kutatua upungufu wa rasilimali watu katika mafunzo ya shahada ya uzamili katika sayansi na teknolojia, pamoja na kuongeza uzalishaji na ukuaji wa uchumi katika Afrika Kusini mwa Sahara. Kama sehemu ya ufadhili huo, NM-AIST ilianzisha Kituo cha Umahiri katika Taaluma (ACE) chini ya mradi wa Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu kwa Matumizi ya Baadae (WISE-Futures). ACE inalenga kutoa elimu bora ya shahada ya uzamili na kujenga uwezo wa utafiti wa ushirikiano katika maeneo muhimu ya kikanda.

Nimefanya ukaguzi ili kupima uendelevu wa shughuli za mradi kwa kuzingatia uwezo wa kukusanya mapato wa ACE baada ya ukomo wa ufadhili wa IDA na kubaini kwamba ACE ina uwezo mdogo wa kuzalisha mapato yake yenye kwa ajili ya kuendesha shughuli za mradi pindi ufadhili utakapokoma. Uchambuzi wangu wa mwelekeo wa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ACE katika kipindi cha miaka mitano ya fedha iliyopita umebaini kwamba Kituo cha Umahiri katika Taaluma (ACE) ina uwezo mdogo wa kukusanya mapato ambapo katika kipindi chote cha miaka mitano imefanikiwa kukusanya mapato sawa na wastani wa 6% kwa mwaka kulinganisha na mapato yake kwa ujumla kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 26.**

## Jedwali Na. 26: Mwelekeo wa ukusanyaji mapato kutoka mwaka 2017/18-2021/22

Maelezo	Mwaka (kiasi kwa Dola za Kimarekani)				
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
<b>WISE-Futures</b>					
Mapato kutoka IDA	1,096,272.00	511,697.95	1,019,047.62	1,201,176.50	1,670,275.57
Mapato mengine	950.96	6,292.90	9,530.15	362,245.97	66,220.93
<b>Jumla ya mapato</b>	<b>1,097,222.96</b>	<b>517,990.85</b>	<b>1,028,577.77</b>	<b>1,563,422.47</b>	<b>1,736,496.50</b>
Asilimia ya mchango wa "mapato mengine" kwa "jumla ya mapato"	0.09%	1.21%	0.93%	23.17%	3.81%
<b>CRATES-FNS</b>					
Mapato kutoka IDA	1,096,278.00	665,187.00	813,651.68	912,443.79	1,093,679.00
Mapato mengine	8,036.90	60,669.92	303,042.46	120,719.00	237,972.00
<b>Jumla ya Mapato</b>	<b>1,104,314.90</b>	<b>725,856.92</b>	<b>1,116,694.14</b>	<b>1,033,162.79</b>	<b>1,331,651.00</b>
Asilimia ya mchango wa "mapato mengine" kwa "jumla ya mapato"	1%	8%	27%	12%	18%

**Chanzo:** Taarifa za fedha zilizokaguliwa miaka ya nyuma

Aidha, mradi wa Kituo cha Utafiti katika Maendeleo ya Kilimo, Ufundishaji Bora na Uendelevu - Usalama wa Chakula na Lishe (CRATES-FNS) uliotekeliezwa na NM-AIST unakabiliwa na changamoto inayofanana na ACE katika suala la uwezo mdogo wa kukusanya mapato yake yenye baada ya ukomo wa ufadhili wa IDA ambapo katika kipindi chote cha miaka mitano imefanikiwa kukusanya mapato sawa na wastani wa 13% kwa mwaka kulinganisha na mapato yake kwa ujumla kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 35** hapo juu.

Athari ya kukosekana uendelevu wa shughuli za mradi kunaweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya kuanzishwa kwa miradi ya WISE-Futures na CRATES-FNS.

NM-AIST inapaswa kuanzisha mpango mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa mapato yake kuhusiana na miradi ya WISE-Futures na CRATES-FNS kwa ajili ya muendelezo wa shughuli za miradi hiyo baada ya ukomo wa ufadhili wa IDA.

## 5.2.8 Kasi ndogo katika utekelezaji wa programu ya EASTRIP

Serikali ya Tanzania ilisaini mkataba wa ufadhili na Benki ya Dunia kwa ajili ya Mradi wa Ujuzi wa Afrika Mashariki kwenye Mageuzi na Ushirikiano wa Kikanda (EASTRIP) ili kuanzisha Vituo vya Juu vya Mafunzo ya Elimu ya Ufundu (TVETs). Mradi huu unatekelezwa katika Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) Kampasi ya Dar es salaam (DIT Dar es salaam) na Mwanza (DIT Mwanza), Taasisi ya Kitaifa ya Usafirishaji (NIT), na Chuo cha Ufundu Arusha (ATC) kwa kipindi cha miaka mitano. Shughuli za ujenzi zilipangwa kukamilika ndani ya miaka mitatu ya mradi, ambao ulianza 30 Oktoba 2018 na unatarajiwa kukamilika ifikapo 31 Desemba 2024.

Mwezi Oktoba 2020, mfadhili (IDA) alilipa kiasi cha Sh. 51,421,041,623.13 sawa na Dola za Kimarekani 22,447,472.28 ikiwa ni 30% ya ufadhili wote kama malipo ya awali kwa taasisi za TVETs zilizolengwa, ambapo zinatakiwa kutumia 80% ya fedha hizo kwenye shughuli za ujenzi.

Wakati wa ukaguzi wangu uliofanyika mwezi Oktoba 2022 nimebaini TVETs zimetumia kiasi kidogo cha fedha walizopokea kwa kiwango cha 46% ilhali shughuli za ujenzi zikiwa bado hazijaanza kufanyika ambapo shughuli hizo zinaghari mu 80% ya fedha zilizopokelewa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 27** na **28** hapo chini.

### **Jedwali Na. 27: Muhtasari wa fedha zilizopokelewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na TVETs**

Na.	Taasisi	Kiasi	
		Dola za Kimarekani	Sh.
1	Kitengo cha Uratibu Kitaifa katika Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	1,447,472.28	3,645,186,247.00
2	DIT (Kampasi Kuu Dar es salaam)	4,875,000.00	11,142,362,026.13
3	DIT (Kampasi ya Mwanza)	4,875,000.00	11,105,350,000.00
4	NIT	6,375,000.00	14,516,632,350.00
5	ATC	4,875,000	11,011,511,000.00
Jumla		22,447,472.28	51,421,041,623.13

Chanzo: *Taarifa za fedha za miaka 2021/22*

## Jedwali Na. 28: Utendaji wa kifedha wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na TVETs

Taasisi	Kiasi kilichotengwa (Dola za Kimarekani)	Kiasi kilicholipwa (Dola za Kimarekani)	Matumizi halisi (Dola za Kimarekani)	Salio (Dola za Kimarekani)	% ya matumizi kwa jumla kilicholipwa
Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	5,000,000	1,447,472	1,271,698.35	175,773.93	88
ATC	16,250,000	4,875,000	1,583,439.65	3,291,560.35	32
DIT (Kampasi Kuu Dar es salaam)	16,250,000	4,875,000	1,625,510.13	3,249,490.00	33
DIT (Kampasi ya Mwanza)	16,250,000	4,875,000	986,015.46	3,888,985	20
NIT	21,250,000	6,375,000	4,902,944	1,472,056	77
<b>Jumla</b>	<b>75,000,000</b>	<b>22,447,472</b>	<b>10,369,607</b>	<b>12,077,864</b>	<b>46</b>

Chanzo: Taarifa ya Maendeleo ya MoEST, 2021/22

Aidha, mapitio yangu zaidi juu ya maendeleo ya mradi kwa ujumla katika shughuli za ujenzi na ununuzi katika TVETs yamebaini kwamba; NIT haikuandikisha wanafunzi wa kikanda kinyume na lengo la PAD; NIT ilifanikiwa kufikia 87% ya lengo la kukusanya mapato kiasi cha Dola za Kimarekani 5,170,000 ifikapo mwaka 2024; Ujenzi katika Kampasi ya DIT Mwanza ulikuwa katika hatua ya kuhama; Ununuzi wa miundombinu muhimu katika Kampasi ya DIT Dar es Salaam upo katika hatua za awali; na Shughuli za ujenzi katika ATC hazijaanza licha ya kipindi cha utekelezaji wa mradi kuwa kinamalizika mwezi Desemba 2024. Undani zaidi kuhusu bajeti ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 29**.

## Jedwali Na. 29: Utekelezaji wa bajeti kwenye TVETs

Taasisi	Budget iliyoidhinishwa	Bajeti iliyotekelizwa kwa sehemu	Bajeti iliyotekelizwa kikamilifu	Bajeti ambayo haijatekelez wa
Kitengo cha Uratibu Kitifa katika Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	Sh. 3,465,000,000	Sh. 966,702,890 (82%)	Sh. 305,819,970 (18%)	-
NACTVET	Sh. 2,647,912,500	Sh. 1,067,300,000 (40%)	Sh. 181,100,000 (7%)	Sh. 1,399,512,500 (53%)

Taasisi	Budget iliyoidhinishwa	Bajeti iliyotekelawa kwa sehemu	Bajeti iliyotekelawa kikamilifu	Bajeti ambayo haijatekelez wa
DIT (Kampasi Mwanza)	Dola za Kimarekani 16,250,000	Dola za Kimarekani 13,011,740 (80%)	-	-
DIT (Kampasi Kuu Dar es salaam)	Sh. 29,003,249,218	-	-	-
NIT	-	-	-	-

**Chanzo:** Taarifa ya maendeleo ya mradi ya Juni 2022 na bajeti ya mradi

Kushindwa kufikia baadhi ya Viashiria vya Ugawaji wa Fedha (DLIs) na michakato ununuzi inayochukua muda mrefu ikihusisha kupata kibali cha mfadhili kumepelekea kuchelewa kwa ujenzi na baadhi ya ununuzi kwenye mradi. Kifungu 2.03 cha mkataba wa ufadhili kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia kinaelezea kiwango cha juu cha adhabu cha riba ya nusu ya asilimia moja kwa mwaka kwa kiasi cha fedha ambacho Serikali ya Tanzania itakatwa kwenye kiasi ambacho imeshindwa kukitoa kutoka Benki ya Dunia (unwithdrawn amount) kutokana na kiasi cha mkopo kilichoidhinishwa ambacho ni Sh. 75,000,000 ambapo itapelekea kupunguza kiasi cha mkopo huo, aidha ni gharama isiyo ya lazima kwa serikali.

**Ninapendekeza Menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na TVETs husika waongeze kasi ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya EASTRIP.**

#### 5.2.9 TASAF haikupeleka kiasi cha Sh. milioni 651.85 zilizoidhinishwa kwenda kwenye miradi tisa katika Wilaya za Ludewa na Makete

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) unatekeleza mradi wa TASAF wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN) kwa jumla ya wanufaika 186 wanaoishi kwenye kaya hatarishi. Kitengo cha Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TMU) kinawajibika kuhakikisha kuwa shughuli za mradi zinapata kibali na fedha zinatolewa kwa wakati. Hii imeelezwa katika kipengele 2.5.3 (iii) na (iv) cha Kitabu cha Miundombinu ya TASAF.

Ukaguzi wangu umebaini kuwa TMU haikutoa kiasi cha Sh. 273,751,233 kwenda kwenye miradi mitano ya Wilaya ya Ludewa na Sh. 378,097,010 kwa miradi minne iliyoidhinishwa kwenye Wilaya ya

Makete licha ya miradi hiyo kuidhinishwa na Kamati ya Kitaifa ya TASAF.

Nina wasiwasi kwamba TMU inaweza kutumia fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya Wilaya za Ludewa na Makete kwenda kutekelezea shughuli zingine za TASAF kinyume na matakwa ya mradi. Aidha, kunazuia kufikia malengo ya mradi na manufaa ambayo jamii husika ingepata kutohana na mradi.

**Napendekeza kwamba TMU ipeleke kiasi cha Sh. 651,848,243 kilichoidhinishwa na Kamati ya Kitaifa ya TASAF kwenda Wilaya za Ludewa na Makete ili zitumike kutekeleza miradi hiyo tisa ya kijamii kama iliyoidhinishwa na Kamati ya Kitaifa ya TASAF.**

#### **5.2.10 Mapungufu kwenye udhibiti wa idhini ya kuhuisha Nambari ya Taifa ya Utambuzi (NIN) kwa wafaidika wa OTC kwenye kiwango cha PAA**

TASAF hutumia njia ya malipo ya kielektroniki inayoitwa “Over the Counter (OTC)” kwa ajili ya kuwalipa wanufaika wa mradi, ambapo huthibitishwa kwa kutumia Nambari zao za Utambuzi wa Kitaifa na alama za vidole kwa kutumia Programu ya Malipo ya TASAF. Kifungu cha 5.1.3 cha Mchakato wa Biashara wa Malipo Ya Kielektroniki kinahitaji kudhibiti na kuthibitisha Nambari za Utambuzi wa Kitaifa katika kiwango cha Mamlaka ya Eneo la Mradi (PAA) kwa malipo ya OTC. Programu ya malipo ya simu ya TASAF huthibitisha wafaidika kwa kulinganisha Nambari za Utambuzi wa Kitaifa zilizochukuliwa kwa mtindo wa alama za vidole na kuhifadhi katika kumbukumbu za Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa (NIDA), na ikiwa kuna utofauti, malipo ya OTC huwa hayafanyiki.

Wakati wa ukaguzi wa mchakato wa malipo ya OTC, ilibainika kwamba baadhi ya Nambari za Utambuzi wa Kitaifa zilichukuliwa kimakosa, hali iliyosababisha kushindwa kuthibitika baadhi ya wanufaika wa TASAF wakati wa malipo ya OTC.

Aidha, nilibaini kwamba maafisa ufuutiliaji wa TASAF (TMOs) wanaweza kuhuisha Nambari za Utambuzi wa Kitaifa za wanufaika kuititia Mfumo wa Malipo wa Kielektroniki Serikalini (GePG) pasipo idhini au udhibiti wa ukaguzi, pia, hapakuwa na udhibiti mahususi kwenye uhakiki. Mapungufu haya ya udhibiti wa uthibitisho wakati

MSCL haikutoa data za kuaminika au kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuwasilisha vipimo vya meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600, tani 400 za mizigo na magari 20-30. Baadaye Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliomba mabadiliko ya kuongeza uwezo wa kubeba abiria 1200 na tani 400 za mizigo, lakini hakukuwa na ushahidi wowote unaoonyesha kuwa mabadiliko hayo yalitokana na takwimu za uhakika. Ukosefu huu wa uwazi unaweza kusababisha ujenzi wa meli kubwa kuliko inavyohitajika, na kusababisha gharama kubwa za mtaji na uwezekano wa meli isiyo na faida, kinyume na

Kifungu cha 39 (c) na Kifungu cha 3 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011.

### **8.2.2 Kuchelewa kumshirikisha mshauri mwelekezi kwa siku 638**

Mwongozo wa 7.8.1 wa Mwongozo wa Uendeshaji wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma na Kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 vinahitaji mamlaka ya mkataba kumshirikisha mshauri au mtaalam kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mradi. Walakini, MSCL ilikawia kumshirikisha mshauri kwa siku 638 tangu kuanza kwa ujenzi wa meli mpya tarehe 17 Januari 2019, na iliwatambulisha M/S OSK-SHIPTECH A / S kutoka Denmark kwa mkandarasi tu tarehe 16 Oktoba 2020. Kuchelewesha huku kulitokana na kutegemea sana timu ya ukagazi wa kiufundi iliyopo na meneja wa mradi. Kuchelewesha huku kulinjeza hatari ya kutoweza kufuata viwango na maelezo ya kiufundi wakati wa ujenzi wa meli mpya.

Napendekeza menejimenti ya MSCL kufanya upembuzi yakinifu wa kutosha kwa miradi mpya ya ujenzi na ukarabati wa meli na kuhakikisha kuwa timu ya wahandisi wenye ujuzi na uzoefu inakagua na kuchunguza meli zitakazofanyiwa ukarabati ili kutoa makadirio sahihi ya gharama ya kina kabla ya zabuni kuitishwa zabuni. Hii itasaidia kutathmini uwezekano wa mradi na kuzuia kuongezeka kwa gharama na ucheleweshaji.

### **8.3 Usimamizi wa mikataba**

#### **8.3.1 Mabadiliko ya muundo wa mradi bila idhini ya msimamizi wa mradi**

Ukagazi ulibaini kuwa msimamizi wa mradi hakuidhinisha mabadiliko ya muundo kama inavyotakiwa na Kifungu cha 5.2 (d) cha mashariti ya jumla ya mkataba .Kumefanyika marekebisho kadhaa ya muundo kwa MV Mwanza bila kumbukumbu sahihi au ukagazi upya na idhini ya mamlaka husika.

Hii ilisababishwa na udhaifu katika usimamizi wa mkataba, ambao ulisababisha kuharibika kwa muundo wa meli na hatari ya kutoweza kutumika kwa usalama kwenye maji. MSCL inashauriwa iboresha

usimamizi wa mkataba na kuhakikisha kumbukumbu sahihi na ukaguzi wa marekebisho ya muundo katika miradi ya baadaye.

### **8.3.2 Maelezo ya injini zilizowekwa yanatofautiana na mahitaji ya mwajiri**

Wakati wa mazungumzo ya ununuzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria, MSCL na mkandarasi walikubaliana kuhusu vipimo vya injini, ikiwa ni pamoja na nguvu ya 2,720kW na injini mbili za MAN-B&W Diesel Alpha inline zenyenye miiko minne yenye mitungi minane.

Hata hivyo, wakati wa kutembelea mradi, iligundulika kuwa injini zilizowekwa zilikuwa na uwezo wa 2380 kW na mitungi saba tu. Nilibaini kuwa injini na sanduku la gia zilitakiwa kujengwa na M/S Man Diesel na M/S Turbo South Korea Limited lakini badala yake zilitengenezwa na Kampuni ya M/S STX MAN Engine kutoka Korea Kusini. Hakuna sababu na ufanuzi uliotolewa kwa mabadiliko hayo, na haijulikani kama bodi ya zabuni iliidhinisha. Tofauti hizi zinatia shaka iwapo injini zinaweza kufanya kazi kwa kiwango kinachohitajika.

### **8.3.3 Upangaji usiofaa wa tangi la maji kwenye injini kuu**

Wakati wa ziara ya eneo la mradi, ilibainika kuwa tangi kuu la maji ya kupozea injini kubwa lilikuwa na kasoro kwenye upande ambao mabomba yanaungana na mfumo wa injini kuu. Chanzo cha kasoro hiyo ilikuwa ni kiungio kilichovuta upande wa tangi na kuharibu. Tangi hilo liko juu ya sehemu ya meli inayozua maji kuingia kutokana na ubovu huo matumizi ya kawaida yanaweza kusababisha kubadilika kwa umbo la bakuli la meli, ambayo inaweza kusababisha kuvuja na kupunguza kiwango cha maji ya kupoeza injini, ambayo inaweza kuathiri utendakazi wa jumla wa injini.

### **8.3.4 Uwekaji usiofaa wa milango kwenye sehemu ya kupaki gari kwenye meli**

Milango miwili kutoka kwenye chumba cha usukani hadi kwenye sitaha ya gari ilipatikana kuwa imewekwa vibaya wakati wa ukaguzi wa njia tofauti za kutorokea, sehemu za kuuzia na kuingia kwenye

meli mpya. Huu ni ukiukaji wa utaratibu wa kawaida wa utengenezaji wa mali.

#### Kielelezo Na. 3: Ugawaji usiofaa wa milango kwenye staha ya gari



Milango imewekwa vibaya kwenye sitaha ya Gari (Picha ilipigwa na wakaguzi tarehe 21 Oktoba 2022)

Wakati wa ukaguzi, iligundua kuwa milango inayoelekea kwenye injini na vyumba vya gia za usukani ilikuwa na ufikiaji wa sehemu ya kupaki gari ambayo inaweza kuruhusu abiria kufikia maeneo yaliyozuiliwa. Hii ilitokana na hitilafu za muundo. maafisa wa MSCL wamefunga milango na kusakinisha mfumo wa kengele, uamuzi huu unaweza kuwa hautoshi kuhakikisha usalama kwani kengele inaweza kushindwa.

#### 8.3.5 Kuchelewa kuanza kazi kwa siku 167

Kifungu cha 8.1 cha Mashariti ya jumla ya mkataba kwa ajili ya ukarabati wa MV Umoja na MV Sangara kinahitaji mwajiri kupata dhamana ya usalama wa utendaji kutoka kwa mkandarasi. Hata hivyo, kulikuwa na kuchelewa katika kupata eneo la kazi na kuanza kazi kwa miradi yote miwili kutoka tarehe ya kusaini mkataba tarehe 15 Juni 2021 hadi 25 Novemba 2021 kwa MV Umoja na tarehe 26 Mei 2021 hadi 8 Novemba 2021 kwa MV Sangara, mtawalia, MV Umoja ikiwa imechelewa kwa siku 163 na MV Sangara kwa siku 167. Hii ilisababishwa na kucheleweshwa kwa uwasilishaji wa dhamana ya utendaji na mkandarasi, kutokana na mchakato wa kupata kuitia benki za ndani na uhakiki kuchukua muda mrefu ili kulingana na

Kifungu 4.2. Kuchelewa huku kuliathiri kuanza kazi kwa wakati uliokubaliwa.

### 8.3.6 Ukarabati usio sahihi wa sehemu zilizoharibika au zenye matundu chini ya meli

Wakati wa ziara ya kutembelea MV Umoja mwezi Oktoba 2022, iligunduliwa kupitia kipimo cha unene wa chuma ya meli kwa kutumia kipimo cha ultrasonic kuwa ulipungua kufikia upungufu unaoruhusiwa wa zaidi ya 25%.

Katika maeneo kadhaa, ambayo ilihitaji kubadilishwa kwa chuma za chini. Walakini, wakati wa kazi ya moto inayoendelea ya chuma za upande wa chini na sehemu ya chini ya chombo, ubora wa kazi haukuridhisha, kwani mkandarasi alikata eneo dogo tu na kuliweka chuma mpya kwenye upande wa nje wa chombo badala ya kuondoa chuma nzima iliyo na unene uliopungua au uharibifu kwenye fremu, kama inavyoonyeshwa kwenye **Kielelezo Na. 4** hapa chini

**Kielelezo Na. 4: Ukarabati usio sahihi wa sehemu zilizoharibika na zenye matundu**





Ukarabati usio sahihi wa sehemu zilizoharibika au zenyé matundu kwenye uso wa chini wa meli

Wakati wa ukaguzi uliofanywa mwezi Desemba 2022, iligundulika kuwa mkandarasi hakuwa amerekebisha bati zozote zilizosahauliwa kwenye MV Umoja, licha ya kupewa maagizo ya kufanya hivyo na Meneja wa Mradi. Hii ilisababishwa na usimamizi usiofaa wakati wa kazi ya urekebishi haji na timu ya kiufundi ya mradi. Kama matokeo, bati za zamani zilidhoofika kwenye fremu.

#### **8.3.7 Upimaji wa kukubalika kiwandani kwa injini kuu za MT Sangara haukufanyika katika kiwanda cha utengenezaji kama inavyohitajika**

Kifungu cha 30 cha SCC na Kifungu cha 14.4 cha mashariti ya jumla (GCC) kinataka MSCL kufanya ukaguzi na majaribio wakati wote wa ukarabati wa MT Sangara.

MSCL ilituma wahandisi kuhudhuria Majaribio ya Kukubalika Kiwandani (FAT) ya injini mpya, lakini injini hizo zilijaribiwa na kukaguliwa katika karakana ya MANTRAX jijini Dar es Salaam, Tanzania. Hii haikidhi matakwa ya makadirio ya gharama za ujenzi ambayo inaamuru kwamba injini mpya ifanyiwe Majaribio ya Kukubalika Kiwandani (FAT) na majaribio yafanyike katika kiwanda cha utengenezaji wa injini.

Mkandarasi alileta injini mbili za aina moja badala ya injini pacha za baharini kama inavyotakiwa na mwajiri, na MSCL ilipoomba majaribio ya kipimo cha uwezo, MANTRAC ilikataa. Hii inaweza

kusababisha utendakazi duni wa injini baada ya kufungwa na pia inakiuka matakwa ya mwajiri kulingana na mahitaji ya jumla ya sekta ya baharini, na kuibua wasiwasni kuhusu ahadi ya mkandarasi kwenye suala la ubora na usalama.

### **8.3.8 MSCL haikushiriki katika jaribio la kuhakiki uimara kiwandani kwa ajili ya meli ya MV Victoria**

Kifungu cha 23.1 na kifungu cha 23.2 cha Mashariti ya ujumla (GCC) kati ya MSCL na M/S KTMI Co. Ltd kwa ubia na kampuni ya Yuko's Enterprises E.A Ltd kwa ajili ya ukarabati wa MV Victoria inamtaka mkandarasi kufanya majaribio na ukaguzi wa bidhaa na vifaa katika eneo la utengenezaji na kumpatia mwajiri na meneja wa mradi haki ya kuhudhuria vipimo na ukaguzi huo.

MSCL ilishindwa kutuma wataalam kuhudhuria majaribio ya kuhakiki uimara kiwandani (FAT) ya mitambo ya baharini, hususan injini, katika M/S STX engine Co. Ltd ya Korea Kusini, ambayo inahitajika na GCC. Kutokana na hali hiyo, masuala kadhaa ya utendakazi duni wa injini hizo yaliripotiwa baada ya meli hiyo kufanya kazi kwa muda wa miezi mitatu. Iwapo MSCL wangehudhuria FAT, wangeweza kubaini masuala hayo mapema na kuchukua hatua ya kuyashughulikia kabla ya vifaa hivyo kufika Tanzania.

### **8.3.9 Gharama za ziada zilizotokana na kutoandaa kwa usahihi makisio ya gharama za ujenzi (BoQs) ya ukarabati wa meli ya MT Sangara**

Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ina jukumu la kufuatilia gharama na muda wa utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa Kanuni ya 114 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma.

Hata hivyo, udhibiti duni wa gharama ulibainika kutokana na utayarishaji duni wa makisio ya gharama za ujenzi (BoQs) na makadirio ya wahandisi. Wakati wa ukarabati wa meli, baadhi ya vitu kama vile uingizwaji wa reli za ulinzi na ukarabati wa sahani za chini ya meli havikujumuishwa katika mahitaji ya mwajiri na hivyo kusababisha amri ya mabadiliko ya kiasi cha ziada cha Sh. 591,118,400.

Meneja wa Mradi alipendekeza bei ya chini kulingana na upatikanaji wa soko la ndani, ambayo inaweza kupunguza gharama kwa Sh. 25,234,000. Zoezi la utaratibu wa mabadiliko lilikuwa bado kwenye mazungumzo wakati wa ukaguzi.

#### 8.3.10 Udhahifu wa boti za uwokoaji katika meli ya MV Victoria

MSCL ilifanikiwa kubadilisha vifaa vya zamani vya kupambana na moto na kuweka vya kisasa; kuongeza maboya mapya mawili ya kuokoa maisha yenye uwezo wa kubeba watu 25 kila moja na kuboresha mfumo wa umeme. Kulingana na kipengele (S) ya BoQ zilizokubaliwa kwa ukarabati wa MV Victoria.

Niligundua kwamba ubora wa vibao vilivyowekwa katika mashua za kuokoa maisha yaliyoinuliwa ilikuwa duni, na tayari vilikuwa vikioza baada ya mwaka mmoja tu. Vibao hivyo vilitengenezwa kwa mbao laini, na ilibainika kwamba vilikuwa vimeharibiwa kutokana na unyevu na jua kama inavyoonyeshwa kwenye **Kielelezo Na. 5** hapa chini.

##### Kielelezo Na. 5: Mbao za boti za uokoaji zilizoharibika



Ubao ulioharibika wa boti za uwokoaji za MV Victoria. Picha ilipigwa na mkaguzi tarehe 5 Novemba 2022 bandari ya kaskazini - Mwanza

Bodi ambazo hazina kiwango ziliwekwa kwa sababu ya kutokuwa sehemu ya mkataba. Hii ilipelekea MSCL kuingia gharama ya ziada.

### **8.3.11 Mkataba ulioteklezwa wakati tayari dhamana ikiwa imeisha muda wake MV Mwanza**

Kifungu cha 4.2 cha mashariti ya jumla (GCC) kinamtaka mkandarasi kuwasilisha dhamana ya utendakazi ndani ya siku 14 za kazi baada ya kukubalika na kuhakikisha uhalali wake hadi kukamilika kwa mradi.

Hata hivyo, dhamana ya utendakazi iliyotolewa na Standard Charter kwa niaba ya GAS Entec Co. Ltd kwa MSCL ya kiasi cha Dola za Kimarekani 3,900,000 iliisha tarehe 2 Septemba 2020, kabla ya kukamilika kwa mradi. Kwa hiyo mradi ulitekelezwa bila dhamana ya utendakazi kwa zaidi ya mwaka mmoja, na kuwaweka MSCL katika hatari ya kupoteza rasilimali ikiwa mkandarasi atashindwa kutekeleza kazi zilizowekwa kandarasi.

### **8.3.12 Uwezekano wa kucheleweshwa kwa ukarabati wa MV Umoja na MT Sangara**

Muda uliokubaliwa wa kukamilika kwa mradi wa ukarabati wa MV Umoja ulikuwa miezi 12 kuanzia 25 Septemba 2021. Ucheleweshaji unaowezekana uligunduliwa kutokana na ucheleweshaji usiotarajiwa, kama inavyothibitishwa na barua ya Oktoba 12, 2022, iliyoomba kuongezwa kwa muda hadi 24 Aprili 2023. Kuchelewa kwa uzalishaji na utoaji wa injini za MV Umoja ni sababu iliyochangia kuchelewa kukamilika kwa mradi kama ulivyopangwa.

MSCL haikukubali kuongezwa kwa muda, licha ya kuchelewa kwa injini, kutokana na kushindwa kukusanya vifaa eneo la mradi, na kusababisha kazi kusimama. Kulikuwa na ucheleweshaji unaowezekana katika kukamilisha ukarabati wa MT Sangara kwani muda wa mkataba uliokubaliwa ulikuwa miezi 12 tangu tarehe ya kuanza.

Mkandarasi aliagizwa kuondoa na kubadilisha vitu viliviyokataliwa, ikiwa ni pamoja na Windlass, Jenereta ya Dharura, chujio na gia ya usukani na kitengo cha mfumo, lakini hadi tarehe 1 Novemba 2022, bidhaa hizo zilikuwa bado hazijabadilishwa, na hivyo kusababisha

kuchelewa zaidi. Hali ya jumla ya utekelezaji wa mradi wa MT Sangara ilikuwa 72.67%, nyuma kwa 19.37% kutoka kwa mpango halisi badala ya kuwa 92%.

#### **8.3.13 Utekelezaji wa mradi bila uteuzi wa meneja wa mradi**

Kifungu cha 3.1 cha Masharti ya Kitaalam ya Mkataba kinataka mwajiri amteue Meneja wa Mradi, ambaye ni kampuni huru au taasisi iliyosajiliwa na vyombo husika vya kitaalamu nchini Tanzania na imesaini mkataba na mwajiri. Majukumu ya Meneja wa Mradi ni pamoja na kupanga kwa usahihi, kusimamia hatari, na kudhibiti ubora wa mradi.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa mradi ulitekelezwa bila Meneja wa Mradi, na badala yake afisa wa ngazi ya juu kutoka JWTZ alisimamia mradi huo. Kutokuwepo kwa uteuzi wa Meneja wa Mradi mwenye sifa husababisha hatari ya kushindwa kwa mradi na upotevu wa muda, fedha, na rasilimali.

**MSCL inapendekezwa kumteua Meneja wa Mradi mwenye sifa kwa ajili ya usimamizi wa mkataba, kuweka mikakati ya kuwawezesha wataalamu wa kiufundi katika ujenzi na ukarabati wa meli, kuhakikisha uwepo wa wahandisi wa bahari wenye ujuzi wakati wa Testi ya Kukubalika Kiwandani (FAT) katika kampuni ya utengenezaji, kufanya vipimo wakati wa ujenzi na ukarabati wa meli, kuhakiki ipasavyo vitu vipyta vilivytangazwa na vipuri kabla ya matumizi, na kudhibiti wafanyakazi wa mkandarasi na washauri katika eneo la kazi.**

#### **8.3.14 Utupaji wa taka usiofaa ndani ya eneo la mradi**

Wakati wa ziara , ilibainika kuwepo na taka nyingi hatari za chuma, kama vile mabaki ya waya, vumbi, taka za chuma za kuchomelea, na uchafu mwingine, ambao ungeweza kuchangia uchafuzi wa mazingira na kutishia usalama wa watu. Mchakato wa kupaka kuta za meli pia unaweza kusababisha uchafuzi wa mazingira kupitia rangi iliyobaki, mivuke ya kutengenezea, na vifungashio.

Hata hivyo, hakukuwa na hatua za kutosha za kukabiliana na mazingira ili kuzuia uchafuzi wa mazingira, na taka zote za chuma kutoka kwa ukarabati wa MV Umoja zilikusanywa kwenye eneo la kazi, ambayo ililetatatu hatari mbaya ya mazingira. Hii inakiuka Kifungu cha 115(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 na Kifungu cha 4.18 cha GCC, ambacho kinahitaji uhifadhi na utupaji sahihi wa taka ngumu na ulinzi wa mazingira wakati wa mchakato wa ukarabati.

**Kielelezo Na. 6: Utupaji wa taka usiofaa kwenye eneo la mradi**



Mlundikano wa Taka zilizotokana na ukarabati wa MV Umoja

Napendekeza Kampuni ya Huduma za Meli kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari kuweka mikakati ya ujenzi wa mitambo ya kupokelea taka katika eneo la bandari ili kuhakikisha taka zinazotoka kwenye meli haziendi kwenye ziwa.



**SURA YA TISA**



**UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA KUBORESHA  
UBORA WA ELIMU YA SEKONDARI**

## **9.0 Utangulizi**

Mwaka 2016 Serikali ya Tanzania ilianzisha sera ya Elimu ya Msingi Bure ili kutoa elimu ya msingi na sekondari kwa wote. Mwaka 2018, takribani wasichana 1,025,629 na wavulana 965,242 walihudhuria shule za sekondari za chini. Ingawa, takribani wanafunzi 134,000 nusu yao wakiwa wasichana hawakuweza kuendelea na masomo kutokana na ukosefu wa nafasi katika shule za sekondari za Serikali. Katika kukabiliana na suala hili, Serikali inatekeleza Programu ya Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), mradi huu una thamani ya Dola za Kimarekani milioni 500 sawa na Sh. trilioni 1.15 unaofadhiliwa na Benki ya Dunia katika Halmashauri 184.

Lengo la ukaguzi ni kutathmini usimamizi wa ujenzi wa shule za sekondari chini ya Programu ya Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) inayosimamiwa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.Ukaguzi ulijumuisha miaka ya fedha kuanzia 2019/20 hadi 2021/22. Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kuhakikisha thamani ya pesa inapatikana. Zifuatazo ni hoja muhimu za ukaguzi na mapendekezo.

### **9.1 Mpango na usanifu wa mradi**

#### **9.1.1 Uandaaji usiojitosheleza wa usanifu wa michoro na kukosekana kwa michoro**

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa timu ya usanifu haikufuata kanuni 63(1) na (4) ya kanuni za Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) za mwaka 2010 ambazo zinataka michoro yote ya usanifu ya uhandisi iwe na kitalu cha kawaida kinachoonesha watu waliosanifu, kuhakiki na kuidhinisha michoro hiyo kwa kusaini na kupiga muhuri. Aidha, ilibainika kuwa kuna michoro mingine iliyokosekana ikiwa ni pamoja na michoro ya kina na vipimo kwa ajili ya njia za kutembelea na kuweka sakafu ya matofali madogo, mitaro ya maji ya mvua, wigo wa waya, kibanda cha mlinzi, kibanda kwa ajili ya nishati ya umeme na nyumba ya wafanyakazi (nyumba mbili kwa moja).

Nilibaini kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Chemchem katika halmashauri ya wilaya ya Rufiji ilikuwa haijaanza ujenzi wa nyumba mbili kwa moja ya watumishi sababu walikuwa bado wakingojea ufanuzi wa michoro iliyokosekana kutoka OR-TAMISEMI lakini mawasiliano yaliyofanyika kwenda OR-TAMISEMI yalikuwa hayajawekwa katika kumbukumbu. Katika shule nyingine mbili za sekondari za mkoa, nyumba za wafanyakazi zilikuwa zinaendelea kujengwa kwa kutumia michoro iliyotayarishwa na kuwekwa kwenye tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mnamo mwaka 2019 kama mwongozo wa ujenzi wa shule za sekondari. **Jedwali 32** linaonesha mapungufu katika michoro ya usanifu iliyofanyiwa mapitio kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari ngazi ya mkoa.

### **Jedwali Na. 32 Uwandaaji usiojitosheleza wa usanifu wa michoro na kukosekana kwa michoro**

Mchoro	Masuala yaliyobainika
Jengo la Utawala	Ukosefu wa maelezo yasiyotosha na vipimo namna litakavyoonekana, miinuko na sehemu za michoro.
	Ukosefu wa mipango ya vyumba vya majimaji, uwekaji wa maeneo kwa ajili ya kuweka vifaa vya usafi na vingine vinavyohusiana na usafi
	Ukosefu wa michoro na vigezo vinavyoelewaka kwa ajili ya milango migumu na madirisha ya chuma
	Ukosefu wa michoro maalum kwa ajili ujenzi wa shimo la kuhifadhi maji taka
	Ukosefu wa usanifu wa sakafu, nguzo na nguzo mlalo
	Ukosefu wa mpangilio wa samani kwa ajili ya usanifu wa michoro ya umeme.
	Ukosefu wa mpango wa umaliziaji wa jengo
Bwalo la chakula / Ukumbi matumizi mbalimbali (Titanic)	Ukosefu wa maelezo yasiyotosha na vipimo namna litakavyoonekana, miinuko na sehemu za michoro.
	Kutokuwepo kwa mpangilio wa michoro ya samani
	Ukosefu wa chumba, vifaa vya sehemu za maji maji, vyumba vya kuhifadhi, eneo la kusafishia na maeneo ya "server".
	Ukosefu wa mpango kumaliza na vigezo vya vifaa
	Ukosefu wa michoro ya kuzima moto.
	Miundo isiyojitosheleza, ukosefu wa mahesabu ya muundo wa jengo "structural calculations" na mpango wa ukunjaji nondo "bar bending schedule"
	Ukosefu wa mpango ya michoro ya ujenzi wa shimo la maji taka
Mabweni	Ukosefu wa maelezo yasiyotosha na vipimo namna litakavyoonekana, miinuko na sehemu za michoro.
	Kutokuwepo kwa vyumba, sehemu za kuwekea vifaa vyooni, mabweni, sehemu ya kufulia and chumba cha kupigia pasi
	Ukosefu wa michoro ya kina na vigezo kwa ajili ya madirisha, milango ya mbaao ngumu na madirisha ya chuma
	Ukosefu wa mpango wa kumaliza na vigezo vya vifaa
	Ukosefu wa michoro ya kuzima moto.
	Ukosefu wa michoro ya muundo
	Ukosefu wa mpango ya michoro ya ujenzi wa shimo la maji taka

Mchoro	Masuala yaliyobainika
Maabara za Kemia na Bailojia	Kutokuwepo kwa michoro na vigezo kwa ajili ya kazi za kutengeneza mabenchi ya maabara, kabati za kuhifadzia na chumba cha maandalizi. Ukosefu wa michoro ya kuzima moto.
	Kutokuwepo kwa maelezo na vigezo kwa ajili ya ufungaji wa "Fume hood" na vyombo nya kuoshea macho

**Chanzo:** Uchambuzi wa data baada ya kutembelea na kuona maeneo ya shule yaliyotembelewa, 2023

Uchambuzi zaidi ulibaini mapungufu katika michoro iliyotumiwa katika ujenzi wa shule za sekondari ngazi za kata. **Jedwali Na. 33** linaonesha majengo manne ambayo ni maabara, vyooo, chumba cha kompyuta, na nyumba ya vyuma vitatu pamoja na mapungufu yaliyobainika katika usanifu.

### **Jedwali Na. 33: Mapungufu yaliyobainika katika usanifu wa miundombinu ya shule ngazi ya kata**

Michoro	Masuala Yaliyobainika
Jengo la Utawala	Ukosefu wa michoro ya usambazaji maji kwenye vyoo nya watumishi na ukosefu wa vituo nya kupatia huduma kwa wafanyakazi wenye ulemavu.
Maabara	Hakuna ufanuzi na vipimo kwa ufungaji wa kabati za kuitishia hewa chafu na vyombo nya kufua macho. Hakuna ufanuzi wa vipimo na michoro ya meza za maabara, kabati za uhifadhi na vyumba nya maandalizi. Ukosefu wa michoro za kupambana na moto.
Choo cha Maji Kinachotirishwa kwa ajili ya watumishi 16	Tofauti zilizobainika kati ya michoro na orodha ya vifaa ambapo Orodha inatao Matofali ya sakafu ya porcelain ya saizi 500 x 500 x mm8 wakati Michoro inasema sakafu ya chini ngumu ya saruji na orodha ya vifaa. Hakuna ufanuzi wa wazi wa vipimo nya vifaa nya usafi. Hakuna michoro ya kina kwa ajili ya milango ya mbaao. Hata hivyo, kwa ajili ya fremu za milango ya choo na shutters, Ilishauriwa kutumia PVC au vifaa vingine ambavyo havitaathiriwa na maji.
Chumba cha Kompyuta	Ukosefu wa sehemu ya kuhifadzia vitu kama vite vitabu na vifaa vingine na chumba cha "server" Vigezo nya vifaa kwa ajili ya madirisha ya chuma yalikuwa hayajatolewa
Nyumba ya vyumba vitatu nya Kulala Tatu (aina ya mjini)	Ukosefu wa michoro na vipimo kwa ajili ya vyumba nya choo, chumba cha kuhifadzia, makabati ya chumba cha kulala, sehemu za juu za jikoni na makabati ya ukutani. Ukosefu wa michoro na vipimo nya milango, dirisha na vifaa kwa ajili ya grill za chuma

**Chanzo:** Uchambuzi wa data zilizotokana na kutembelea maeneo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa mwaka 2023

Uwepo wa usanifu usiojitosheleza kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari ilipelekeea kutofautiana kwa usanifu wa jumla wa kazi iliyofanyika na ubora, ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa usawa katika milango na madirisha, grills za metali, rangi za kupaka, vifaa vya sakafu na vifaa vya usafi. Pia ilipelekeea kutofautiana kwa udanifu uliyokusudiwa, kama vile kutokuwepo kwa eneo la ufungaji wa gesi na kabati za kutolea hewa (gas chambers) katika maabara zote zilizojengwa katika mashule.

**Ninapendekeza kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI kuanzisha mifumo ili kuhakikisha kuwa sanifu za mradi zinapitiwa na kuidhinishwa kabla ya kuanza kazi ya ujenzi, kuanzisha mfumo wa kubaini gharama halisi za ujenzi. Aidha, katika kuhakikisha kwamba mipango ya eneo la ujenzi inatayarishwa na kupitiwa na wataalamu waliodhinishwa na kuandaa seti ya taarifa za usanifu kwa mradi maalum ambazo zinaweza zikatolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kwa ajili ya usimamizi wa mradi.**

## **9.2 Usimamizi wa ununuzi**

### **9.2.1 Kuchelewa kufanya ununuzi wa mtathmini wa kujitegemea kwa zaidi ya miaka miwili**

Sehemu I.B.4 ya Jedwali la 2 ya makubaliano ya ufadhilli kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) yaliyosainiwa tarehe 21 Mei 2020, ilibainisha kuwa mtathmini huru alipaswa kuajiriwa ndani ya miezi mitatu baada ya kusaini makubaliano ya ufadhilli kwa Programu ya Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Katika kupitia zabuni Na. ME-023/WB-SEQUIP-P170480/235256/2021-22/HQ/C/12 nilibaini kuwa ununuzi wa mtathmini wa kujitegemea (independent verifier) ulichelewa kwa miezi 26 na haukuwa umeingizwa katika mpango wa manunuzi wa wizara wa mwaka 2020/21.

Hii ilitokana na kutokuwepo kwa mzabuni aliye na sifa, hivyo kupelekeea manunuzi hayo kuingizwa katika mpango wa manunuzi wa

mwaka 2022/23. Hii imepelekea mafanikio ya mradi kutolinganishwa vizuri na fedha zilizotolewa ambayo inaweza kusababisha kuchelewa kwa utoaji wa fedha kwa hatua za mradi zinazofuata.

#### **9.2.2 Mawanda ya kazi yaliyotolewa kwa mafundi “local fundis” ambayo hayajitosheleza wakati wa mchakato wa zabuni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Kanuni ya 182(b) na 184(c) za Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 zinataka taasisi nunuzi kuandaa tangazo la zabuni na kutolewa nyaraka za maombi ya zabuni zikiwa na maelezo ya kiufundi, mipango, michoro na usanifu kwa ajili ya kazi au huduma zinazonunuliwa.

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kwamba katika halmashauri ya wilaya ya Lindi, hakukuwa na nyaraka ambazo zilikuwa na orodha ya shughuli za kina zinazotakiwa kufanywa na watumishi kwa kila jengo wakati wa ununuzi wa mafundi. Katika mamlaka za serikali za mitaa nyingine, orodha ya shughuli kwa kila jengo ilionekana kuwa imeandaliwa na kutolewa kwa mafundi kwa ajili ya kujaza bei zao za kazi. Katika halmashauri ya wilaya ya Lindi, mafundi walitoa jumla ya pesa kwa kila ujenzi wa jengo bila kutoa orodha ya kina ya gharama kwa kila shughuli. Malipo kwa kazi yalifanyika sawa sawa katika hatua nne, bila kuzingatia uzito wa shughuli katika hatua hizo.

Migogoro ilijitokeza wakati wa utekelezaji kutokana na kutokuwepo kwa mawanda ya kazi na mafundi walikataa kutekeleza baadhi ya shughuli na kulalamika kwamba malipo yalikuwa hayaendani na kazi iliyo fanyika. Matokeo yake, hadi wakati wa ukaguzi ujenzi wa mitaro na mashimo ya majitaka kwa ajili ya vyoo na majengo ya utawala Kilangala katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi yalikuwa hayajakamilika.

#### **9.2.3 Uandaaji usiojitosheleza wa mikataba ya mafundi**

Aya ya 11.1 na 11.2 ya Mwongozo wa kutekeleza kazi kwa njia ya kutumia uwezo wa ndani katika utekelezaji wa miradi “Force Account” uliotolewa mwezi Mei 2020 kinahitaji kubainisha mawanda ya kazi kwa ajili ya utekelezaji. Vilevile, kipengele cha 52.1 cha

masharti ya jumla ya mikataba kwa huduma zisizo za ushauri iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma yenye kumbukumbu Na.PPRA/GCC/NC/02/2022 kinahitaji kufanya malipo kwa mafundi kwa mujibu wa taratibu wa malipo iliyowekwa katika masharti maalum ya mkataba.

Nimebaini kuwa mikataba ya kazi na mafundi katika miradi 8 kati 24 ya ujenzi wa shule za sekondari chini ya mpango wa SEQUIP katika mikoa minne ya Tanzania bara ilikosa ufanuzi wa mawanda ya kazi na taratibu za malipo. Maelezo zaidi yapo katika **Jedwali Na. 34**.

#### **Jedwali Na. 34: Mikataba iliyokosa ufanuzi wa mawanda ya kazi na utaratibu wa malipo**

Mkoa	Halmashauri	Shule
Songwe	Tunduma TC	Uwanjani
		Chiwezi/ Namole
Shinyanga	Shinyanga MC	Ikana
		Lubaga
Lindi	Lindi MC	Ndembezi
		Kilangala
Singida	Ikungi DC	Mingoyo
		Makilawa

*Chanzo: Uchambuzi wa nyaraka za mikataba kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari zinazotekelizwa na programu ya SEQUIP katika mikoa minne iliyotembelewa nchini, 2022*

Uzoefu mdogo katika maandalizi ya mikataba kwa kufanya manunuzi kwa njia ya kutumia uwezo wa ndani katika utekelezaji wa miradi “Force account” kumesababisha ukosefu wa mawanda ya kazi ya kina na utaratibu sahihi wa malipo kwa huduma zisizo za ushauri. Hii imesababisha baadhi ya shughuli za ujenzi kuachwa bila kufanyiwa kazi kutokana na masharti ya mkataba ambayo hayakueleweka vizuri.

Ninapendekeza kwa OR-TAMISEMI kutoa mafunzo kwa watumishi na kamati za utekelezaji wa miradi ili kuongeza uwezo wao wa kutekeleza majukumu yao. Aidha, utaratibu wa uandaaji wa mikataba unapaswa kuimarishwa kwa huduma zisizo za ushauri ili kuhakikisha kuwa watumishi waliohusika katika mamlaka za serikali za mitaa wana uwezo wa kutosha.

## 9.3 Usimamizi wa fedha

### 9.3.1 Bajeti isiyo halisi kwa ajili ya ujenzi wa shule katika ngazi ya kata

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI zilikuwa na jukumu la kuandaa michoro na bajeti husika za shule zilizojengwa chini ya Programu ya SEQUIP.

Mapitio ya makadirio ya gharama na ziara zilizofanywa kwenye shule 24 za sekondari zilizojengwa katika awamu ya kwanza ya Programu ya SEQUIP ilibainika kwamba bajeti iliyotengwa haikuwa ya kutosha kukamilisha ujenzi wa majengo ya shule. Kwa shule 20 katika ngazi ya kata zilizotembelewa, asilimia ya matumizi ya fedha zilizopokelewa ilikuwa juu kuliko asilimia ya ujenzi uliokamilika kwa shughuli za awamu ya kwanza kama ilivyoelezwa katika Jedwali Na. 35.

**Jedwali Na. 35: Salio la fedha dhidi ya ukamilishaji wa kazi hadi kufikia tarehe 25 Septemba 2022**

Halmashauri	Jina la shule	Fedha zilizotumika kati ya Sh. Milioni 470 zilizopokelewa (Sh. Milioni)	Asilimia ya fedha zilichotumika	Asilimia ya kazi zilizokamilika
H/W Lushoto	Mlalo	394.8	84	47
	Kwemashai	360	77	41
H/W Korogwe	Bagamoyo	426	91	61
	Mgwashi	26	6	4
H/W Lindi	Mingoyo	453	96	85
	Kilangala	468.7	100	86
H/W Kilwa	Ngome	464.3	99	73
	Somanga	462.3	99	78
H/W Rufiji	Ngarambe	458.5	98	78
H/W Kibaha	Kikongo	470	100	75
H/W Ikungi	Makilawa	470	100	85
	Ikungi	470	100	84
H/M Shinyanga	Lubaga	470	100	88
H/W Kishapu	Bupigi	470	100	95
H/W Muleba	Mafumbo	470	100	70
	Buligi	470	100	87
H/W Karagwe	Nyakakika	470	100	88
H/M Bukoba	Kashai	470	100	56
H/M Tunduma	Uwanjani	470	100	74
H/W Momba	Ikana	451	96	91

**Chanzo:** Data kutoka OR-TAMISEMI za mwaka 2023

Kati ya shule 20 zilizotembelewa, 11 zilitumia fedha zote zilizopokelewa, nane zilitumia fedha kwa kiwango kikubwa licha ya kutokamilisha kazi ya ujenzi hali ambayo imehatarisha ukamilishaji wa mradi na kuchelewa uandikishaji kwa kipindi cha miezi minne hadi saba.

### **9.3.2 Kuchelewa kuhamisha fedha kwa ajili ya shughuli za usimamizi**

Mikoa na mamlaka za serikali za mitaa husika imepewa jukumu la usimamizi ambapo hutumia wahandisi na wasanifu wa majengo kuongoza shughuli za ujenzi.

Fedha kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi wa EQUIP katika ngazi za mkoa na halmashauri zilipelekwa kwa kuchelewa iliyoambatana na barua iliyotumwa tarehe 17 Juni 2022 mara baada ya ujenzi kuanza. Fedha zilizotumwa zilikuwa ni kwa ajili ya shule za kata 232 na usimamizi kwa ngazi nne, ambapo mikoa ilipokea Sh. milioni 10, ofisi za kikanda zilipokea Sh. milioni 8, halmashauri zilipokea Sh. milioni 2 na shule zilipokea Sh. milioni 1.

Ripoti ya ufuutiliaji ya mwezi Julai 2022 na taarifa ya utekelezaji ya mwezi Julai 2021 hadi Juni 2022 zilionesha kwamba kulikuwa na kuchelewa kwa utoaji wa fedha kwa ajili ya usimamizi katika ngazi za mkoa na halmashauri. Hatimaye maafisa katika ngazi za mikoa na halmashauri hawakusimamia utekelezaji wa miradi, na kusababisha ubora usioridhisha.

**OR-TAMISEMI inashauriwa kuimarisha mfumo wa utoaji wa fedha ili kuhakikisha kwamba fedha inatolewa kwa kuzingatia gharama halisi na kipindi muafaka cha utoaji wa fedha.**

### **9.3.3 Malipo kwa mafundi bila kufanya ukaguzi makini na tathmini ya kazi iliyofanyika**

Aya 9.4 ya Mwongozo wa kutekeleza ujenzi kwa njia ya kutumia uwezo wa ndani katika utekelezaji wa miradi “force account” ya mwaka 2020 inamtaka Meneja wa Mradi kuthibitisha kazi zilizofanyika na gharama za kazi hiyo. Wahandisi wa wilaya, ambao ndiyo walikuwa mameneja wa miradi, walipaswa kuhakikisha kuwa Hati zote za Malipo/vyeti

vyote vya malipo vilivyoombwa na mafundi vinaambatana na uthibitisho, gharama, na taarifa ya kazi iliyofanywa kabla ya malipo.

Nilibaini kuwa kati ya shule 24 nilizozitembelea, shule 21 zililipa mafundi bila kukagua na kutathmini kazi zilizofanywa. Malipo yalifanyika baada ya kikao cha kamati ya ujenzi kuidhinisha malipo ya cheti kilichotolewa. Ukaguzi pia ulibaini kasoro katika kazi zilizokamilika, ikionesha kuwa ukaguzi uliofanyika haukuwa makini. Kwa mfano, kutokana na ukaguzi usioridhisha na kutofanyika kwa tathmini ya kazi zilizotekelawa za ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Ngome katika halmashauri ya wilaya ya Kilwa kulifanya kuwepo kwa kasoro kama ubora usioridhisha wa majengo yaliyojengwa.

Kati ya shule 24 zilizotembelewa ambazo ujenzi ulikuwa unaendelea, ni shule tano tu ambazo vyeti vyao viliidhinishwa na meneja wa mradi. Shule zilizobaki zililipa mafundi bila ukaguzi wa kiufundi wa kazi iliyofanywa badala yake ilitumia idhini kutoka kwa kamati ya ujenzi. Ukosefu wa ukaguzi huu unaleta hatari ya kufanya malipo kwa kazi ambayo haijafanyika na kwa viwango vinavyohitajika.

**OR-TAMISEMI** inahimizwa kuhakikisha kuwa inatengeneza mfumo wa kuhakikisha kwamba, fedha zilizotengwa kwa miradi zinatumika kwa ajili ya malengo yaliyokusudiwa. Aidha, uhakiki wa kazi unafanyika kabla ya malipo ya vyeti vilivyotolewa.

## **9.4 Utekelezaji wa miradi kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

### **9.4.1 Muundo duni wa timu za utekelezaji**

Aya ya 31 ya Mwongozo wa “force account” wa Mei 2020 inahitaji kuundwa kwa timu za mradi, ikiwa ni pamoja na utekelezaji, ukaguzi na kukubalika, na timu za ununuvi, ili kuhakikisha ununuvi unafanywa kuhusu thamani ya fedha. Kamati zinapaswa kuwa na angalau mjambo mmoja mwenye ujuzi wa kiufundi kulingana na ugumu wa mradi.

Nilibaini kuwa timu za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa shule za kata zilikosa wataalamu na ziliundwa na walimu, wanavijiji na maafisa wa kata, na wanajamii. Wafanyakazi wa kiufundi kama vile

wahandisi, wataalam wa manunuizi, na wataalam wa mazingira na kijamii hawakuwa sehemu ya timu ya utekelezaji, na kazi ya usimamizi na wafanyakazi wa kiufundi kutoka wilaya ilifanyika kwa dharura.

Hii ilisababisha usimamizi usiotosha wa shughuli za ujenzi, kwani ilibidi walimu au wanajamii wafanye kazi za kila siku za usimamizi wa mradi.

#### **9.4.2 Ukaguzi na usimamizi usiotoridhisha katika ujenzi wa shule za kata**

Nilibaini kuwa walimu walikuwa wakifanya usimamizi wa kila siku wa ujenzi wa shule za kata wakati wataalam wa kiufundi kutoka wilayani walifanya usimamizi wa dharura, ambapo ni kinyume na mwongozo katika aya 6.4.5 na 7.2.6 ya Mwongozo wa kutekeleza kazi za ujenzi kwa njia ya kutumia uwezo wa ndani katika utekelezaji wa miradi “force account”, ya mwezi Mei mwaka 2020. Mwongozo huu unamtaka mkurugenzi wa halmashauri kusimamia utekelezaji wa mradi na mhandisi wa halmashauri kuwa na jukumu la shughuli za ujenzi za kila siku.

Hii ilisababisha kasoro katika ujenzi kama vile nyufa kwenye sakafu na kuta, mteremko mkali, matumizi ya mbao zisizokauka vizuri, kazi ya ufundi isiyoridhisha ya shata za milango ya mbao na fremu na upigaji wa rangi za ukutani katika baadhi ya shule zilizotembelewa. Masuala haya yalibainika katika shule nane kati ya 24, ambazo ni sawa na asilimia 33 ya shule zilizotembelewa. Kasoro zilizobainika zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 36**.

#### **Jedwali Na. 36: Kasoro zilizobainika katika shule zilizojengwa na kutembelewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Mapungufu yaliyobainika	Na. za shule zilizobainika kuwa na mapungufu	Asilimia ya shuele zenyne mapungufu
Miteremko mikali	8	33
Kazi ya umalizaji wa milango na fremu zisizo na ubora	6	25
Umalizaji wa kazi ya upigaji wa rangi isiyoridhisha	4	17
Ukuta/sakafu yenyne nyufa	8	33
Paa lisilosikiliwa	3	13

**Chanzo:** Uchambuzi wa data wa wakaguzi katika shule zilizotembelewa, 2023

Ukosefu wa usimamizi wa ujenzi wa shule usioridhisha katika mamlaka za serikali za mitaa umepelekeea mabadiliko mbalimbali katika usanifu bila idhini kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia/OR-TAMISEMI. Angalia **Jedwali Na. 37** hapa chini.

### **Jedwali Na. 37: Mabadiliko ya usanifu na vigezo katika shule zilizotembelewa bila idhini**

Maboresho ya usanifu	Shule katika halmashauri	Jina la shule
Ujenzi wa kuta kwa kutumia kuta za matofali zenyne unene wa mm 150 badala ya mm 230mm	Halmashauri zote isipokuwa Rufiji	Kilangala Mingoyo Somanga Ngome Bupigi Ndembezi Lubaga
Mabadiliko ya usanifu wa paa na ufungaji kwa kuta. Matumizi ya waya wa 'Kench' badala ya 'anchor J'.	Halmashauri zote	Shule zote
Kuondoa nguzo katika jengo la madarasa na upenuni mwa maabara	H/W Kishapu	Bupigi
Matumizi ya vigae visivyoainishwa badala ya sakafu ya saruji	H/W Kishapu na H/W Karagwe	Shule ya Sekondari Bupigi - Imeweka sakafu ya kiwango cha chini na vigae vyatukani chooni Shule ya Sekondari Bashungwa -Imeweka vigae (Twyford) katika madarasa na jengo la utawala
Mbao za paa zimebekwa dawa "Dudu killer" badala ya dawa iliyoainishwa	H/W Muleba	Shule ya Sekondari Buligi
Kuondolewa kwa dari la paa kwenye ukumbi	H/W Kishapu	Shule ya Sekondari Bupigi
Kutumia "barrel bolts" na "pad locks" badala ya "Union Locks" zilizoainishwa	H/W Muleba H/W Karagwe	Shule za Sekondari Mafumbo and Bashungwa
Mabadiliko ya dirisha la mbao la kuwa dirisha za kuteleza za aluminium kwenye jengo la utawala	Halmashauri zote isipokuwa H/W Lushoto	Shule zote isipokuwa Shule ya Sekondari Bagamoyo
Kuungeza ukubwa wa dirisha za madarasa kutoka m 1.5x1.5 hadi m 2.0x1.7 hivyo kuungeza garama	Manispaa ya Shinyanga	Shule ya Sekondari ya Wasichana Ndembezi
Mabadiliko ya usanifu kwa kuunganisha vyoo vyatukani moja ambapo hapana faragha	H/W Mombasa	Shule ya Sekondari Ikana

**Chanzo:** Uchambuzi wa wakaguzi wa data katika shuele zilizotembelewa, 2023

#### **9.4.3 Upimaji wa vifaa vyatya ujenzi usioridhisha kabla ya kutumika kwenye mradi**

Kanuni ya 244 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kinataka vifaa vilivyopokelewa kukaguliwa, kupimwa na kufanyiwa majaribio na taasisi nunuzi na kukataliwa ikiwa havikidhi viwango vilivyowekwa. Mikataba na wazabuni lazima iwe na kipengele kinachowajibisha kwa gharama zinazotokana na kukataliwa kwa vifaa. Sehemu ya 1 ya Viwango vya Ujenzi vya (BS 8110) inataka vipimo vifanyike kwenye chuma na vifaa vya chuma vilivyomo ili kuhakikisha kuwa vinakidhi viwango vilivyowekwa.

Ilibainika kuwa vifaa vya ujenzi vilivyoletwa na wazabuni vilikaguliwa kwa macho kabla ya kukubaliwa bila kupimwa ili kuhakikisha kuwa vinakidhi vigezo vya kiufundi. Vifaa kama nondo, maji ya ujenzi na mabati havikupimwa katika shule zote 24 zilizotembelewa, wakati shule 14 tu (asilimia 58%) zikifanya vipimo vya zege. **Jedwali Na. 38** hapa chini linatoa maelezo zaidi.

#### **Jedwali Na. 38: Hali ya vifaa vya ujenzi vilivyopimwa katika shule zilizotembelewa**

Vifaa vya ujenzi	Namba ya shule ambazo vifaa vya ujenzi vilipimwa kabla ya kutumika	Asilimia ya shule zilizojengwa ambazo zilipima vifaa vya ujenzi
Kokoto	3	13
Mchanga	2	8
Nondo	-	-
Matofali ya saruji	5	21
Ubora wa maji	-	-
Bati	-	-
Zege	14	58

**Chanzo:** Uchambuzi wa data za vifaa vya ujenzi vilivyopimwa katika shule zilizotembelewa, 2023

Upimaji wa vifaa vya ujenzi usioridhisha una athari kwa uendelevu wa mradi kwani unaweka hatari ya kutumia vifaa vya visivyo na ubora katika mradi.

#### **9.4.4 Uhaba wa mafundi wenge ujuzi wa kazi za ufundi wa umeme, mawasiliano ya habari na teknolojia, bomba na ufungaji wa gesi**

Aya 32.5 ya Mwongozo wa utekelezaji wa kazi za ujenzi kwa njia ya kutumia uwezo wa ndani katika utekelezaji wa miradi “force account” ya mwezi Mei mwaka 2020 kinataka mafundi wenge ujuzi kuwasilisha uthibitisho wa vyeti vya kitaaluma kutoka kwa Bodi au Mamlaka husika kwa taaluma hiyo.

Mapitio ya nyaraka za mkataba katika mamlaka za serikali za mitaa kwa mafundi wenge mikataba ilibainika kutokuwasilishwa kwa nyaraka zinazoonesha sifa za kitaalam za mafundi wanaofanya kazi za ufungaji wa bomba, umeme, mawasiliano ya habari na teknolojia, au ufungaji wa gesi katika mradi wa SEQUIP katika shule zote 24 zilizotembelewa. Mamlaka za serikali za mitaa hazikujiridhisha na mafundi wadogo waliopewa mikataba kwa ajili ya kazi maalum ili kuhakikisha sifa na uzoefu wao kwa kazi hizo, na kazi za ufungaji wa huduma zilifanywa na mafundi wengine waliopewa mkataba na fundi mkuu.

Kutokuwepo kwa mafundi wenge ujuzi kwa kazi maalum za ufungaji wa huduma ulitokana na mapungufu katika maandalizi ya nyaraka za mkataba kwani hazikuwa na vipengele vya huduma maalum za ufungaji na mahitaji kwa mafundi wanaotarajiwa kutekeleza kazi za huduma ya ufungaji kuwasilisha uthibitisho wa vyeti vyao vya kitaalam kama inavyooneshwu kwenye **Jedwali Na. 39** hapa chini. Matokeo yake, kazi za huduma ya ufungaji katika shule zilizotembelewa hazikufanyika vizuri kutokana na uhaba wa mafundi wenge ujuzi.

#### **Jedwali Na. 39: Mapungufu ya usimikaji wa huduma kulikotokana na kuwatumia mafundi wasio na sifa**

<b>Jina la Shule</b>	<b>Mapungufu</b>
Shule zote 24 katika hal mashauri	Kutokuwepo kwa ufungaji wa gesi maabara na kabati za kuzuia gesi katika maabara na vyumba vya maandalizi.
Shule zote 24 katika hal mashauri	Kutokuwepo kwa eneo kwa ajili ya ufungaji wa umeme na habari, mawasiliano na teknolojia (ICT) kwenye sakufu ya chumba cha ICT na mabenchi ya maabara.
Mingoyo and Kilangala-H/Manispaa ya Lindi	<ul style="list-style-type: none"><li>• Marekebisho ya muundo wa ufungaji wa umeme kwa majengo yote bila idhini na michoro iliyorekebishwa ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa taa za dari na feni za kwenye dari.</li><li>• Ukosefu wa ufungaji wa mfumo wa maji (masinki kwa ajili haja ndogo(urinals) na ya kuoshea mikono) katika vyoo vya jengo la utawala.</li><li>• Ufungaji mbaya wa mfumo wa maji taka kama vile vifuniko vya chemba visivyofoaa, vifuniko vilivyofungwa kwa zege.</li></ul>

Jina la Shule	Mapungufu
	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kutokuwepo kwa sehemu za kuwekea mabomba kwa ajili ya ukaguzi na kufuta uchafu.</li> </ul>
Ngome- Kilwa Masoko -H/W Kilwa	Kutokuwepo sehemu za kuwekea mfumo wa maji, gesi na kabati za moshi katika maabara na chumba cha maandalizi wakati kazi ya kazi ya kupiga lipu imekamilika.
Ngarambe- H/W Rufiji	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ukosefu wa maji na vifaa nya kuoshea mikono katika vyoo nya wanafunzi na majengo ya maabara.</li> <li>Kutokuwepo kwa sehemu za ufungaji wa mabomba (masinki kwa ajili haja ndogo(urinals) na ya kuoshea mikono) katika vyoo nya jengo la utawala</li> </ul>
Ndembezi - H/Manispaa Shinyanga	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ukosefu wa ufungaji wa usafi wa mazingira katika eneo mbalimbali katika ukumbi wa chakula kabla ya kumwaga saruji.</li> <li>Ubudilishaji wa mpangilio wa choo na ujenzi wa kuta zenyewe urefu kamili zilizotengenishwa, kupunguza uingizaji hewa na mwanga ndani ya vyoo.</li> </ul>
Bipigi - H/W Kishapu	<ul style="list-style-type: none"> <li>Marekebishi ya ufungaji wa umeme kwa kuweka sehemu mbili za taa katika darasani badala ya sita.</li> <li>Ufungaji mbaya wa vituo nya usafi wa mazingira.</li> <li>Vifuniko nya chemba vilivyofungwa.</li> <li>Ufungaji wa vyuma nya metali katika madarasa kinyume na mwongozo</li> </ul>
Karambi (Buligi) - H/W Muleba	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ukosefu wa maji na vyombo nya kuoshea mikono katika vyoo nya wanafunzi.</li> <li>Ujenzi usiofaa wa mfumo wa maji taka (usawa wa chemba ilivyojengwa ili kuwezesha mtiririko) katika jengo la utawala na matumizi ya mabomba ya PVC yasiyo na ubora</li> </ul>

**Chanzo:**Uchambuzi wa data kutokana na uhakiki uliofanyika katika shule zilizotembelewa, 2023

**OR-TAMISEMI** inapaswa kuwajumuisha wataalam wa kiufundi katika timu za utekelezaji wa miradi katika mamlaka za serikali za mitaa, kuimarisha mifumo ya usimamizi, kuhakiki ubora wa vifaa nya ujenzi, na kushirikisha wataalam katika kupata mafundi kwa ajili ya shughuli za ujenzi.



**SURA YA KUMI**



**UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU  
YA MABASI YA MWENDOKASI DAR-ES-SALAAM**

## 10.0 Utangulizi

Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) - Dar es Salaam unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihuisha ujenzi wa miundombinu ambayo ni pamoja na njia za mabasi zenye urefu kilometa 20.3 zilizo katikati ya njia za magari mchanganyiko pamoja na miundombinu kwa ajili ya Usafiri Usiotumia vyombo vya moto kandokando mwa barabara ya Kilwa, sehemu za barabara ya Bandari, Barabara ya Sokoine na Barabara ya Kawawa. Mradi huu unaanzia eneo la Mbagala katika Wilaya ya Temeke hadi katikati ya jiji ambapo unakutana na awamu ya kwanza ya mfumo wa BRT katika vituo vya Kariakoo na eneo la kivukoni kuelekea Zanzibar. Sehemu ya pili ilihuisha ujenzi wa majengo ikiwa ni pamoja na kituo kikuu cha Mbagala, vituo viwili, na vituo vidogo vidogo vitano katika maeneo mbalimbali.

Mradi huu unatarajiwa kuwanufaisha watu wapatao milioni 1.2, sawa na 25% ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam. Wengine watakaonufaika ni watumiaji wa barabara kuu zinazounganisha jiji kuu zikiwemo barabara za Mandela na Nyerere. Mradi unakusudia kuboresha usafiri wa ndani ya mji kwa kupunguza muda wa unaotumika kufika katikati ya jiji na pia kupunguza msongamano. Gharama ya mradi inakadirwa kufikia dola za Marekani milioni 159.32 sawa na Sh. bilioni 285.1 kabla ya kodi. Mradi huu unafadhiliwa kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) (61.1%), Mfuko wa Kukuza Maendeleo ya Afrika (AGTF) (27.8%) na Serikali ya Tanzania (11.1%). Mradi ulitarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne (2016-2020).

Lengo kuu la ukaguzi ni kutathmini iwapo Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) anahakikisha mradi huu unafanyika kwa ufanisi kwa kuzingatia muda, gharama na ubora ili kufanikisha malengo ya mradi. TANROADS ambayo ipo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ndiye msimamizi mkuu wa mradi kwa ujumla akisimamia kazi za ujenzi wa vituo vya basi, eneo la kuegeshea magari, vituo vya basi, madaraja, na njia za kulisha barabara kuu. Hoja na mapendekezo yaliyojitokeza kwenye ukaguzi huu yamejadiliwa kama ifuatavyo;

## 10.1 Usimamizi wa muda

### 10.1.1 Udhibiti wa muda wa kukamilisha mradi usioridhisha

Mapitio ya nyaraka za mradi wa BRT awamu ya 2 yanaonesha ucheleweshaji wa siku 326 katika kukamilisha mradi, ambao umerefushwa kutoka tarehe ya awali ya kukamilika kwa mradi 5 Mei 2022 hadi tarehe 27 Machi 2023. Aidha, wakati wa ukaguzi, maendeleo ya mradi yalikuwa 80.09% kulinganisha na 86.11%, ikionesha kuchelewa kwa 6.02%.

Sababu zilizochangia ucheleweshaji huu, ikiwa ni pamoja na kucheleweshwa kwa malipo kwa mkandarasi, kucheleweshwa makabidhiano ya eneo la kazi kwa mkandarasi, ongezeko la kazi za ziada katika mchanganuo wa kazi (BOQ), mabadiliko katika kazi za usanifu wa awali, kuchelewa kulikosababishwa na mashirika mengine ya serikali (DAWASA, TTCL na TANESCO), muda wa nyongeza kwa sababu ya mabadiliko ya usanifu na muundo wa mradi, kucheleweshwaji wa michoro iliyorekebishwa, utendaji mbaya wa mkandarasi, na usimamizi dhaifu kutoka kwa mshauri na mwajiri.

**TANROADS inatakiwa kuchukua hatua za haraka kushughulikia masuala haya na kusawazisha mikakati yake ya utekelezaji wa mkataba ili kukamilisha mradi ndani ya muda wa nyongeza uliotolewa.**

### 10.1.2 Kuchelewa kuhuisha dhamana ya malipo ya awali

Kifungu cha 14.2 cha Masharti Jumla ya Mkataba kinahitaji mkandarasi kuhakikisha kuwa dhamana inabaki halali na inatekelezeka hadi fidia ya malipo ya awali itakapokuwa imelipwa.

Mapitio yangu ya nyaraka za mradi yalibaini kuwa dhamana ya malipo ya awali ilifikia ukomo tangu tarehe 30 Desemba 2020, mpaka wakati wa ukaguzi huu Novemba 2022 dhamana hiyo ilikua haikuhiushwa licha ya mkandarasi kukumbushwa na TANROADS. Wakati dhamana ilipokwisha muda wake, kulikuwa na kiasi cha Sh. 6,392,778,506.57 ambacho hakijalipwa kama sehemu ya malipo ya awali, hii inaweza kuleta hasara kwa mwajiri. Aidha, TANROADS imeshindwa kukata

kiasi kilichosalia cha dhamana hiyo kutoka kwenye hati za malipo ya mkandarasi (IPC). Badala yake, TANROADS iliendelea kulipwa kiasi kilichosalia kupitia makato ya 30% ya kiasi cha hati za malipo ya makandarasi (IPC) kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 14.2.5 (b) cha Masharti ya Kawaida ya Mkataba na Sehemu A ya Masharti Maalum ya Mkataba.

Napendekeza menejimenti ya TANROADS iimarishe mfumo wake wa usimamizi wa mikataba, uchunguze uwezo wa watendaji wakuu wa Mhandisi Mshauri wa mradi na wakandarasi, utekeleze mpango wa hatua za uhamishaji, na utekeleze masharti ya mkataba yanayosimamia malipo ya awali. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa kazi za ujenzi zinakamilishwa ndani ya ratiba ya kazi iliyoidhinishwa, sababu zinazosababisha kuongezeka kwa muda zinadhibitiwa, na athari zinazohusiana na hasara ya mapato ya serikali zinapunguzwa.

## 10.2 Usimamizi wa ubora wa kazi

### 10.2.1 Ujenzi haukukidhi ubora na viwango vilivyo hitajika

Michoro ya ujenzi wa kazi za barabara inahitaji unene wa milimita 200 ya lami nene “dense bitumen macadam (DBM)” kwa njia za magari yaliyochanganyika kwenye barabara ya Kilwa. Jedwali 7111/4 la mwongozo wa viwango vya barabara linabainisha kiwango cha ukomo cha upungufu wa milimita 15 yaani isiwe chini ya unene milimita 185 kwa daraja la unene wa lami na unene wa safu/tabaka linahitaji kuhakikiwa kila baada ya mita 25 au zaidi.

Hata hivyo, tathmini yangu ilibaini kwamba 12% ya alama za data (*data points*) za barabara nilizokagua sawa na alama 318 kati ya 2,631 zilikuwa na kiwango cha chini cha unene wa milimita 185 za tabaka la lami nene (DBM).

Alama hizi zinaweza kusababisha sehemu dhaifu katika mfumo wa lami. Kasi ya uharibifu wa mfumo wa barabara ni kubwa sana wakati safu ya lami ya DBM ni nyembamba. Hata hivyo, kadri unene wa safu ya lami unavyoongezeka, ndivyo uwezo wa kubebea mzigo wa muundo wa barabara unavyoongezeka, ambayo inamaanisha kuwa barabara

itaharibika polepole, na ubora wa kuendesha utaendelea kuwa juu kwa muda mrefu. Ukosefu wa unene wa DBM nje ya kikomo kilicho ruhusiwa unaonesha udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ubora wa mkandarasi na mfumo wa hakikisho wa ubora wa mshauri. Pia inaonesha kuwa TANROADS haikuweza kuhakikisha kuwa mkandarasi alisimamiwa vizuri na mhandisi mshauri kuweza kuthibitisha kuwa unene uliowekwa wa lami nene (DBM) ulikidhi vigezo vilivyowekwa.

Vipimo vyta mradi wa barabara ya mchanganyiko wa magari karika barabara ya Kilwa ilihitaji unene wa tabaka la lami mnato (Binder course) ya milimita 80. Lakini, hali halisi ilibaini kuwa unene ulianzia 36 mm hadi 187 mm, ikiwa ni unene wa wastani wa milimita 78. Takriban 19% ya pointi za data zilizochunguzwa, karibu alama 503 (au 19%) kati ya alama 2,631 zilizochunguzwa ziliwa nyembamba kuliko kizingiti cha unene wa chini cha 70 mm. Alama hizi zinaweza kusababisha sehemu dhaifu katika mfumo wa lami. Safu ya “binder course” inakuja katika mawasiliano moja kwa moja na magurudumu ya mzigo wa trafiki na anga, kama vile mzigo wa trafiki, mvua, na joto, kabla ya kuweka safu ya kucaa. Kwa hivyo, kiwango cha huduma ya muundo wa lami kitategemea ubora wa lami. Unene wa safu ya lami una athari kubwa kwenye muundo wa uharibifu wa utendaji wa lami.

Aidha, kulingana na sehemu 7,115 ya viwango vyta kawaida kwa kazi za barabara, unene wa tabaka la lami unapaswa kuchunguzwa angalau kila mita 25 kando ya mstari wa kati, mbadala kushoto na kulia ya barabara, lakini hii haikufanya kikamilifu. Ukosefu wa unene wa safu ya “binder course” katika barabara zilizotajwa unaashiria udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ubora wa mkandarasi na mfumo wa uhakikisho wa ubora wa mshauri.

#### **10.2.2 Vifaa vyta ujenzi kutohifadhiwa kulingana na viwango vyta mkataba na vipimo maalum**

Nilibaini kwamba vifaa vyta ujenzi vilirundikwa sehemu moja kwa kinyume na kifungu 3902A(k) cha masharti maalum ya mkataba ambacho kinahitaji kuhifadhi, kupima, na kugawanya vifaa kwa ajili ya zege ili kuhifadhiwa kwa safu zenye unene usiozidi futi tatu kwa kila safu. Kuhifadhi vifaa kwa umbo la koni kunaweza kusababisha

utengano wa vifaa, ambao ungeathiri mgawanyiko wa chembe za kifusi, ambapo ukubwa tofauti za chembe za vifaa zingegawanywa kwa usawa kwa ajili ya kuchanganya zege. Kwa kuongeza, kokoto hazikuhifadhiwa vizuri ili kuhifadhi ubora wake, na vifaa vilivyo hifadhiwa vilikuwa chini ya mti wa mwembe, ambapo majani ya mti na uchafu mwozo vilidondo kea kwenye kokoto jinsi zilizohifadhiwa.

Nilibaini kuwa unene uliozidi ulisababishwa na uchafuzi wa uozo (organic) uliopelekeea kuondolewa kwa mipako, ambayo ni utenganishaji wa kiungo cha lami kutoka kwenye kokoto ambayo hupunguza utendaji na ubora wa barabara iliyojengwa. Kasoro iliyobainishwa inaonyesha kuwa TANROADS haikuhakikisha kwamba mkandarasi alisimamiwa ipasavyo na mhandisi mshauri ili kuhakikisha ubora wa vifaa unalindwa kwa kuhifadhiwa ipasavyo.

#### **10.2.3 Uimara duni wa miundo ya zege**

Niligundua kuwa baadhi ya miundo ya zege iliyopimwa haikutimiza kiwango kinachohitajika cha uwezo wa zege. Kwa mfano, uwezo wa ngazi upande wa kulia wa daraja la juu la waenda kwa miguu Mbagala ilikuwa  $22 \text{ N/mm}^2$  kati ya  $40 \text{ N/mm}^2$ , na uwezo wa vizuizi vya ajali upande wa kushoto na kulia vya makutano ya barabara ya juu ya Kilwa na Mandela vilikuwa 28 na 23 mtawalia ukilinganisha na  $40 \text{ N/mm}^2$  inayohitajika.

Mapungufu haya yanatokana na udhibiti duni wa joto, ubora mbaya wa malighafi, kutofuata uwiano wa kuchanganya, na sababu zingine.

Kutowiana na kiwango kinachohitajika kuliadhihirisha udhaifu katika mfumo wa uhakiki na udhibiti wa ubora wa mhanisi mshauri na mkandarasi mtawalia. Miundombinu iliyopimwa ambayo haijatimiza uwezo na kiwango kinachotakiwa iko hatarini kwa kuendeleza au nyufa za usinyao na joto na upungufu wa uwezo wa tabaka la juu.

**Napendekeza menejimenti ya TANROADS kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa maelekezo ya mshauri kwa mkandarasi, kuhakikisha unafuatwa na udhibiti wa ubora na viwango vya uhakiki wa ubora wa unene wa tabaka /safu ya lami na unene wa**

lami nene, na kuhakikisha kuwa mhandisi mshauri anasimamia mkandarasi kulingana na masharti ya mkataba.

### 10.3 Usimamizi wa gharama za ujenzi

#### 10.3.1 Ongezeko la gharama za ushauri kutokana na mabadiliko ya usanifu Sh. bilioni 7.67

Mapitio yangu yamebaini kuwa mabadiliko ya mawanda ya kazi kwa miradi ya Lot 1 na 2 yamesababisha kuzidi kwa gharama za mkataba wa ushauri wa awali kwa 107% na 67% mtawalia. Lot 1 ilikuwa na kiasi cha Sh. 7,031,346,281.94 zaidi kutokana na nyongeza nne, wakati Lot 2 ilikuwa na kiasi cha Sh. 635,937,655 zaidi kutokana na nyongeza tano kama inavyo onekana katika Jedwali Na. 40.

#### Jedwali Na. 40: Ongezeko la kipande cha kwanza

Mkataba	Kiasi cha mkataba wa kwanza (Sh.)-A	Kiasi cha mkataba uliorekebishwa (Sh.)-B	Jumla ya gharama za nyongeza (B-A)
Mkataba wa kilichokubaliwa	6,543,718,364.25	-	-
Nyongeza 1	364,929,716.25	6,908,648,080.50	364,929,716.25
Nyongeza 2	1,543,773,534.38	8,452,421,614.88	1,908,703,250.63
Nyongeza 3	232,992,550.82	8,685,414,165.69	2,141,695,801.44
Nyongeza 4	4,889,650,480.50	13,575,064,646.19	7,031,346,281.94
Jumla	13,575,064,646.19	13,575,064,646.19	7,031,346,281.94

**Chanzo:** Uchambuzi wa nyaraka na nyongeza za mkataba za mwaka 2022

Mabadiliko katika mawanda ya kazi yalitokana na marekebisho ya muundo wa daraja la pili la reli juu ya barabara ya Gerezani-Bandari, huduma zaidi za kuboresha makutano ya barabara ya KAMATA, utafiti kamili wa kihaidrolojia na usanifu wa kihandisi wa kina uliopangwa katika sehemu ya kilometra nn3 na mita 950 (Km. 4+950) kwenye barabara ya Kawawa, usanifu ambao haukukamilika/usio timilifu ununuzi wa ardhi na uhitaji wa wafanyakazi wa huduma za mhandisi mshauri wa ziada ili kuimarisha huduma za usimamizi.

Napendekeza menejimenti ya TANROADS ihakikishe inamkata fedha mkandarasi na mshauri wa mradi kutoka kwenye madai ya malipo (IPCs) yao ikiwa kuna uhalali wa kufanya hivyo kimkataba. Aidha, ishirikiane na Wizara ya Ujenzi na Usafirishaji kuhakikisha

kwamba muda wa kuidhinisha malipo unakua mfupi, mshauri wa mradi kuchukuliwa hatua za kimkataba atakaposhindwa kutekeleza mapendekezo ya usanifu wa mchoro wa mradi, na kumsimamia mkandarasi kwa ukaribu ili atimize matakwa ya mkataba kikamilifu.

#### 10.4 Mazingira, afya na usalama

##### 10.4.1 Hatua za kupunguza athari za kimazingira hazichukuliwi kwa ukamilifu

Katika ukaguzi wa ujenzi wa barabara za Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Pili, nilibaini kuwa TANROADS hawakufuatilia kwa ufanisi utendaji wa mkandarasi katika kushughulikia hatua za kupunguza athari zilizobainishwa katika mpango wa usimamizi wa mazingira wa mradi huo. Hali hii inapingana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003 na Kifungu cha 12.2.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba ambacho kinahitaji kwamba wakati wote mkandarasi achukue hatua za kuepuka uchafuzi wa mito, mifereji na mazingira kwa petroli, mafuta au vifaa vingine vinavyoweza kuleta madhara.

Niliona mafuta machafu (ya grisi) yaliyosambaa juu ya udongo katika kambi ya wafanyakazi ya Mbagala, kambi ya Taifa na daraja la Bandari-Gerezani kando ya barabara ya Kilwa. Katika kambi ya Taifa, lami ilisambaa kwa kiasi kikubwa ardhini kutoka kwenye mapipa au makontena ya lami. Usambazaji wa mafuta/grisi na lami unachafua ardhi na maji ya chini ya ardhi.

Katika madaraja ya Tazara-Mtongani na Bandari-Gerezani, kulikuwa na utekelezaji usiofaa wa hatua za kuzuia mmomonyoko na hakuna hatua za kudhibiti mmomonyoko wa udongo, ambayo huzuia mmomonyoko wa udongo.

Ninapendekeza kwamba TANROADS ihakikishe wakandarasi wanazingatia masharti ya kimkataba kuhusu usalama na mazingira,

na kutibu maji machafu mahali yanapozalishwa, na kuhuisha maeneo yote yaliyoathiriwa na ujenzi.

## 10.5 Usimamizi wa rasilimali watu

### 10.5.1 Wafanyakazi wa kigeni wa mkandarasi kutokuwa na vibali vyakazi

Kifungu cha 9 (2) (a) cha Kanuni za Ajira za Wasio Raia ya mwaka 2015 kinazuia kuajiri mtu ambae si raia mpaka awe anamiliki kibali halali cha kazi ambayo inatambulika.

Wakati wa mapitio yangu ya nyaraka za maafisa wa ngazi ya juu wa mkandarasi (Sinohydro Corporation Limited) kuhusiana na Lot 1, nilibaini kwamba maafisa sita kati ya 11 waliochaguliwa kama sampuli walikuwa wanafanya kazi bila vibali vyakazi, kinyume na kanuni za ajira.

Hii inasababishwa na jitihada ndogo zilizowekezwa na maafisa hao wa kigeni katika kukamilisha taratibu zinazohitajika za kupata vibali, kutokuwepo kwa mfumo wa kuhakikisha kuwa vibali vyakazi vinashughulikiwa kabla ya kuwasili kwa wafanyakazi wa kigeni nchini, na ukosefu wa ushirikiano wa kutosha kati ya mamlaka husika za serikali kuhusiana na vibali vyakazi na kazi.

Kuwepo kwa wakazi na wafanyakazi wa kigeni haramu kunatishia usalama wa nchi na kusababisha upotevu wa mapato ya serikali, ambapo kwa mkandarasi huyu imefikia kiasi cha dola za kimarekani 6,000 sawa na Sh. 13,800,000, ikizingatiwa kuwa ada ya vibali vyakazi ni kiasi cha Dola za Kimarekani 1,000 kwa miaka miwili, taarifa za wafanyakazi hao zinaonekena katika **Jedwali Na. 41** hapo chini.

#### **Jedwali Na. 41: Wafanyakazi wa kigeni wasiokuwa na vibali vyakazi**

Na.	Maelezo
1	Meneja Uthibiti Ubora/Mhandisi Mkuu
2	Mhandisi wa Barabara
3	Mhandisi Majenzi/Madaraja
4	Meneja wa Karakana
5	Mhandisi wa Umeme
6	Mtaalamu wa Upimaji Ardhi

**Chanzo:** Kumbukumbu za wafanyakazi wa mkandarasi

### **10.5.2 Wataalamu wa kigeni wanaofanya kazi pasipo kusajiliwa na bodi za kitaaluma za ndani**

Kifungu cha 6.12 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinahitaji kampuni kusajiliwa na bodi za ndani kama Bodi ya Usajili wa Wakandarasi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, na Bodi nyingine za kitaalamu.

Nilifanya ukaguzi kwa kuchukua sampuli ya maafisa 10 wa ngazi ya juu wa mkandarasi kutoka katika kipande cha kwanza ( Lot 1) nakubaini kwamba maafisa wanane sawa na 80% ya sampuli hawajasajiliwa na bodi za kitaalamu za ndani kama inavyooneka katika **Jedwali Na. 42** hapo chini.

#### **Jedwali Na. 42: Wafanyakazi wa kigeni walioajiriwa bila usajili wa bodi za kitaalamu za ndani**

Na.	Maelezo
1	Meneja Mikataba
2	Mhandisi wa Barabara
3	Mhandisi Majenzi/Madaraja
4	Mhandisi wa Udongo/Vifaa
5	Meneja wa Karakana
6	Mhandisi wa Umeme
7	Mtaalamu wa Upimaji Ardhi
8	Meneja wa Mazingira na Jamii

*Chanzo: Kumbukumbu za wafanyakazi wa mkandarasi*

Hali hii imetokana na udhaifu katika ufuatiliaji na usimamizi wa mradi. Kutokuwa na ithibati kutoka kwa bodi za kitaalamu za ndani kunaleta ugumu katika kujiridhisha kama wafanyakazi wenye ujuzi, uzoefu, maarifa, na ujuzi unaohitajika kwenye kutekeleza majukumu ya mradi kwa ufanisi.

Ninapendekeza kwamba TANROADS ihakikishe washauri na wakandarasi wa mradi ambao si raia wa Tanzania wanakuwa na vibali vya kazi, sifa na wanasajiliwa na bodi za kitaaluma za ndani. Aidha, kabla ya kuidhinisha maafisa wa ngazi ya juu ambao ni raia wa kigeni, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) wahuishwe katika kutathmini sifa zao.

## **10.6 Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi**

### **10.6.1 Utekelezaji usioridhisha wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita**

Nimebaini utekelezaji usioridhisha wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita yanayohusiana na miundombinu ya barabara za mabasi ya mwendokasi (BRT) awamu ya pili ambayo iliwasilishwa kwenye Bunge mnamo mwezi Aprili 2021. Kati ya mapendekezo yote 41 yaliyotolewa (mapendekezo 40 yanahusiana na TANROADS na pendeleko moja linahusiana na DART), mapendekezo sita yalitekelezwa kikamilifu na mapendekezo 35 yalitekelezwa kwa sehemu, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 43 na 44** hapo chini.

#### **Jedwali Na. 43: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa kila hatua ya ununu**

Hatua ya ugavi	Jumla ya Mapendekezo	Yaliyotekeliza	Yaliyotekeliza kwa sehemu
Kupanga (planning)	4	-	4
Ubunifu (designing)	3	-	3
Zabuni (tendering)	1	1	-
Usimamizi wa mkataba	32	4	28
Hatua zingine	1	1	-
Jumla	41	6	35

**Chanzo:** Majibu ya wakaguliwa kuhusu mapendekezo ya ukaguzi ya mwaka 2021/22

#### **Jedwali Na. 44: Hali ya utekelezaji kwa taasisi**

Taasisi	Hali ya utekelezaji			Jumla
	Yaliyotekeliza	Yaliyotekeliza	Yasiyotekeliza	
TANROADS	6	34	-	40
DART	-	1	-	1
Jumla	6	35	-	41

**Chanzo:** Majibu ya wakaguliwa kuhusu mapendekezo ya ukaguzi ya mwaka 2021/22

TANROADS na DART wanaweza kuwa hatarini kwa kutoimarika kiutendaji na kuathiri ufanisi kwenye kutekeleza mradi ikiwa mapendekezo ya ukaguzi hayatakelezwa kwa ukamilifu na ndani ya wakati.

TANROADS inapaswa kuweka mfumo imara wa kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi na Usafirishaji pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango

kupunguza muda wa kuidhinisha malipo yasiyofanyika kwa wakati kwa wakandarasi na washauri, ambayo yanaweza kusababisha malipo ya riba na fidia ya kukiuka mikataba.





# SURA YA KUMI NA MOJA



**UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU  
YA MABASI YA MWENDOKASI DAR-ES-SALAAM**

## 11.0 Utangulizi

Serikali ya Tanzania inatambua maendeleo ya mtandao wake wa barabara kama mkakati muhimu wa kusaidia ukuaji wa kijamii na kiuchumi. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, serikali imetenga wastani wa Sh. trilioni 47.33 kila mwaka kwa ajili ya kuendeleza barabara kuu za mikoa. Miongoni mwa miradi ya barabara inayoendelea ni pamoja na ujenzi wa sehemu kadhaa, zikiwemo Sehemu ya Mvugwe - Makutano ya Nduta, Makutano ya Nduta - Sehemu ya Kabingo, Makutano ya Kanyani - Sehemu ya Mvugwe, na Makutano ya Kasulu - Manyovu ikijumuisha barabara za mjini, kwa kiwango cha lami, iliyogharimu Sh. bilioni 217.54.

Miradi hii inafadhiliwa na serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo Afrika. Miradi mingine ilioanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22 ni pamoja na ujenzi wa Barabara ya Itoni - Ludewa - Manda (kilomita 211.4) yenye Kipande cha 1: barabara ya Itoni - Lusitu (kilomita 50) na kipande cha 2: barabara ya Lusitu - Mawengi (kilomita 50) kuweka kiwango cha zege. Miradi hii ilikusudiwa kuchangamkia fursa za kiuchumi zinazopatikana katika kilimo na uchimbaji wa madini. Zaidi ya hayo, Wakala wa Barabara Tanzania(TANROADS) inaboresha sehemu ya Kidatu hadi Barabara ya Ifakara yenye urefu wa kilometra 66.9 kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na Daraja la Ruaha, linalofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Ulaya na Serikali ya Tanzania. Mfuko ambao tayari umejitolea kwa ajili ya ujenzi kiasi cha Euro milioni 42.08 (Sh. bilioni 103.81). Hata hivyo, pendekeso la kurekebisha gharama ya mkataba hadi Euro milioni 49.92 (Sh. bilioni 123.16) bado linasubiri idhini.

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathimini kama TANROADS alitekeleza ipasavyo ujenzi wa Barabara ya Kabingo - Kasulu - Manyovu, Uboreshaji wa Barabara ya Itoni - Ludewa - Manda, kipande cha 1: Sehemu ya Barabara ya Itoni - Lusitu na uboreshaji wa barabara ya Kidatu - Ifakara kwa kuzingatia muda, gharama, na ubora. Ukaguzi ulihusisha muda usiozidi miaka sita ya fedha, kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22. TANROADS ndiyo iliyokaguliwa kama watekelezaji wakuu wa miradi ya barabara na madaraja nchini Tanzania chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Matokeo muhimu yanawasilishwa katika aya zifuatazo.

## 11.1 Upangaji na usanifu wa mradi

### 11.1.1 Upana wa barabara uliofanyiwa ubunifu/usanifu ulikuwa chini ya mita 7.5

Sehemu ya 2.5 ya Mwongozo wa Usanifu wa Kijiometri wa Barabara (RGDM) ya mwaka 2011 unataka upana wa usanifu wa barabara uwe mita 7.5 kwa daraja la 2 la usanifu wa barabara kwa barabara zenyen wastani wa magari zaidi ya 7000 kwa kila siku kwa mwaka mzima. Mapitio ya mchoro namba KI/RD/01 na usanifu wa kina uliotayarishwa na M/S Crown Tech Co Ltd, na kutembelea miradi mitatu, yalionesha kuwa upana wa usanifu wa barabara ulikuwa chini ya mita 7.5 kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 45**.

#### Jedwali Na. 45: Maelezo ya kina ya usanifu

Jina la Mradi	Wastani wa Magari kwa Siku Mwaka	Upana wa Barabara unaotakiwa (mita)	Vipimo halisi (mita)	Utofauti wa vipimo vya upana wa barabara (mita)
Ujenzi wa Barabara ya Kidatu - Ifakara kwa Kiwango cha Lami ikijumuisha Daraja la Mto Ruaha	7,551	7.5	6.5	1.0
Ujenzi wa Barabara ya Itoni - Lusitu Sehemu ya 1: kwa Kiwango cha Zege	4,136	7.5	7.0	0.5
Ujenzi wa Barabara ya Lusitu - Mawengi Sehemu ya 2: kwa Kiwango cha Zege	7,551	7.5	6.5	1.0

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi Juu ya Ubunifu wa Barabara, 2023

TANROADS walitumia Mwongozo wa Usanifu wa Uganda badala ya miongozo ya kitaifa ya usanifu wa mradi wa barabara ya Itoni-Lusitu kipande cha 1. Chaguo la daraja la chini la usanifu wa barabara linaweza kuhatarisha usalama wa barabarani na kusababisha ajali kwa watumiaji wa barabara.

Nilibaini kuwa mwendokasi uliyopendekezwa wa sehemu tambarare hadi yenyeye mteremko ulikuwa km 100 kwa saa na sehemu yenyeye mteremko hadi kilimani ulikuwa km 80 kwa saa kutokana na usanifu wa kiwango cha chini cha usanifu wa daraja la barabara. Menejimenti ya TANROADS ilihalalisha upana uliopunguzwa wa barabara kuwa mita 7.0 badala ya mita 7.5 kama inavyotakiwa katika Mwongozo wa Usanifu wa Kijiometri kwa Barabara wa Mwaka 2011 kutokana na sababu ya ulinganisho wa gharama ya Sh. Bilioni 3.0 kwa kilomita, lakini haikuweza kutoa ushahidi wa maandishi kuhusu upana uliopunguzwa kuhusiana na uhakikisho wa usalama kwa watumiaji wa barabara.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya TANROADS itumie Mwongozo wa Usanifu wa Kijiometri wa Barabara wa mwaka 2011 katika kufanya usanifu wa miradi.**

## **11.2 Usimamizi wa ununuzi**

### **11.2.1 Mchakato wa manunuzi uliochukua muda mrefu wa mkataba wa Kabingo - Kasulu - Manyovu**

Kifungu cha 71 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 (iliyorekebishwa mwaka 2016) kinawataka wazabuni kuweka zabuni zao na dhamana zao halali kwa muda ulioainishwa kwenye nyaraka za zabuni. Kipindi hiki cha uhalali wa zabuni kinapaswa kuwa kirefu vya kutosha kukamilisha ulinganifu na tathmini ya zabuni, na kwa bodi ya zabuni kupitia mapendekezo na kuidhinisha kandarasi itakayotolewa wakati zabuni zingali bado ni halali.

Mchakato wa ununuzi wa mradi wa Uboreshaji wa Sehemu ya Barabara ya Makutano ya Kanyani - Mvugwe ulianza tarehe 27 Disemba 2018. Mikataba ya vipande vya 1, 2, 3, na 4 ilisainiwa tarehe 15 Juni 2020, 16 Juni 2020, 15 Septemba 2020, na tarehe 24 Desemba 2020 mtawalia. Muda wa kuanza kwa mchakato wa manunuzi hadi kusainiwa kwa mkataba ulikuwa siku 536, siku 537, siku 628 na siku 728 kwa kipande cha 1, 2, 3, na 4 mtawalia.

Mchakato wa muda mrefu wa ununuzi ultokana na mchakato mrefu wa kuidhinisha utoaji wa "Idhini/Kibali" kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB). Ucheleweshaji wa mchakato wa manunuzi unaweza

kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi na kuchelewa kufikia malengo ya mradi.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya TANROADS iwasiliane na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) ili kupunguza muda wa kutoa "Idhini/Kibali" ili miradi ianze kwa wakati kama ilivyopangwa.**

#### **11.2.2 TANROADS ilichelewa kushirikisha wahandisi washauri katika uboreshaji wa mradi wa barabara ya Itoni - Lusitu kipande cha 1 na Kabingo - Kasulu - Manyovu (Mvugwe - Nduta Junction) kipande cha 3**

Kanuni ya 252(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) inampa Afisa Masuuli mamlaka ya kuteua mshauri mwelekezi mara moja wa kusimamia kazi za kandarasi inapobidi.

Kulikuwa na ucheleweshaji wa kushirikisha washauri wa Uboreshaji wa Mradi wa Barabara ya Itoni - Lusitu Sehemu ya 1 na Mvugwe - Makutano ya Nduta kipande cha 3. Mkataba wa kazi za ujenzi wa Uboreshaji wa Mradi wa Barabara ya Itoni - Lusitu kipande cha 1 ulisainiwa tarehe 29 Machi 2022, lakini mchakato wa manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usimamizi wa kazi za ujenzi, ulioanza tarehe 9 Septemba 2021, haukumpata Mhandisi Mshauri hadi kufikia Oktoba 2022, na kusababisha ucheleweshaji usio wa lazima. Vile vile, Sehemu ya Mvugwe - Makutano ya Nduta kipande cha 3, kulikuwa na ucheleweshaji wa miezi saba katika kumshirikisha mshauri msimamizi, na mkataba ulitiwa saini tarehe 15 Septemba 2020, licha ya kuanza kazi tarehe 26 Oktoba 2020.

Kupishana kwa muda katika utiaji saini wa mkataba kunawenza kuathiri mkataba wa kazi, kwani mkandarasi anahitaji mwongozo kutoka kwa mshauri kuanzia mwanzo wa utekelezaji.

Maofisa wa TANROADS walisema kuwa kuchelewa kwa mshauri mwelekezi wa kipande cha 3 kumetokana na mchakato mrefu wa kupata kibali kutoka Benki ya Maendeleo Afrika kwa ajili ya hatua mbalimbali za mchakato wa manunuzi. Pia sababu zingine zilikuwa mazungumzo kwa ajili ya mapatano kuhusu kandarasi, athari za

Uviko - 19 na idadi kubwa ya maombi ya nia ya kufanya kazi (276), kama sababu zinazochangia.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya TANROADS iimarishe utaratibu wa udhibiti ili kupunguza muda mrefu wa upatikanaji unaohusika katika manunuzi ya mshauri mwelekezi.**

#### **11.2.3 Kutojumuisha vitu/vipengele muhimu katika mchakato wa zabuni ya mradi wa ujenzi wa kuboresha barabara ya Lusitu-Mawengi kipande cha 2 kwa kiwango cha zege**

Kifungu cha 39(1)(c) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) kinaeleza moja ya kazi za idara ya watumiaji wa taasisi nunuzi ni kuandaa michango ya kiufundi kwa taarifa za mahitaji na/au hadidu za rejea kwa mahitaji ya manunuzi kwa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi.

Wakati wa mapitio ya nyaraka za zabuni ya Mradi wa Barabara ya Lusitu-Mawengi kipande cha 2, ilibainika kuwa baadhi ya vitu muhimu havikujumuishwa kwenye nyaraka za zabuni, hususani nondo (chuma) zenye uimara wa kiwango cha juu kwa ajili ya kuweka kwenye tabaka la juu la barabara (Wearing course), njia ya ziada kwa ajili ya magari kupandisha na sehemu ya maegesho ya basi yenye kiasi cha tani 5,372 na nailoni ngumu ambayo huwekwa juu ya barabara kutenganisha kati ya msingi na tabaka la zege kiasi cha mita za mraba 578,270.

Agizo la Mabadiliko Na.01 lilitolewa kwa mkandarasi kuwasilisha nukuu ya bei ya bidhaa hizo, lisababisha ongezeko la bei ya mkataba kwa Sh. 10,226,800,000.00 na Sh. 980,167,650.00 kwa chuma na polyethylini, mtawalia, wakati wa utekelezaji wa mkataba.

Mapitio yasiyotosheleza ya nyaraka za zabuni na idara ya watumiaji kabla ya kutolewa kwa wazabuni yalifahamika kama sababu kuu ya suala hili. Kuachwa kwa vipengele hivi katika hatua ya zabuni

kunazua wasiwasi kuhusu ushindani na uhalisia wa bei zilizonukuliwa.

Ninapendekeza kwamba menejimenti ya TANROADS iimarishe utaratibu wa udhibiti ili kuhakikisha kuwa idara za watumiaji zinapitia ipasavyo nyaraka za zabuni zilizotayarishwa na kujumuisha vitu/vipengele vyote muhimu kabla ya kuwasilisha nyaraka za zabuni kwenye bodi ya zabuni kwa ajili ya kuidhinishwa.

### 11.3 Usimamizi wa mikataba

#### 11.3.1 Itifaki isiyofaa ya kubadilisha tabaka za barabara kutoka matabaka matatu za mm 150 kila moja (mm 450) hadi matabaka mawili ya mm 200 na mm 250

Ukaguzi ulibaini kuwa viwango vya awali vya usanifu/ubunifu kwa ajili ya tabaka ndogo za chini zilizoboreshwu katika Mkataba Na. TRD/HQ/1012/2020/21 kwa kipande cha 3 zilihitaji matabaka mawili ya milimita 150 kila moja ya udongo wenye daraja la 7 la ubora (G7) na tabaka/safu moja ya milimita 150 ya udongo wenye daraja la 15 la ubora (G15), na kufanya jumla ya unene wa tabaka la barabara kuwa milimita 450. Hata hivyo, Mkandarasi alipendekeza kubadilisha unene wa tabaka hadi milimita 250 za G7 na milimita 200 ya G15, ambayo iliidhinishwa na Mhandisi Mshauri bila kushauriana na Mwajiri (TANROADS).

Mkandarasi kisha alijenga kilomita 23.090 za barabara kwa kutumia marekebisho yake, kinyume na maelezo ya awali ya viwango vya usanifu wa barabara. Kukosekana kwa mawasiliano kati ya wahusika kumesababisha kuvunjika kwa uaminifu na migogoro inayoweza kutokea.

Ninahitimisha kuwa kuidhinishwa na utekelezaji wa mabadiliko ya unene wa tabaka dogo lililoboreshwa bila kushauriana na TANROADS kulikiuka sehemu ndogo ya 20.1 ya Masharti ya Jumla ya Mkataba na Kifungu cha 5.1(w) cha Hadimu Rejea, ambayo inamtaka Mhandisi Mshauri kushauriana na TANROADS kabla ya kufanya mabadiliko hayo ambayo yangeboresha usanifu au viwango vya kazi. Kutokana na hali

hiyo, TANROADS ilimtaka Mshauri Mwelekezi kutoa mbadala wa Mhandisi Mkazi na Mhandisi wa Barabara kwa mujibu wa Kifungu kidogo cha 32.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba. Kubadilika kwa unene kunaweza kuathiri ubora wa ujenzi wa barabara, na kusababisha hatari zinazoweza kutokea kwa watumiaji wa barabara.

TANROADS inapaswa kuhakikisha kuwa mabadiliko yote yanayopendekezwa kwenye viwango vya usanifu yanaandikwa na kuwasilishwa kwa pande zote zinazohusika, akiwemo Mwajiri. Mhandisi Mshauri anapaswa kujadilina mabadiliko yoyote yaliyopendekezwa na Mwajiri kabla ya kuyaiddinsha, kulingana na masharti ya mkataba. Ukaguzi wa mara kwa mara wa maeneo ya mradi unakofanyika unapaswa kufanywa ili kuhakikisha kwamba ujenzi unalingana na viwango vya usanifu vilivyoidhinishwa. Zaidi ya hayo, hatua zinazofaa zinapaswa kuchukuliwa ili kuwawajibisha wahusika kwa hitilafu zozote kutoka kwa vipimo vya awali vya usanifu ili kuhakikisha ubora wa mradi hauathiriwi. Hii ni pamoja na kutekeleza agizo la TANROADS la kutafuta mbadala wa nafasi ya Mhandisi Mkazi na Mhandisi wa Barabara anayesimamia kipande cha 3 kwa ajili ya usimamizi mzuri wa mradi.

#### **11.3.2 Ubora hafifu (ubora usiotosheleza) wa miundo ya zege iliyojengwa**

Kifungu cha 61.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinamtaka Mkandarasi kuwa na jukumu la kurekebisha kasoro au uharibifu wowote kwa gharama zake mwenywewe na haraka iwezekanavyo.

Nilibaini madhaifu yafuatayo katika miundo ya zege iliyojengwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 46 hapo chini:

## Jedwali Na. 46: Mapungufu katika miundo iliyotengenezwa

Matokeo ya Ukaguzi	Maelekezo	Tarehe ya Ukaguzi	Picha
(a) Nyufa kwenye Daraja la Makere	Nyufa zilizoonekana kwenye Daraja la Makere lililopo Km 110+407 katika Sehemu ya 2 ya Makutano ya Kanyani - Mvugwe Barabara ya Mvugwe (Km 70.50) kutokana na tatizo la ujenzi. Mkandarasi ameshirikisha wataalam kusoma sababu na hatua za kuchukua.	4 Novemba 2022	
(b) Nyufa kwenye Zege kwenye makalvati kutokana na mkandamizo/msuguan o	Nyufa kutokana na mkandamizo/msuguan o zilizoonekana kwenye kalvati la pembe nne na kalvati la muundo wa duara kando ya Barabara ya Kidatu-Ifakara. Maafisa wa TANROADS walibaini kasoro hizo na Mkandarasi atazirekebisha kabla ya kumalizika kwa Kipindi cha mazazamio. Ufutiliaji duni wa maeneo ya mradi unaweza kuhusishwa na kasoro hizi.	3 Novemba 2022	

Matokeo ya Ukaguzi	Maelekezo	Tarehe ya Ukaguzi	Picha
(c) Kasoro za ubora kwenye barabar a ya Lusitu-Mawengi	Nyufa zilizobainika kwenye kazi za zege zilizotekelzewa kwenye mradi wa Barabara ya Lusitu-Mawengi Sehemu ya 2 kutokana na kuchelewa kwa uwekaji wa kitenganishi cha kuziba maungio ya sakafu mbili kwa pamoja na athari katika ufanyaji kazi.	1 Novemba 2022	

Chanzo: Picha iliyochukuliwa wakati wa kutembelea mradi, 2022

Menejimenti ya TANROADS inapaswa kuhakikisha kuwa kuna nyaraka na mawasiliano sahihi ya mabadiliko yoyote yanayopendekezwa kwenye usanifu wa mradi, ukaguzi wa mara kwa mara wa eneo ili kuhakikisha uzingatiaji wa ujenzi, na kuwawajibisha wahusika kwa ukiukaji wowote kutoka kwa vipimo vya awali vya usanifu vilivyopendekezwa. Zaidi ya hayo, wamuelekeze mshauri msimamizi wa kipande cha 2 kushughulikia kwa kina nyufa za Daraja la Makere, kufanya utafiti wa tathmini ya miundo yote yenye kasoro kwenye mradi wa barabara ya Kidatu-Ifakara, na kuhakikisha kuwa kasoro zote za miundo thabiti zinarekebishwa kulingana na mahitaji ya kiufundi na kimkataba.

### **11.3.3 Kipande cha 3: Makutano ya barabara ya Mvugwe - Nduta ilitumia gharama ya ziada ya Sh. bilioni 4.41 kwa ajili ya kudhibiti mchwa bila idhini kutoka kwa mwajiri**

Kanuni ya 110(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) inahitaji kwamba, mabadiliko yoyote yanayopendekezwa ambayo hayahusiani na au yanayotokana nje ya mkataba, na ambayo yanabadilisha mawanda/upeo, kiwango, au nia ya mkataba, lazima yawasilishwe kwenye bodi ya zabuni husika ili kupata idhini kabla ya maagizo kutolewa kwa mzabuni.

Mkataba wa awali haukujumuisha kiwango cha fedha kudhibiti mchwa, lakini Mwajiri aliidhinisha kiwango cha Sh. 29,163.30 kwa lita kwa lita 20,000, sawa na Sh. 583,266,000. Hata hivyo, hadi kufikia Novemba 2022, Mkandarasi alikuwa ametumia Sh. 4,991,853,189.33 kwenye kifungu hiki, kiasi cha ziada cha Sh. 4,408,587,189.33 kilitekelezwa bila idhini ya awali. Kiasi cha fedha kilichoongezeka cha kutekeleza nyongeza rasmi ya kazi bado hakijaidhinishwa na Bodi ya Zabuni ya Makao Makuu ya TANROADS. Hii inaweza kuongeza gharama ya mradi.

TANROADS inapaswa kuboresha usimamizi wa mikataba na kuhakikisha kuwa mshauri mwelekezi anamsimamia mkandarasi ipasavyo. Endapo shughuli hazijajumuishwa kwenye makadirio ya gharama za ujenzi, mkandarasi anapaswa kuzitekeleza tu kulingana na idadi iliyoidhinishwa na mwajiri.

### **11.3.4 Usimamizi duni wa masuala ya uhamiaji kwa wafanyakazi wa kigeni**

Kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Wasiokuwa Raia (Kanuni ya Ajira), (Sura ya 436) inasema mwajiri yeyote aliyeko Tanzania Bara na anayetaka kumuajiri raia wa kigeni kufanya kazi yoyote ataomba kibali cha kazi kwa Kamishna wa Kazi.

Nilibaini madhaifu yafuatayo kuhusu masuala ya uhamiaji kwa wafanyakazi wa kigeni.

- (a) Hadi Novemba 2022, wataalam wote 15 walifanya kazi bila vibali kabla ya kuanza kwa Mkataba Na. TRD/HQ/1050/2021/22 kwenye kipande cha 1 cha ujenzi wa barabara ya Itoni - Lusitu kwa kiwango cha zege.
- (b) Kuchelewa kupata vibali nya kazi kabla ya kuanza kwa Mkataba Nambari TRD/HQ/1009/2016/17 kipande cha 2 ya ujenzi wa barabara ya Lusitu - Mawengi kwa kiwango cha zege - wafanyakzi wote kutoka nje ya nchi wanaohusika na mradi walichelewa kupata vibali nya kazi, kuanzia siku 18 hadi siku 1479.
- (c) Wataalam 26 kutoka nje ya nchi wanafanya kazi bila vibali nya kazi katika ujenzi wa barabara ya Kabingo - Kasulu - Manyovu (260.60km) kwa kiwango cha lami - wataalam kutoka nje wanaofanya kazi kwa wakandarasi katika kipande cha 2 na 3, na mkandarasi na mshauri mwelekezi katika kipande cha 4 hawakuwa na vibali nya kazi.
- (d) Wafanyakazi 27 kutoka nje ya nchi walioajiriwa na mkandarasi na mhandisi mshauri katika kipande cha 2, 3 na 4 hawakuwa na vibali nya makazi katika ujenzi wa barabara ya Kabingo - Kasulu - Manyovu (km 260.60) kwa kiwango cha lami.

Maeleo ya wafanyakazi kutoka nje ya nchi kuhusu vibali nya kazi na vibali nya makazi kwa gharama husika kwa kipande cha 2,3, na 4 katika ujenzi wa Barabara ya Kabingo - Kasulu - Manyovu (kilomita 260.60) kwa kiwango cha lami yamewasilishwa katika **Jedwali Na. 47.**

#### **Jedwali Na. 47: Hali ya umiliki wa vibali nya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni**

Kipengele/taarifa inayohitajika	Namba ya sehemu ya barabara			Jumla
	2	3	4	
Idadi ya wafanyakazi wa kigeni	21	16	26	63
Idadi ya wafanyakazi wa kigeni wasiokuwa na vibali nya kazi	12	10	4	26
Idadi ya wafanyakazi wa kigeni wasiokuwa na vibali nya ukaazi	13	10	4	27
Gharama ya kibali cha kazi (Dola za kimarekani 1000 kwa kibali)	12,000	10,000	4,000	26,000
Gharama ya kibali cha ukaazi (Dola za Kimarekani 2,650 kwa kibali)	34,450	26,500	10,600	71,550

Kipengele/taarifa inayohitajika	Namba ya sehemu ya barabara			Jumla
	2	3	4	
Jumla ya Gharama za vibali (Dola za Kimarekani)	46,450	36,500	14,600	97,550
Jumla ya Gharama za vibali (Sh.)	110,597,450	86,906,500	34,762,600	232,266,550

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Majalada ya Uhamiaji, 2023

Masuala haya yalisababishwa na uwezeshaji duni wa vyombo vyatatu na utawala juu ya upatikanaji wa nyaraka za kisheria kabla ya kuanza kwa miradi, na udhibiti usiofaa katika usimamizi wa miradi ili kuhakikisha wafanyakazi wote wa kigeni wana vibali vyatatu na kuishi.

Kushindwa kwa wafanyakazi wa kigeni kumiliki vibali vyatatu na ukaazi kunaashiria kuwa wanaishi nchini kinyume cha sheria na taratibu za nchi na hivyo kusababisha upotetu wa mapato yatokanayo na makusanyo ya ada za vibali vyatatu na ukaazi kiasi cha Sh. 232,266,550 (Sh. 61,906,000 kutokana na vibali vyatatu na Sh. 170,360,550 kutokana na vibali vyatatu makazi) kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 62.**

Ninapendekeza kwamba TANROADS ishirikiane na ofisi za serikali zinazohusika ili kuhakikisha kwamba jitihada za kutosha za utekelezaji zinafanya ili kuwezesha raia kutoka nje kupata vibali vyatatu na kuishi nchini kwa wakati.

#### 11.3.5 Wafanyakazi wa kigeni kutosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi katika ujenzi wa barabara ya Itoni - Lusitu kipande cha 1 cha mradi wa barabara: Kwa kiwango cha zege

Nilibaini kuwa wafanyakazi tisa waliokuwa wanafanya kazi ya Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Itoni - Lusitu kipande cha 1 hawakusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), kama inavyotakiwa na Kifungu cha 14 (2) cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi, 1997. Hii ilitokana na kutopatanisha na kuunganisha miongozo ya utekelezaji wa mradi na mahitaji ya kisheria ya kitaifa.

Kukosekana kwa usajili kulisababisha upotetu wa mapato, kwani kila raia kutoka nje alitakiwa kulipia ada za maombi ya usajili, ada za

usajili, leseni za kufanya kazi za uhandisi, muhuri, na ada za usajili za mwaka, jumla ya dola za Kimarekani 1,405 au Sh. 3,231,500 kwa kila mhandisi wa kigeni. Maelezo ya gharama yanawasilishwa katika **Jedwali Na. 48.**

#### **Jedwali Na. 48: Mchanganuo wa ada za wahandisi**

Kipengele/taarifa inayohitajika	Gharama (Dola za Kimarekani)	Idadi ya Wafanyakazi wa kigeni	Kiasi (Dola za Kimarekani)	Kiasi (Sh)- Sh. 2,300/Dola za kimarekani
Ada ya Maombi ya Usajili	300	9	2,700	6,210,000
Ada ya Usajili	500	9	4,500	10,350,000
Leseni ya kufanya kazi za uhandisi	30	9	270	621,000
Ada ya Muhuri	75	9	675	1,552,500
Ada ya mwaka	500	9	4,500	10,350,000
<b>Jumla</b>			<b>12,645</b>	<b>29,083,500</b>

**Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi kutokana na Taarifa Zilizokusanywa, 2023

Kwa wafanyakazi tisa wa kigeni wasiosajiliwa, ilisababisha hasara ya jumla ya Sh. 29,083,500. Zaidi ya hayo,

Pamoja na wahamiaji tisa waliotoka nje kusajiliwa, hii ilifikia hasara ya jumla ya Sh. 29,083,500. Zaidi ya hayo, kukosekana kwa usajili wa bodi ya kitaaluma kunaleta hatari kwamba wafanyakazi muhimu wanaweza kukosa sifa za kitaaluma zinazofaa ili kutekeleza majukumu yao kikamilifu katika mradi.

**TANROADS** inapaswa kushirikiana na **Wizara ya Fedha na Mipango na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB)** ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote walitoka nje ya nchi wanjasajiliwa.

## **11.4 Usimamizi wa fedha na matokeo mengine ya ukaguzi**

### **11.4.1 Malipo ya ziada ambayo hayajarejeshwa ya Sh. milioni 233.39 kwa kiasi cha kujaza mawe yatokanayo na miamba katika kuboresha barabara ya Mvugwe - Makutano ya Nduta, kipande cha 3**

Kifungu kidogo cha 14.6.4 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinamruhusu Mhandisi Mshauri kufanya masahihisho au marekebisho yoyote kwenye hati za malipo zilizopita. Hata hivyo, hati ya malipo haionyeshi kukubaliwa au kuidhinishwa na Mhandisi Mashauri.

Mapitio ya mkataba Na. TRD/HQ/1035/2019/20 wa Uboreshaji wa mradi wa barabara ya makutano ya Mvugwe-Nduta kipande cha 3 yalibaini kuwa mita za ujazo 8,903.965 kwa kifungu 36.02 (d) kwenye kujaza kwa kutumia mawe yatokanayo na miamba yanayogharimu Sh. 413,301,043 zililipwa kimakosa kupitia hati ya malipo ya 3 hadi ya 9. Hii ilipelekea malipo ya ziada ya Sh. 233,394,624.48.

Wakati TANROADS wamerejesha Sh. 179,906,417.46 ya malipo ya ziada, salio lililobaki la Sh. 233,394,624.48 halijarejeshwa kutokana na kutosimamiwa ipasavyo na Mhandisi Mshauri. Kushindwa kurejesha salio lililobaki kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za serikali.

Napendekeza kuwa TANROADS imuelekeze mhandisi mshauri kurejesha salio lililobaki Sh. 233,394,624 katika malipo yanayofuata.

### **11.4.2 Kuongezeka kwa gharama ya Sh. milioni 517.84 kutokana na riba iliyotozwa kwa kucheleweshwa kwa malipo ya mkataba wa kuboresha barabara ya Kabingo - Kasulu - Manyovu kwa kiwango cha lami**

Kifungu kidogo cha 14.7(b) cha masharti ya jumla ya mkataba kinamtaka mwajiri kulipa kiasi kilichoidhinishwa katika kila cheti cha malipo ya kati ndani ya siku 56, tofauti yoyote irekebishwe katika malipo yanayofuata kwa mkandarasi. Kifungu kidogo cha 14.8.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kinasema kwamba wakandarasi

watakuwa na haki ya kupokea riba itakayo ongezeka kila mwezi kwa kiasi ambacho hakijalipwa wakati wa kuchelewa ikiwa hawatapokea malipo kwa mujibu wa kifungu cha 14.7 cha masharti ya jumla ya mkataba.

Hati za malipo ya muda kwa kipande cha 1, 2, na 3 zilichelewa kulipwa na ilipelekeea tozo ya riba kutokana na ucheleweshaji huo, na kusababisha jumla ya Sh. 517,837,562.94 kulipwa kutokana na kuchelewesha malipo kwa wakandarasi. Maeleo yanawasilishwa katika **Jedwali Na. 49**.

#### **Jedwali Na. 49: Riba iliyolipwa kwenye malipo yaliyocheleleweshwa kwa mkandarasi**

Hati ya Malipo Na.	Kiasi cha Riba (Sh.)- Kipande cha 1	Kiasi cha Riba (Sh.)- Kipande cha 2	Kiasi cha Riba (Sh.)- Kipande cha 3
1	0	0	0
2	161,117,998	57,785,939	110,178,996
3	0	0	0
4	0	0	4,422,698
5	0	0	0
6	0	4,780,143	0
7	0	5,734,975	9,167,029
8	0	2,613,401	7,067,155
9	0	10,374,265	7,815,962
10	0	1,267,181	8,058,804
11	0	2,152,349	38,761,642
12	0	0	4,795,672
13	0	0	14,952,182
14	0	14,769,616	4,077,378
15	0	0	26,227,855
16	0	0	5,854,007
17	0	0	15,862,304
Jumla	161,117,998	99,477,873	257,241,690

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi, 2022

Ucheleweshaji wa malipo kwa mkandarasi ulisababishwa na mchakato mrefu na wenye urasimu wa uidhinishaji malipo uliohusisha TANROADS, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Mipango na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na kusababisha ongezeko la gharama na tozo zisizo za lazima. Ucheleweshaji huu wa malipo unaweza kusababisha usumbufu kwa mtiririko wa fedha wa Mkandarasi, ucheleweshaji wa mradi nakuepelekea kuongezeka kwa gharama za mradi.

Ninapendekeza kwamba TANROADS ishirikiane na AfDB, Wizara ya Fedha na Mipango, na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kushughulikia mchakato wa uidhinishaji wa muda mrefu na wenyewe urasimu ili kuhakikisha fedha zinatolewa kwa wakati.

#### 11.4.3 Ongezeko la gharama za mradi katika uboreshaji wa barabara ya Lusitu - Mawengi kipande cha 2: Barabara ya kiwango cha zege, iliyosababishwa na usanifu usioridhisha

Kifungu cha 45.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinamtaka Mwajiri amlipe Mkandarasi kiasi kilichoidhinishwa ndani ya siku 28, na Kifungu cha 54.2 kinamtaka Mwajiri kulipa Hati ya Malipo ya Mhandisi Mshauri ndani ya siku 60 baada ya kupokelewa yakiambatana na hati za kuthibitisha.

Nilibaini kuwa gharama ya mradi kwa mkandarasi na Mhandishi mwelekezi ilizidi kiwango cha mkataba kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 50** hapa chini:

**Jedwali Na. 50: Hali ya kifedha ya mradi**

Suala husika	Mkandarasi	Mshauri Elekezi
Gharama ya Mradi	159,217,440,785	5,366,717,939
Gharama za mradi zilizofanyiwa marekebisho	179,176,500,629	10,604,883,814
Tofauti	19,959,059,844	5,238,165,875
Asilimia	13	98

Chanzo: Majalada ya Mawasiliano, 2022



# SURA YA KUMI NA MBILI



**UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UDHIBITI WA UBORA WA  
MIRADI YA BARABARA INAYOENDELEA NA ILIYOKAMILIKA  
ILI KUZUIA UCHAKAVU KABLA YA MUDA WAKE**

## 12.0 Utangulizi

Ukaguzi ulilenga kubainisha sababu zinazochangia uchakavu wa mapema au dosari za barabara, kama vile uimara wa barabara usiotosheleza, kutitia kwa barabara kupita kiasi, vifaa vyta ujenzi duni kama vile udongo usiofaa, na uzito wa magari uliopitiliza na usiothibitiwa vyema. Mawanda ya ukaguzi yanajumuisha mapitio ya sheria na kanuni husika, tathmini ya usanifu (design) na ujenzi wa mradi, na tathmini ya matengenezo ya bararabara. Lengo haswa ni kuhakikisha kuwa barabara zinajengwa na kutunzwa ipasavyo pamoja na kujengwa kwa gharama nafuu na kuchangia maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii sambamba na kuokoa rasilimali fedha ambazo zingetumika kukarabati na kutunza barabara zilizoharibika mapema.

Ukaguzi huu wa kiufundi ulilenga kutathmini hatua za udhibiti wa ubora katika miradi ya barabara inayoendelea na iliyokamilika nchini ili kuzuia uchakavu na uharibifu wa barabara mapema. Ukaguzi ulihusisha miradi minane (8) ya barabara iliyotekelizwa na TANROADS kuanzia mwaka 2009 hadi 2022, kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 51** hapa chini.

### Jedwali Na. 51: Miradi iliyotekelizwa

Jina la mradi	Urefu wa Barabara katika (km)
Mradi wa barabara ya Ruangwa - Nanganga	49.3
Mradi wa barabara ya Bagamoyo - Msata	64
Mradi wa barabara ya Korogwe - Mkumbara	76
Mradi wa barabara ya Tanga - Pangani Road Project	50
Loliondo - Mto Wa Mbu; Wasso - kipande cha barabara ya mradi Sale	49
Dodoma - kipande cha barabara Fufu	70.9
Maswa - mradi wa barabara Mwigumbi	50.3
Barabara ya Nzega - Tabora; kipande cha Puge - Tabora	50.3
<b>Jumla</b>	<b>459.8</b>

**Chanzo:** Hati za mkataba kwa miradi iliyotembelewa

Nilipitia nyaraka za miradi, nikawahoji maafisa wa Wakala wa Barabara za mkitaifa nchini (TANROADS), washauri na wakandarasi, na kutathmini hali halisi ya barabara. Matokeo ya ukaguzi muhimu ni kama yafuatayo.

## 12.1 Upangaji na usanifu wa miradi

### 12.1.1 Usanifu duni wa barabara

Sura ya 8 kifungu cha 8.1 cha Mwongozo wa Usanifu wa Lami na Vifaa vya ujenzi wa 1999 inahitaji usanifu na ubunifu wa muundo wa lami uwezeshe barabara zilizojengwa ziwe zenye kuhimili mizigo ya magari yanayotumia barabara hiyo kwa muda wake uliopangwa na kutoa huduma inayokubalika bila kuharibika mapema kabla ya muda wake na kuwa isiyokuwa ya viwango thabiti na kutoa huduma chini ya kiwango.

Kati ya miradi nane ya barabara zilizokaguliwa, miradi saba ilionekana kuwa na mapungufu wa kiufundi katika usanifu, kama vile ufinyu wa mifereji ya maji na uwepo wa vizuizi vikubwa, mabadiliko ya miundo ya mifereji ya maji na makalavati kujengwa sehemu ambazo siyo sahihi, makadirio ya kiwango cha chini cha udongo korofi na namna ya kuimarisha hali ya udongo (udongo mweusi tifutifu (black cotton soil), ukadiriaji wa idadi ya magari yatakayotumia barabara hiyo uliokuwa siyo sahihi, maisha mafupi, usanifu wa miundombinu ya barabara na usanifu wa miundombinu ya barabara isiyo ridhisha kama vile barabara kukosa njia za watembea kwa miguu na barabara mchepuko za kuingia na kutoka, na ukosefu wa alama za usalama barabarani. Mapungufu yaliyobainika yalirekebishwa wakati wa ujenzi lakini mengine hayakurekebishwa kama vile matumizi ya vifaa duni vya ujenzi, ukadiriaji wa kiwango kidogo cha magari yatakayotumia barabara wakati wa usanifu na uwekaji wa matabaka duni ya lami, na hivyo kuchangia uharibifu wa barabara mapema.

Kutokana na hali hiyo, barabara sita (Barabara za Makofia - Msata; Korogwe - Mkumbara; Mwigumbi - Maswa; Nzega - Puge - Tabora, Dodoma - Fufu na Fufu - Iringa) kati ya miradi minane ya barabara zilizokaguliwa zilipata madhara makubwa na hivyo kuharibika kabla ya uhai wake, hali iliyochangia uwepo wa bajeti kubwa ya matengenezo.

TANROADS inapaswa kuchukua hatua za tahadhari katika hatua ya usanifu, kusimamia mawanda ya usanifu wa mradi kwa ufanisi, na kuimarisha uwezo wao wa usanifu/ubunifu wa ndani na usimamizi

wa mikataba. Hii itasaidia kushughulikia mapungufu ya miundo mbinu, kuhakikisha ubora wa barabara, na kuzingatia gharama za ujenzi katika maisha yote ya barabara.

#### 12.1.2 Kanuni za viwango vya kazi za barababara havijahuishwa kwa takriban miaka 22 iliyopita

Nyaraka kuu ya kudhibiti ubora wa kazi za barabara nchini ni Kanuni za Viwango vya Ujenzi wa Barabara zilizoandalishi mwaka 2000. Kanuni hizi zilianzishwa na iliyokuwa Wizara ya Ujenzi mwaka 2000.

Nilibaini kuwa, kanuni na mwongozo huo wa viwango vya barabara haujafanyiwa mapitio au kuboreshwa kwa takribani miaka 22 iliyopita ili kurekebisha dosari na kasoro na kujumuisha mabadiliko yaliyojitokeza.

Nilibaini kuwa kanuni na miongozo hiyo haikuweka vigezo vya viwango vya ubora kwa uthibiti wa muundo wa barabara, uimara na aina ya tabaka nene la (macadam) yaani lami nene, viwango vya mchanga kwa ajili ya zege, viwango na ukomo wa uwepo wa chumvi kwenye kokoto au changarawe asilia kwa tabaka la pili kutoka juu ya lami yaani (base course). Kwa kuongeza, mwongozo hauelezi hatua zinazoweza kuchukuliwa (kwa mfano, kuchelewesha uwekaji wa tabaka la mwisho la lami, miashirio ya nyufa, viashiria vya nyufa ndogo ndogo ambazo zinaweza kujitokeza na ambazo ni lazima kufanyiwa marekebisho hususani tabaka la barabara lililochanganywa udongo na saruji na mchakato wa kutokea kwa nyufa ambazo lazima zichukuliwe wakati wa ujenzi wa barabara ili kupunguza uwezekano wa kupasuka kwa tabaka zilizoimarishwa za saruji.

Ninapendekeza TANROADS, kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kuboresha viwango vya ujenzi wa Barabara (2000) kwa kurekebisha makosa ya uchapaji na kasoro/dosari nydingine na kuweka viwango sahihi zaidi vya ubora na uimara wa barabara. Zaidi ya hayo, TANROADS inashauriwa kusahihisha au kubuni vipimo vipya vya nyenzo na vifaa vya ujenzi wa barabara kulingana na utendaji kazi uliothibitishwa badala ya maelezo dhania yaliyotengenezwa kutokana na tafiti kutoka katika nchi

nyingine. Mwisho, TANROADS inapaswa kuoanisha maneno “Mhandisi” na “Meneja wa Miradi” yanayotumika katika nyaraka na kanuni na miongozo ya viwango vya ubora na masharti ya mkataba ili kuepusha mkanganyiko au mamlaka tata za usimamizi wa miradi ya barabara.

#### **12.1.3 Mwongozo wa Usanifu na ubunifu wa lami na vifaa ya mwaka 1999) haikufanyiwa marekebisho kwa takribani miaka 23**

Ili kuanisha Usanifu wa barabara nchini, Wizara ya Ujenzi ilitayarisha Mwongozo wa Usanifu wa Lami na Vifaa wa mwaka 1999 kama viwango vya marejeleo wakati wa usanifu na ubunifu wa miundo mbinu ya barabara mpya na za ukarabati zilizopo.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Mwongozo wa Usanifu wa Lami na Vifaa, wa mwaka 1999 haukuwa umehuishwa au kuhakikiwa kwa miaka 23. Mwongozo huu unaanisha usanifu wa barabara, lakini maelezo yake yamepitwa na wakati, ambapo yalichangia uwepo wa miundo duni ya barabara za lami ambayo haikudumu. Hasa, maelezo ya mwongozo wa tabaka zilizoimarishwa za saruji (C1 na C2) zilisababisha nyufa za kusinyaa (shrinkage cracks) ambazo ziliruhusu maji kuingia kwenye lami, na kusababisha uharibifu wa barabara.

Hii ni kwa sababu Mwongozo hauhitaji kutumia tabaka la kupunguza athari za mzigoto kwenye tabaka la barabara za lami kama vile vifusi visiviyofungwa au kitambaa aina ya (geotextile) kati ya msingi ulioimarishwa na safu ya juu ili kuzuia nyufa zinazoweza kutokea kabla hazijafika kwenye tabaka la juu la lami.

Napendekeza TANROADS ipitie Mwongozo wa muda mrefu wa Usanifu wa Sakafu na Vifaa (1999), na kutathmini ubora wake wa kiufundi ili kusaidia kurekebisha udhaifu ambao unawenza kusababishwa na viwango vya usanifu wa barabara za lami na kuharibika mapema kwa barabara.

## 12.2 Usimamizi wa ununuzi

### 12.2.1 Kuchelewa kumuajiri mshauri mwelekezi na Msimamizi wa miradi ya barabara

Jukumu kuu la Mshauri Msimamizi ni kusimamia miradi kwa niaba ya TANROADS, kulingana na Hadidu za Rejea za Huduma za Usimamizi. Pia ana jukumu mahususi la kupitia na kukagua muundo wa barabara uliosanifiwa na uliopendekezwa ili kuhakikisha kuwa ni sahihi katika nyanja zote na utakidhi malengo ya mradi.

Miradi mitano kati ya minane iliyokaguliwa ilikuwa na Washauri Wasimamizi walioshirikishwa baada ya mkandarasi kuanza kufanya kazi. Ucheleweshaji huo ilitokana na mpango wa manunuzi wa TANROADS usiojitosheleza. Kwa mfano, katika miradi ya barabara za Tanga hadi Pangani na Maswa hadi Mwigumbi, mhandisi mshauri alipatikana miezi mitano baada ya wakandarasi kuanza kufanya kazi.

Kuajiri mhandisi mshauri kabla ya mkandarasi kunampa muda wa kutosha mhandisi mshauri wa kupitia upya barabara iliyosanifiwa na kutambua maeneo yanayohitaji mabadiliko ili kupata barabara bora. Hii pia itamsaidia mshauri kudhibiti usimamiaji na usahili na mapitio ya utoshelevu wa rasilimali za mkandarasi, kama vile vifaa vya kupima na kubaini vyanzo (borrow pits, quarry etc) vya vifaa vya ujenzi.

**Napendekeza kuwa Menejimenti ya TANROADS ihakikishe kuwa mifumo ya ufadhili wa miradi ya barabara inaruhusu kupata washauri wasimamizi kabla ya mkataba wa kuanza kazi za mkandarasi.**

### 12.2.2 Migongano ya kimaslahi na kutopendelea kuingia katika mchakato wa kuingia mikataba na M/s TECU chini ya TANROADS

Kanuni Na.264 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inaeleza kuwa makampuni ya ushauri yanayodhibitiwa au kufadhiliwa na mamlaka za umma yanaweza kuwa na sifa ya miradi inayofadhiliwa na umma ikiwa muundo na hadhi yao ya kisheria

---

itawaruhusu kuingia katika makubaliano ya kisheria na utekelezaji wa mradi.

Nilibaini sababu za kimfumo zinazoweza kusababisha udhaifu katika usimamizi wa ubora wa mradi ya barabara ikiwa ni pamoja na ushiriki wa M/s Kitengo cha Ushauri wa Uhandisi (TECU) kama mshauri ambaye yuko chini ya TANROADS mwenye jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi ambayo TANROADS pia inasimamia mradi huo suala ambalo linakinzana. Hii iliibua migongano ya kimaslahi kuhusu uthibiti wa ubora unaojitegemea na unaofaa.

Nilibain kuwa M/s TECU haijasajiliwa na msajili wa makampuni (BRELA) kwa mujibu wa rejista ya kampuni ya BRELA. Hii ni kinyume na Sehemu ya 9 ya usajili wa makampuni ya Ushauri ya Uhandisi wa Ndani (LECF) ya Bodi ya Usajili wa Wahandisi.

Mtu aliyeingia mkataba kwa niaba ya TANROADS pia aliingia mkataba kwa niaba ya M/s TECU, na kusababisha wasiwasu kuhusu migongano ya kimaslahi. Zaidi ya hayo, hapakuwa na mikataba iliyosainiwa ya usimamizi wa mradi wa Loliondo - Mto wa Mbu (Loti 1) na mradi wa Ruangwa - Nanganga (Kipande cha 2) chini ya M/s TECU, licha ya kutolewa kwa Hadidu za Rejea na barua ya kazi iliyosainiwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa TANROADS.

Ukosefu huu wa mikataba iliyosainiwa inaweza kusababisha masuala ya kisheria na migogoro. Kutokuwa na upendeleo kati ya mwajiri na mshauri ni muhimu kwa uwajibikaji na kuzuia dosari au makosa ya mshauri.

**Ninapendekeza TANROADS isajili M/s TECU kwa msajili wa makampuni, itengeneze uwiano ulio wazi kati ya majukumu ya mwajiri na mshauri, na kuhakikisha kuwa kitengo kinachosimamiwa na serikali au kitengo cha umma kinachonunua huduma za ushauri kina uwezo wa kisheria wa kuingia na kutekeleza mikataba ya huduma za ushauri.**

## 12.3 Usimamizi wa mikataba

### 12.3.1 Usimamizi duni wa mradi na usimamizi wa mikataba unaofanywa na washauri

Masharti ya Jumla ya Mkataba wa Huduma za Usimamizi yanaainisha majukumu ya Mshauri na msimamizi wa mirdi, ambayo ni pamoja na kuajiri wafanyakazi waliohitimu elimu na wenye uzoefu, kutekeleza majukumu kwa bidii, ufanisi, na uchumi, na kufanya kazi kama mshauri mwaminifu kwa mteja ili kuhakikisha kuwa mshauri anatoa huduma za viwango vya juu vya ubora pamoja na kufanya kazi kwa maslahi bora ya mteja.

Mapitio ya mikataba ya msimamizi yalibaini kuwa TANROADS iliteua wasimamizi wa miradi kwa kuzingatia sifa za kitaaluma na uzoefu wa kazi. Hata hivyo, sharti kwamba meneja wa mradi lazima awe amemaliza mafunzo ya usimamizi wa mradi halikujumuishwa katika ombi la mapendekezo wakati wa mchakato wa ununuvi. Zaidi ya hayo, ratiba ya wafanyakazi wa huduma za usimamizi haikujumuisha Mkadiriaji majenzi, ambalo ni hitaji chini ya Sheria ya Usajili wa wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (Sheria Ndogo, 2015) kwa ajili ya kushughulikia wingi wa kazi za barabara.

Mapitio ya nyaraka za mradi yaligundua kuwa wafanyakazi wengi wakuu wanaohusika na kazi za uhandisi katika miradi ya barabara hawakuwa wahandisi wa kitaalamu waliosajiliwa, jambo ambalo ni kinyume na masharti ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi. Hii inaleta wasiwasi kuhusu sifa na uzoefu wa wataalamu hao, ambayo inaweza kusababisha kupungua kwa ubora wa kazi nzima.

Zaidi ya hayo, baadhi ya wasimamizi wa mradi waliokabidhiwa kusimamia vipengele vya kiufundi na kiutawala vya mradi hawakuweza kutekeleza majukumu yao, hivyo kuwaacha wafanyakazi wa chini kuathiri ubora wa kazi kwa manufaa ya kibinaksi. Kutokuwepo kwa wafanyakazi wakuu hupunguza nguvu kazi ya usimamizi na hutoa mianya ya utovu wa nidhamu.

TANROADS inapaswa kuwapa miradi wasimamizi wenyewe uwezo wa kiufundi, kiutaalamu na kiuongozi ili kusimamia wafanyakazi mbalimbali na kuhakikisha kuwa malengo ya mradi yanafikiwa kwa ufanisi. Zaidi ya hayo, kutekeleza utifu na viapo vya kitaalamu kwa kuhitaji kuwa miradi ya barabara itekelezwe na wahandisi wa kitaalamu waliosajiliwa ili kuboresha ubora wa kazi na kupunguza athari za ubora na hatari ya utovu wa nidhamu katika kazi na hivyo kutofanya kazi vizuri.

### 12.3.2 Usimamizi duni wa ubora

Kifungu cha 1408(c) cha Kanuni za Kiwango cha Ujenzi wa Barabara (2000) kinahitaji mkandarasi kumpatia mshauri wataalam wa kufanya ukaguzi, upimaji, na majoribio ya kazi. Kulingana na hati za mradi idadi ya wafanyakazi iliyotolewa na mkandarasi kwa mshauri wa usimamizi katika kila mradi ilianzia watano hadi 12.

Ni sharti kwa mikataba kuanzisha mfumo ya udhibiti wa ubora na kutoa wafanyakazi wenyewe uzoefu na vifaa ili kuhakikisha usimamizi mzuri na udhibiti mzuri wa kazi, ikiwa ni pamoja na uwepo wa maabara inayofaa na vifaa vya kupimia vya kutosha kwa ajili ya kupima kazi zinazotekelzeza. Hata hivyo, mifumo ya udhibiti wa ubora katika miradi minane ya barabara ilionekana kutoridhisha, huku wakandarasi wakishindwa kutoa watumishi na vifaa vya kutosha kwa ajili ya usimamizi na udhibiti wa ubora mara kwa mara. Baadhi ya vifaa nyeti vya maabara havijasahihishwa (calibrated) na TBS, na mbinu za upimaji na ufuatiliaji hazikuzingatia vipimo kikamilifu. Masuala muhimu yalibainishwa katika kila mradi, kama ilivyoordheshwa kwenye **Jedwali Na. 52** hapa chini.

#### **Jedwali Na. 52: Masuala ya sifa yaliyobainishwa katika miradi**

Mradi	Mapungufu yaliyojitekeza
Ruangwa - Nanganga Road Project (49.3 km)	<ul style="list-style-type: none"> <li>-Mhandisi wa Barabara kuu alikosa uzoefu wa usimamizi na ujuzi;</li> <li>- Mshauri hakuwa na Mpango wa Kuhakiki Ubora;</li> <li>- Mpango wa Kudhibiti Ubora wa Mkandarasi haukuwa sahihi na haukutii;</li> <li>- Vifaa vya tabaka la chini ya lami ) Crushed Rock Base (CRR) zilikuwa na maudhui ya udongo ambayo hayaruhusiwi katika nyenzo za CRR.</li> </ul>
Bagamoyo Msata (64 km)	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Kutitia kwa makalavati kwa sababu ya usimamizi duni wa ubora;</li> <li>- Matumizi ya saruji ya kiwango cha juu (42.5) kwa kuimarisha udongo wa tabaka lililoimarisha la msingi hadi C1 ilisababisha kupungua kwa kiasi kikubwa na kuanzisha nyufa kwenye safu ndogo ya msingi;</li> </ul>

Mradi	Mapungufu yaliyojitekeza
	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Udongo mpana haukushughulikiwa vya kutosha wakati wa ujenzi, na kusababisha kuinuliwa na kusinya kwa gredi ndogo ya in-situ na hivyo kupasuka kwa lami;</li> <li>- Mgawanyiko mkubwa katika tabaka la juu lami unaosababisha maji ya mvua kuingia kwenye lami;</li> <li>- Matengenezo tendaji yaliyofanywa isivyofaa na michanganyiko isiyodhibitiwa, na kusababisha kuzorota kwa Barabara haraka na hatimaye kushindwa kuhimili kishindo cha magari kutokana na athari za hali ya hewa na magari.</li> </ul>
Korogwe - Mkumbara (76 km)	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Mchanganyiko duni wa lami unoazalishwa na mkandarasi;</li> <li>- Yaliyomo ya lami kuita kiasi na uwekaji alama usio sahihi wa jumla ulisababisha ukosefu wa hewa katika mchanganyiko wa lami, na kusababisha kuvuja kwa lami na maendeleo ya mapema ya mibonyeo ) rutting kwenye lami.</li> </ul>
Tanga - Pangani (50 km)	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Mshauri wa Usimamizi hakuwa na Mpango wa Kuhakiki Ubora;</li> <li>- Mpango wa Kudhibiti Ubora wa Mkandarasi haukukamilika na haukujumuisha vipengele vyote vya kazi;</li> <li>- nyenzo za (CRR) kwa tabaka la kokoto zilikuwa zikizalishwa kutoka kwenye mawe ya matumbawe, ambayo yana tofauti kubwa ya ubora na yana mifuko ya udongo ambayo haihitajiki katika nyenzo za CRR.</li> </ul>
Loliondo - Mto Wa Mbu; Wasso - Sale (49 km)	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Meneja Mkazi wa Mradi hakuwepo wakati wote kwenye eneo la mradi, na majukumu yake yote yalikabidhiwa kwa Mhandisi wa Barabara Kuu ambaye hakuwa na uzoefu wa usimamizi na ujuzi;</li> <li>- Mkandarasi hakutayarisha Mpango wa Kudhibiti Ubora;</li> <li>- Mshauri wa Usimamizi hakuwa na Mpango wa Kuhakiki Ubora;</li> <li>- Mkandarasi aliruka mchakato wa kudhibiti ubora na kuchanganya vifaa vya tabaka la kokoto (CRR) ambavyo havijajaribiwa kwenye rundo la akiba yaani (Sockpile) ya ambayo tayari ilikuwa imejaribiwa na kuidhinishwa kwa kazi hiyo;</li> <li>- Mifereji ya pembeni iliokamilishwa vibaya, alama za barabarani na alama za usalama .</li> </ul>
Dodoma - Fufu (70.9 km)	<p>Mashimo na utitivu mwangi kwenye barabara hii umesababishwa na ukosefu wa uhusiano kati ya ya mshikamano wa lami na changarawe ya mviringo na laini ya jiwe jeupe angavu (quartzite) kwenye msingi wa tabaka lililoimarishwa yaani ( C1) pamoja na nyufa zinazoakisi ambazo zilikuwa zikiruhusu maji kuingia kwenye lami hadi chini ya tabaka la changarawe yaani (G45);</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>- Kiasi cha ongezeko la magari kwa sehemu ya barabara kati ya Fufu Escarpment na Dodoma Kusini kiliainishwa kama kiwango cha chini cha magari daraja la kwanza (yaani TLC1), ambacho hakingepaswa kutumika kwa barabara hii kuu.</li> </ul>
Maswa - Mwigumbi (50.3 km)	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Matumizi ya vifaa (material) duni (yenye viwango vya chini ya kiwango kilichoweka cha tabaka la lkokoto yaani CBR na yenye mfinyanzu wa hali ya juu sana (high Palasticity katika tabaka za kujaza na kwenye safu ya chini (G7);</li> <li>- Mfumo duni wa usimamizi wa ubora;</li> <li>- Nyenzo/vifaa na vipimo vilikuwa vikitibitishwa na kuidhinishwa na mtu mmoja au wataalamu wengine wa Mshauri wa Usimamizi ambao hawakuwa Mhandisi wa Vifaa.</li> </ul>

**Chanzo:** Uchambuzi wa wakaguzi na mapitio ya Mikataba ya miradi husika

**Ninapendekeza menejimenti ya TANROADS iongeze uwezo wake katika kusimamia wakandarasi na washauri wa usimamizi ili kuhakikisha vifaa/nyenzo na mbinu za ujenzi zinakidhi vipimo vya matakwa ya mradi. Wakati huo huo, wasimamizi wanaofutilia kazi hizo wanapaswa kuhakikisha kwamba tatizo lolote linaloweza**

kuathiri ufanisi wa utendaji linatatuliwa kwa wakati. Aidha, ni muhimu kutekeleza mpango wa matengenezo ili kuzifanya barabara ziwe bado katika hali nzuri ili kudumisha utendakazi/ ufanisi wa barabara na kuongeza muda wa matumizi ya barabara za lami.

#### 12.3.3 Mfumo usiofaa wa uhakikisho wa ubora

Kifungu cha 1408 (c) cha Kanuni za Viwango vya Ujenzi wa Barabara (2000), kinamtaka mkandarasi kumpa mtaalam mshauri idadi ya wafanyakazi wa ziada kwa ajili ya kukagua, kupima na kupima kazi.

Nilibaini kuwa idadi ya wafanyakazi wa wakandarasi aliopewa mshauri katika kila mradi ilikuwa kati ya watano hadi 12. Pia nilibaini kuwa wafanyakazi waliohusika katika udhibiti wa ubora na taratibu za uhakiki ubora wa miradi ya barabara walilipwa na mkandarasi, jambo ambalo liliuba wasiwasi kuhusu uhuru na uwezekano wa mgongano wa kimaslahi. Ingawa wafanyakazi walifanya kazi chini ya usimamizi wa mshauri, mpangilio huu ulipunguza uhuru wa mshauri katika uhakiki wa ubora na hivyo kukiwa na uwezekano wa kusababisha vitendo visivyo vya haki kwa maslahi ya mkandarasi.

Napendekeza TANROADS iongeze uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa uhakiki wa ubora wa kazi za barabara na kuchunguza matokeo yanayoweza kutokea ya mfumo wa sasa wa uhakiki wa ubora. Aidha, iruhusu msimamizi wa mradi kupewa wafanyakazi wasaidizi wa kutosha ili kutekeleza uhakiki wa ubora bila kuhusisha wafanyakazi wa mkandarasi.



**SURA YA KUMI  
NA TATU**



**UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA UJENZI  
WA RELI YA KISASA**

## **13.0 Utangulizi**

Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC), inaendelea na jitihada mbalimbali za kupanua na kuboresha miundombinu ya reli nchini. Moja ya miradi muhimu ni ujenzi wa njia mpya ya reli ya kisasa yaani “Standard Gauge Railway” (SGR), inayounganisha Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi jirani za Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. SGR ina urefu wa kilomita 1,800, upana wa milimita 1,435 na uwekaji umeme wenge msongo wa 25 Kilo Voti (KV) 50 Hezi (Hz) AC. Hii ni reli ya kwanza Afrika Mashariki na Kati ambayo imeundwa kutumia umeme kwa injini za treni na ina uwezo wa kubeba mabehewa ya kusafirisha abiria kwa kasi ya Kilomita 160 kwa saa na treni za mizigo zinazosafiri kwa kasi ya kilomita 120 kwa saa. Ujenzi wa Mtandao wa Reli ya kati kwa kiwango cha kati Tanzania unagawanywa katika vipande vitano vyenye urefu wa jumla ya kilomita 1,395.

Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (MoWT), kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC), inatekeleza ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway) kwa kuzingatia muda, gharama na ubora ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya mradi. Taasisi kuu iliyokaguliwa ni Shirika la Reli Tanzania (TRC), likiwa mtekelezaji mkuu wa mradi huo.

### **13.1 Upangaji na usanifu wa mradi**

#### **13.1.1 Kukosekana kwa Vielelezo vyta Vigezo na Viwango vyta Umeme vinavyotolewa kwa Mkandarasi kwa ajili ya kuweka bei**

Sura ya 2 ya Mwongozo wa Upangaji na Majadiliano ya Miradi ya kuongeza Mikopo, Utoaji wa Dhamana na kupokea Ruzuku, iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha na Mipango mwezi Novemba 2020 inazitaka wakala za utekelezaji wa mradi huu kuhakikisha kuwa upembuzi yakinifu na au mapendekezo ya mradi kuwa na taarifa zote muhimu ili kuwezesha uamuhi sahihi na kuonyesha picha halisi ya uwezekano wa Utekelezaji wa mradi.

Wakati wa majadiliano ya mkataba kati ya YAPI na RAHCO yaliyofanyika Januari, 2017, ilikubalika kuwa, Mkandarasi afanye

tathmini ya masuluuhisho ya Kiutaalamu au Kiufundi na gharama za usanifu na uwekaji wa Mfumo wa wa umeme wa nyaya za Juu. (Overhead Catenary System (OCS)) kwa ajili nyaya za umeme na Vituo vya kupoozea Umeme. Hata hivyo, hapakuwa na viwango na vigezo vingine vya kiufundi vilivyotolewa kwa Mkandarasi ili kuwaruhusu kunukuliwa kwa bei kulingana na mahitaji/matakwa, kama vile idadi ya treni katika kila sehemu za mifumo ya umeme wa treni wa juu (Overhead Catenary System), matumizi yake na nguvu hayakujulikana.

Kwa hivyo mkandarasi aliwasilisha pendekezo kwa kuzingatia mawazo kwamba treni itakuwa na injini (Vichwa vya treni) zisizozidi mbili na matumizi ya sasa katika kila sehemu ya kabati ni takribani 800A. Ukosefu wa uamuzi wa viwango na vielelezo vya reli ya umeme ulikuwa na hatari ya upangaji wa bei ya gharama zisizo halisi za manunuzi na kusambazaji umeme na utoaji wa Vigezo na viwango visivyofaa.

### **13.1.2 Makadirio ya gharama ya mradi kwa ajili ya kusambaza umeme hayakuzingatia miundo na tafiti za awali**

Kanuni ya 69(3) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma GN. 446 ya mwaka 2013 inaitaka Taasisi Nunuzi kuainisha mahitaji yake ya bidhaa, huduma na kufanya kazi kwa usahihi inavyowezekana kwa kurejelea huduma au shughuli ambazo tayari zimeratibiwa katika mpango kazi wa mwaka na kujumuishwa katika makadirio ya mwaka.

Nilibaini kuwa makadirio ya gharama ya mfumo wa umeme wa reli hayakuandaliwa. Mkandarasi alitakiwa kuwasilisha mapendekezo ya mfumo wa kusambaza umeme. Hii ni kinyume na mbinu bora za kuomba nukuu za be kutoka kwa Mkandarasi. Hata hivyo pendekezo lililowasilishwa halikutathminiwa dhidi ya makadirio ya Mhandisi Mshauri.

Menejimenti ya TRC ilinifahamisha kuwa usanifu na tafiti za awali za uwekaji umeme zilifanywa na CPCs kwa kumbukumbu 13359-04. Walakini, iligundulika kuwa Tafiti ya CPCs yenye kumbukumbu 13359-04 ilikamilika mnamo Machi 13, 2019, wakati Mkataba wa kipande cha kwanza (Lot 1) ulitiwa saini mnamo Februari 2017.

## 13.2 Usimamizi wa Ununuzi

### 13.2.1 Masharti ya mkopo kutoka Benki kwenda kwa Serikali kwa mradi kipande cha 3 na 4 yalipunguza njia ya ushindani ya ununuzi wa zabuni

Kifungu cha 64 (1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya 149 (1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma GN. 446 ya mwaka 2013 inataka njia za ushindani wa zabuni upewe kipaumbele kwa sababu ya uwezo wake wa kupata bei za ushindani kutoka kwa wazabuni mbalimbali, hivyo kuruhusu serikali kupata thamani ya fedha.

Mapitio yangu ya njia za ununuzi zilizotumika katika ununuzi wa mkandarasi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha 3 na 4 yalibainisha kuwa Benki ya *Standard Chartered* ambako Serikali ilipata mkopo iliweka masharti kwamba ingekubali jukumu la kuwa Mratibu wa Kimataifa, na Wakala Kiongozi Aliye na Mamlaka kupanga ufadhilli na mkopo kwa Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) tu kwa masharti kwamba kampuni ya Yapi Markezi iteuliwe kama Mkandarasi. Wizara ya Fedha na Mipango (MOFP) ilikubali mkopo huo kwa masharti yasiyofaa kutoka Benki ya Standard Chartered kuitia barua yenye kumbukumbu namba PST/GEN/2021/01/55. Nilibainisha zaidi kwamba TRC iliamua kuchagua njia ya kutoa zabuni kwa njia mzabuni mmoja licha ya ushauri uliotolewa na PPRA na Bodi ya Zabuni, ambayo iliishia kuigharimu serikali fedha zaidi. Gharama hii ya ziada ingweza kuepukwa.

Ni maoni yangu kwamba, hakuna mfadhili anayeweza kuitaka Serikali ya Tanzania kumpa mkataba mkandarasi pasipo kuwa na uwazi, ushindani, usawa na haki kwa wakandarasi wote wenye sifa na wanaostahili katika mchakato wa ununuzi.

### **13.2.2 Gharama za Ujenzi wa SGR kipande cha 3 na 4 ziliongezeka kwa Dola za Kimarekani Milioni 1.3 na 1.6 kwa kilomita moja mtawalia ikilinganishwa na Mikataba Iliyofanyika njia ya Ushindani ya ununuzi**

Mapitio yangu ya nyaraka za Mikataba zilizotolewa kwa kipande cha 1, 2 na 5 yalibaini kuwa gharama za ujenzi wa SGR kwa Kilomita (km), ambapo njia ya ushindani iliyotumika kwa kilomita ilikuwa dola za Kimarekani milioni 4.1, milioni 4.6 na milioni 3.9 mtawalia, wakati kwa kipande cha 3 na 4 mchakato wa zabuni ulifanyika kwa njia ya mzabuni mmoja (Single source), gharama ya ujenzi wa SGR kwa kilomita moja ilikuwa dola 5.2 na dola milioni 5.5 mtawalia.

Kulingana na tofauti hiyo, hapakuwa na faida ya kiuchumi kwa TRC kwa kutoa kandarsi kuititia njia ya chanzo kimoja kwa M/S Yapi Merkezi. Hii ni kwa sababu gharama awali za miradi mingine zilikuwa chini ikilinganishwa na mkataba aliopewa mkandarsi wa kipande cha 3 na 4. Zaidi ya hayo, niligundua kuwa mawanda ya kazi kwa kipande cha 3 na 4 ya mradi ulikuwa mdogo na ulikuwa na miundombinu michache kuliko ile ya kipande cha 1, 2, na 5, na miundo mikuu zaidi.

**Ninapendekeza menejimenti ya TRC kuweka kipaumbele katika matumizi ya mbinu shindani ya ununuzi katika shughuli za manunuzi za siku zijazo ili kuepuwa upotevu wa fedha za walipa kodi.**

### **13.2.3 Gharama ya Ununuzi wa treni (vichwa vya treni, treni za kisasa za umeme na mabehewa ya abiria) Iliongezeka kwa Dola za Kimarekani 215,046,954 baada ya kukataliwa kwa zabuni zote bila sababu ya msingi**

TRC ilialika wazabuni 11 walioteuliwa na kushindanishwa kimataifa na zabuni za Ugavi, Uagizaji, majoribio mafunzo na kukabidhi vichwa vya treni, Mabehewa ya abiria na treni za kisasa za umeme (yaani Rolling Stocks) kwa Ukanda wa Reli ya Standard Gauge (SGR) kipande cha kwanza 1 hadi 4, lakini wazabuni wote walikataliwa kwa sababu ya kutofikia matakwa ya zabuni na bei ya juu iliyonukuliwa kuliko bajeti iliyopo.

Aidha, zabuni ilitangazwa tena na kampuni ya M/S. RRC International Corporation Ltd ilipendekezwa kuleta (vichwa /ingini za treni ya Umeme, treni za abiria za kisasa, mabehewa ya abiria na ya Mizigo) kwa Dola za kimarekani 263,460,514. Hata hivyo, zabuni hii pia ilikataliwa kutokana na kukosekana kwa dhamana kuu ambayo haikuwa mionganoni mwa vigezo katika andiko la zabuni.

Wazabuni waliofanyiwa tathmini ya chini kabisa wakati wa awamu ya kwanza na ya pili ya mchakato wa ununuzi wa treni za abiria za kisasa (EMU), injini za treni na mabehewa ya abiria hawakualikwa. Katika awamu ya pili ya mchakato wa manunuizi, kampuni ya M/S Sung Shin Rolling Stock Technology Ltd, ambayo ilikuwa mzabuni wa pili kwa tathmini ya chini kwa bei ya Dola za Kimarekani 50,569,316.00 ikiwa ni kwa ajili ya usambazaji wa mabehewa 60 ya abiria, ilialikwa, huku M/S. CRRC-International Corporation, ambaye alikuwa mzabuni wa chini kabisa aliyetathminiwa kwa bei ya Dola za Kimarekani 39,223,500.00 hakualikwa. Pia kwa bei ya treni za kisasa za abiria yaani (Electric Multiple Unit) ilipanda kwa 56% kutoka Dola za Kimarekani 12,179,784.80 hadi Dola za Kimarekani 19,012,000.

Pia nilibaini kuwa baada ya kufutwa kwa zabuni katika awamu ya pili, TRC ilitumia njia isiyo ya ushindani ya ununuzi wa kwa awamu zote za mradi, isipokuwa ununuzi wa mabehewa ya mizigo baada ya kushindwa kupata mzabuni aliyeaulu wa mabehewa hayo katika awamu ya tatu na ya nne pamoja na awamu ya sita. Matokeo yake, baada ya kukataliwa mara ya pili kwa zabuni zote gharama ya ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo na mabehewa ya abiria yaani (Rolling Stocks) ikawa ni sawa na Dola za Kimarekani 478,507,468.00 ambayo ni zaidi ya gharama ya kushinda zabuni kwa mara ya kwanza ambayo ilikuwa ni Dola za Kimarekani 263,460,514.00 ambayo ilisababisha ongezeko la Dola za Kimarekani 215,046,954.00 sawa na asilimia 82.

#### **13.2.4 Kutozingatiwa kwa mapungufu yaliyobainika wakati wa uchunguzi wa ununuzi wa wazabuni**

TRC ilimuomba Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uturuki kufanya uchunguzi wa kina kwa mzabuni M/S. Eurowagon juu ya ununuzi wa Treni za Umeme zilizotumika / zilizokarabati mbili na

mabehewa 30 ya Abiria kwa Majaribio na Uagizaji kwa ajili ya reli ya kisasa ili kuthibitisha hali ya kisheria na uwepo wa kampuni, uwezo wa kitaalamu na kiufundi, uwezo wa rasilimali na uthibitishaji wa wateja wanaohudumiwa au waliowahi kufanya kazi na kampuni hiyo. Balozi alibaini kuwa, kampuni haitekelezi mradi wowote kwa sasa isipokuwa mradi pekee uliokamilishwa na Eurowagon ulikuwa wa 2019 ambapo kampuni hiyo iliuza kontena 53 aina ya RGS.Aidha, uwezo wa kifedha wa kampuni ulibainika kutotosha kutekeleza mradi wa uingizaji wa mabehewa yaliyotumika nchini isipokuwa walipata ufadhili kutoka kwa vyanzo vingine. Licha ya hilo, TRC iliidhinisha zabuni hii kutolewa kwa M/s Eurowagon.

Hata hivyo, kampuni ya M/s Eurowagon ilitekeleza Mkataba pasipokuwa na dhamana ya utendakazi (performance security) na haikuwasilisha vichwa viwlili nya treni (Locomotives) na mabehewa ya abiria 30 venye thamani ya Euro 26,602,200 ndani ya muda uliokubaliwa na kwa mujibu wa *mkataba* (miezi tisa).Pia nilibaini kuwa TRC ililipa kampuni ya M/s Eurowagon Kiasi cha Euro 9,310,700 (sawa na 35%) ya jumla ya gharama za mkataba wa kazi baada ya ukaguzi wa awali wa ununuzi na uthibitisho wa uhamishaji wa umiliki.

Ninapendekeza TRC kuzingatia ushauri wa masuala yanayohusiana na uchunguzi wa kina kutoka kwa vyombo vingine nya serikali na kuchukua hatua zote zinazohitajika ili kupunguza mapungufu ya wazabuni ambao hawana uwezo wa kufanya kazi kama inavyotarajiwa.

### **13.2.5 Bei ya Mabehewa 30 ya Abiria yaliyotumika iliongezeka kwa Euro milioni 4.53 (sawa na Sh. Bilioni 11.59) baada ya Ofa ya pili**

Tarehe 7 Februari 2020, kampuni ya M/S Eurowagon iliwasilisha ofa ya bei na maelezo ya mabehewa ya abiria kwa TRC ikionyesha kuwa bei kwa kila behewa moja la abiria ilikuwa Euro 655,000.Tathmini ilifanyika na kupendekeza kampuni ya M/s Eurowagon kupewa zabuni yenye thamani ya Euro 19,650,000.Hata hivyo mnamo tarehe 8 Juni, 2020 kampuni ya M/S Eurowagon iliwasilisha ofa iliyofanyiwa marekebisho iliyokuwa na gharama za juu zaidi ya bei kwa kila behewa moja la abiria kufikia Euro 840,000 hivyo kupelekea

ongezeko la Euro 151,000 kwa bei ya behewa moja ikilinganishwa na bei ya mara ya kwanza ya Euro 655,000.

TRC ilibaini kuwa mawanda ya ofa ya kwanza yalitofautiana na ile ya ofa ya pili. Walakini, mapitio yangu ya hizo ofa nilibaini kuwa mawanda ya kazi yalikuwa sawia. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa katika ofa ya kwanza iliyowasilishwa kwa TRC, mzabuni pia alijumuisha masharti ya kununua na kuleta vipuri vitakavyotumika kwa miaka miwili. Hivyo, TRC iliingia gharama ya ziada ya Euro 4,530,000, sawa na Shilingi bilioni 11.59.

**Ninapendekeza menejimenti ya TRC kuhakikisha hatua zinazofaa zinachukuliwa ili kuhakikisha kuna udhibiti madhubuti wa gharama wakati wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi wa mitambo mikuu ya reli.**

### **13.3 Usimamizi wa Mkataba**

#### **13.3.1 Viwango vyatubora wa treni zilizotumika na mabehewa ya abiria havikuzingatiwa**

Mnamo tarehe 18 Oktoba 2020, mkataba ulitiwa saini kati ya TRC na M/S Eurowagon kwa ajili ya usambazaji wa vichwa viwili (2) yaani (Locomotives) na Mabehewa ya abiria thelathini (30) kwa Euro 26,602,200. Hata hivyo nilibaini TRC haikupata historia kamili ya vitu hivyo, ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za utaratibu na matengenezo makubwa yaliyofanywa kwa mitambo au mashine na stakabadhi/vyeti stahiki ambazo zingeweza kutoa picha kamili na hali halisi ya vichwa vyatreni na mabehewa ya abiria.

Maafisa wa TRC walifahamisha kuwa treni zilizotumika na mabehewa ya abiria yangefanyiwa ukarabati kabla ya kuwasilishwa. Hata hivyo, nilibaini kuwa, Sheria ya Manunuzi haitoi nafasi kwa Taasisi Nunuzi kununua mitambo iliyofanyiwa ukarabati bali ni mitambo iliyotumika.

Pia, nilibaini kuwa TRC ililipa kampuni ya M/s Eurowagon Euro 9,310,700 (sawa na 35% ya jumla ya mkataba) bila kupata historia ya

matengenezo ya mara kwa mara na makubwa yaliyokwishafanywa kwa treni zilizonunuliwa na mabehewa ya abiria.

**Ninapendekeza menejimenti ya TRC kupata historia kamili ya vifaa vikuu vilivyonunuliwa, ikijumuisha matengenezo ya mara kwa mara na matengenezo makubwa yaliyokishafanywa kwa mitambo au mashine na stakabadhi ya ubora.**

### **13.3.2 Hasara ya Euro 5,320,400 (Sh. 13,609,583,200) kutokana na Utekelezaji wa Mkataba bila dhamana ya Utendaji na kuto kata fidia ya ucheleweshaji (Liquidated Damage) iliyowekwa**

Kanuni ya 29(1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma GN. 446 ya mwaka 2013 inamtaka mzabuni aliyeshinda zabuni kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi ili kuhakikisha utendakazi na uadilifu kwa mkataba na malipo ya vibarua wote, wasambazaji, makanika na wakandarasi wadogo, kama wapo.

TRC ilitia saini mkataba na kampuni ya M/S Eurowagon tarehe 18, Oktoba, 2020, kwa kuagiza na kuleta vichwa viwili nya treni (locomotives) na mabehewa 30 ya abiria. Kampuni ya M/s Eurowagon haikuwasilisha dhamana ya utendajikazi (Performance Security) licha ya kukumbushwa mara kadhaa na TRC. TRC iliendelea kutekeleza Mkataba huu pasipo kupatiwa dhamana ya utendajikazi jambo ambalo lilipelekea kusitishwa kwa Mkataba pasipo kukata dhamana kama fidia kwa kutotimiza wajibu wa kazi.

Zaidi ya hayo, kifungu kidogo cha 8.7 cha mkataba kati ya TRC na M/S Eurowagon kinaitaka kutoza 0.15% ya thamani ya mkataba kwa siku kama fidia ya bidhaa ambazo hazijawasilishwa, hadi kiwango cha juu cha 10% ya thamani ya mkataba. TRC haikutoza Euro 2,660,200 kwa ucheleweshaji wa kuwasilisha bidhaa hivyo kuleta hasara ya mapato yenye thamani ya Euro 2,660,200 ambayo ingekatwa kama fidia ya dhamana ya utendajikazi na kupelekea Jumla ya hasara ya Euro 5,320,400.

Zaidi ya hayo, sikupata ushahidi wowote kwamba TRC ilimweleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu kusitishwa kwa mkataba kama

inavyotakiwa na Kanuni ya 113(1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma GN. 446 ya mwaka 2013.

Ninapendekeza menejimenti ya TRC kuhakikisha wazabuni wanawasilisha dhamana ya utendakazi kabla ya utekelezaji wa mkataba ili kuepuka hasara isiyo ya lazima. Pia kukata fidia ya uchelewshaji wa bidhaa au kazi kwa wakati unaofaa endapo kutakuwa na ucheleweshaji.

### 13.3.3 Matumizi Zaidi ya Dola za Kimarekani 11,189,281.50 kutoka Kiasi cha Dharura kwa kipande cha 1

Kifungu cha 4 cha mkataba kati ya TRC na M/S Yapi Merkezi A.S katika ubia JV na M/S Mota kinaonesha kuwa, bei ya mkataba ilikuwa Dola za Kimarekani 1,215,282,000 ikijumuisha VAT. Bei ya mkataba ilijumuisha Dola za Kimarekani 140,000,000 ambapo Dola za Kimarekani 60,000,000 zilikuwa ni fedha ya nyongeza ya kazi za ziada (provision); na Dola za Kimarekani 80,000,000 zilikuwa kiasi cha dharura. Mpango wa malipo ulionyesha kuwa kiasi hicho cha ongezeko la kazi kilitakiwa kutumika kwa kazi za ziada, kuhamisha miundombinu, fidia ya ardhi, bima, vibali, ripoti ya mazingira, washauri wa miamala na mafunzo.

Mapitio yangu ya Ripoti ya Maendeleo ya Kila Mwezi ya Mshauri wa mradi ya Septemba 2022 ilionesha kuwa takribani Dola za Kimarekani 151,189,281.50 zilitarajiwा kutumika kutohuna na fedha za ongezeko la kazi na dharura. Kwa kuwa, Dola za Kimarekani 129,861,627 zilikuwa tayari zimeidhinishwa na pande zote na Dola za Kimarekani 14,139,553.06 zilikuwa bado hazijaidhinishwa na TRC huku Dola za Kimarekani 7,188,101.29 zikiwa katika uhakiki wa Mshauri wa mradi. Ikiwa kiasi chote kitaidhinishwa na kulipwa, basi Dola za Kimarekani 11,189,281.50 zingekuwa zimezidi kiwango kilichopangwa hadi muda wa ukaguzi.

Ninapendekeza menejimenti ya TRC kuchukua hatua stahiki katika udhibiti na usimamizi wa matumizi ya fedha za ongezeko la kazi (provision sum) na Dharura (contingency).

### **13.3.4 Ongezeko la muda zaidi ya Siku 1441 (miaka 3.8) za Kukamilisha mradi wa SGR kipande cha 1**

Kwa mujibu wa mkataba namba PA/003/HQ/2016-17/W/01 wa Ujenzi wa Mradi wa Reli ya kisasa (Standard Gauge Lot 1) kati ya Reli Assets Holding Company Limited inayojulikana kwa sasa kama Shirika la Reli Tanzania (TRC) na YAPI-MOTA ENGIL JV, mradi huo ultakiwa kukamilika tarehe 1 Novemba 2019.

Hata hivyo, nilibaini kuwa, mradi huo uliongezwa muda wa kukamilika mara saba, na kuongeza siku 1414 hadi muda wa kukamilika, sawa na miaka 3.8. Hii ilitokana na kucheleweshwa kwa uamuzi wa uhamishaji wa miundombinu ya bandari na makabidhiano ya eneo la ujenzi (access to site), na kuchangia kwa siku 959 za kuchelewa. Kucheleweshwa kwa maamuzi kuhusu kiunganishi cha bandari cha kilomita 4, na reli ya zamani (MGR), na kucheleweshwa makabidhiano ya eneo la kazi (access to site). Ucheleweshaji huo pia ulisababishwa na kuchelewa kuanzishwa kwa njia za juu 8.1 na mapitio na marekebishesho ya mwajiri ya njia za juu kucheleweshwa 6.1, 9.1, na 11.1, ikijumuisha ucheleweshaji zaidi wa kutompa mkandarasi eneo kamili la kazi na uhamishaji wa miundo mbinu. Muda wa umalizaji kwazi uliongزوا hadi kufikia tarehe 15 Septemba 2023.

### **13.3.5 Ongezeko la ziada la gharama za mkandarasi mshauri sawa na Dola za Kimarekani 11,322,599 kutokana na Ongezeko la muda wa Mkataba wa Ujenzi**

Mkataba wa mkandarasi mshauri wa Mradi uliongezwa muda kutokana na kuongezwa kwa mkataba wa kazi za ujenzi na kusababisha ongezeko la gharama hadi Dola za Kimarekani 11,322,599 ya gharama ya Mkataba iliyoidhinishwa. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa bado kulikuwa na nyongeza tatu za Mkataba wa mkandarasi mshauri ambazo hazijaidhinishwa, hivyo ikimaanisha kwamba kuna hatari ya ongezeko la gharama za ziada kwenye mradi.

Ninapendekeza TRC kuhakikisha usimamizi wa masharti ya Mkataba juu ya muda wa Utekelezaji ili kupunguza hatari ya kupanda kwa gharama ya mkandarasi mshauri wa mradi.

### **13.3.6 Kubadilisha Mawanda ya kazi kwa kupunguza kiwango cha ugumu wa wa reli**

Mapitio yangu yalibaini kuwa, barua ya mkandarasi mshauri ya tarehe 24 Februari, 2022 ilishauri TRC kuzingatia matakwa ya mwajiri baada ya kupokea ombi kutoka kwa mkandarasi kuhusu kubadilisha ugumu wa reli kutoka Brinell yaani viwango vya ugumu wa (BH) 350 hadi BH 310.

Hata hivyo, kupitia barua ya tarehe 3 Juni, 2022, ilibainika kuwa TRC haikutoa pingamizi kwa mkandarasi kubadilisha ugumu wa reli kutumia na hivyo kutumika BH 310. Matumizi ya BH 350 kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanywa na maafisa wa TRC, yalikuwa ni kuzingatia ubora wa awali kwa kipande cha 1 hadi cha 4 zilikuwa kubwa kuliko BH310. Ni maoni yangu kwamba, matumizi ya BH 310 badala ya BH 350 yatazunguza muda wa matumizi ya huduma ya reli ambayo yatahitaji gharama ya juu ya matengenezo.

Ninapendekeza menejimenti ya TRC kuhakikisha ujenzi wa vipengele mbalimbali vya mradi vinatekelezwa baada ya kuidhinishwa na *Mwakilishi wa Mwajiri*, na endapo kutatokea kutolewana kati yao wanatakiwa kutatua migogoro kabla ya kutoa idhini hiyo.

### **13.4 Usimamizi wa Fedha**

#### **13.4.1 Kutolipwa Sh. Bilioni 1.72 kutokana na ukosefu wa vibali vya kazi kwa Watumishi 740 wasio Raia**

Kanuni ya 3 ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Raia (Kanuni ya Ajira) ya mwaka 2015, inataka ada za kibali cha kufanya kazi ziamuliwe kwa kuzingatia daraja la kibali cha kufanya kazi kilichoombwa. Daraja la kazi la mradi wa SGR lilikuwa C na ada ilikuwa Dola za Kimarekani 1000 kwa kipindi cha miaka miwili.

Mapitio yangu yalibaini kuwa vibali vya kufanya kazi kwa wafanyakazi 740 wa kipande 1,2 na 3 katika mradi was SGR amba ni raia wa kigeni vilikuwa vimeisha muda wa matumizi. Hii

ilimaanisha kuwa hawakulipa ada ya kuhuisha vibali vya kufanya kazi vyenye thamani ya Dola za Kimarekani 740,000 sawa na Shilingi 1,725,680,000.

**TRC inashauriwa kuchukua hatua za kukusanya ada za vibali vya kufanya kazi vilivyokwisha muda ili kuepuka athari za kisheria na kifedha.**





## SURA YA KUMI NA NNE



**UKAGUZI WA KIUFUNDI KUHUSU GHARAMA KATIKA  
UJENZI WA MAJENGU YANAYOMILIKIWA NA SERIKALI**

## 14.0 Utangulizi

Ujenzi wa majengo ya Serikali ni uwekezaji muhimu kwa taasisi za serikali ili kuwezesha kukusanya mapato na hatimaye kutoa gawio kwa Serikali. Aidha, ujenzi wa majengo ya Serikali unahakikishia Wizara, Idara na Wakala za Serikali kuwa na majengo yeny nafasi za kutosha, vitendea kazi na mazingira mazuri ya kufanya kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Zaidi ya hayo, majengo ya Serikali yanawawezesha watumishi wa umma na watumishi wa Sekta binafsi kupata makazi yanayofaa.

Ukaguzi huu ulilenga kufanya tathmini ili kubaini kama Serikali ilisimamia vizuri gharama za ujenzi wa majengo ya Serikali, ambayo ni uwekezaji muhimu wa kuwezesha kukusanya mapato na kutoa ofisi na makazi sahihi kwa watumishi wa umma.

Ukaguzi ulifanyika kwenye miradi tisa ya ujenzi iliyotekelawa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Shirika la Nyumba la Taifa (NHIF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Taifa (NSSF), Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) katika kipindi cha miaka sita ya fedha kutoka mwaka 2016/17 hadi 2021/22 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 53**.

**Jedwali Na. 53: Taasisi na miradi iliyokaguliwa**

Na.	Mradi uliokaguliwa	Mahali ulipo	Taasisi iliyokaguliwa
1	Ujenzi wa Nyumba za Magomeni	Dar es Salaam	TBA
2	Ujenzi wa Maghorofa ya Mzizima	Dar es Salaam	NSSF
3	Ujenzi wa Hoteli ya Kitalii Mwanza-NSSF	Mwanza	NSSF
4	Ujenzi wa Jengo la Biashara la Sam Nujoma	Dar es Salaam	PPF
5	Ujenzi wa Jengo la Biashara la PSPF	Dodoma	PSSSF
6	Mradi wa Ujenzi wa nyumba za Makazi Kawe 711	Dar es Salaam	NHC
7	Ujenzi wa Nyumba za makazi Viktoria	Dar es Salaam	NHC
8	Ujenzi wa Magorofa ya matumizi mchanganyiko ya Morocco	Dar es Salaam	NHC
9	Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya DAWASA Yetu	Dar es Salaam	DAWASA

**Chanzo:** Nyaraka za mikataba 2016/17-2021/22

## 14.1 Upangaji na usanifu wa miradi

### 14.1.1 Upembuzi yakinifu usiojitosheleza kabla ya kuanza ujenzi wa miradi

Mwongozo Na. 4.1 wa Mwongozo wa Uendeshaji wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma, 2015 unataka upembuzi yakinifu wa awali kwa miradi mikubwa ili kutathmini uhitaji wa mradi, maswala ya kiufundi, uhandisi, athari kwa mazingira na kwa jamii, uwepo wa rasilimali watu na nyanja za kiuchumi.

Ukaguzi ulibaini mapungufu katika upembuzi yakinifu kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 54** hapa chini.

#### Jedwali Na. 54: Miradi yenyе upembuzi yakinifu usiojitoesheleza

Mapungufu	Jina la Mradi
Upembuzi yakinifu haukufanyika	Mradi wa ujenzi wa nyumba za Magomeni; Usanifu na ujenzi wa Jengo la Ofisi za DAWASA
Upembuzi yakinifu ulifanyika ulipita muda wake	Ujenzi wa Hoteli ya Kitaiti Mwanza-NSSF (Upembuzi yakinifu ulifanyika Machi, 2007 wakati ujenzi ulianza Novemba, 2013)
Upembuzi yakinifu usiojitoesheleza	Jengo la Kibiashara la PPF (PSSSF) na Ofisi ya Makao Makuu ya PSSSF (Jumla ya gharama ya ujenzi iliyotumiwa katika ripoti ya upembuzi yakinifu ilikuwa Sh. 246,216,858,745 ambayo ni zaidi kwa asilimia 5.95 ikilinganishwa na bei ya juu kabisa ya mkandarasi ya Sh. 232,389,459,867; Jengo la Kibiashara la Ghorofa nyingi la PSPF (ripoti ya upembuzi yakinifu haijataja kipindi/mwaka ambapo upembuzi ulifanyika).
Miradi ilianza kabla ya kufanyika/kukamilika kwa upembuzi yakinifu	Mradi wa Ujenzi wa nyumba za Makazi Kawe 711 (upembuzi yakinifu ulikamilika miezi nane baada ya kazi za ujenzi kuanza); Ujenzi wa Nyumba za makazi Viktoria (upembuzi yakinifu ulifanyika mwezi Machi 2015, mkataba ulisainiwa mwezi Disemba, 2013 utekelezaji wa mradi ulianza January, 2014)

Ni busara kwa uongozi wa miradi ya ujenzi kuhakikisha kwamba upembuzi yakinifu unafanya kabla ya kuanza kwa mradi wowote. Upembuzi yakinifu unapaswa kuuishwa mara kwa mara ili kuzingatia mabadiliko yoyote katika vigezo viliviyotumiwa wakati wa upembuzi yakinifu ili kuhakikisha kuwa mradi unabaki kuwa endelevu. Hii itasaidia kupunguza hathari katika miradi na kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa mafanikio.

#### **14.1.2 Miradi ya ujenzi ambayo haikuwa imepangiwa bajeti Sh. 150.51 bilioni**

Kanuni 75 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inahitaji taasisi nunuzi kutenga fedha kabla ya kuanza michakato ya ununuizi.

Nilibaini miradi minne kati ya tisa iliyokaguliwa yenyewe kiasi cha Sh. 150,508,922,458.05 ambacho hakikuwa kimejumuishwa katika bajeti na mpango na wa manunuzi kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 55** hapo chini.

#### **Jedwali Na. 55: Miradi ya ujenzi ambayo haikuwa imepangiwa bajeti**

Na.	Jinala Mradi	Mfadili	Kiasi (Sh.)
1	Ujenzi wa Nyumba za Magomeni	Serikali ya Tanzania	52,195,390,974
2	Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya DAWASA Yetu	DAWASA	48,979,205,784
3	Ujenzi wa Maghorofa ya Mzizima	NSSF	11,806,000,000
4	Ujenzi wa Jengo la Biashara la PSPF	PSSSF	37,528,325,700
Jumla			150,508,922,458

**Chanzo:** Nyaraka za miradi 2016/17 hadi 2021/22

Hii inaweza kusababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi kutokana na kutokuwa na uhakika wa mapokezi ya fedha ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa miradi unakamilika kwa wakati uliopangwa. Pia inaweza kusababisha malipo ya riba kwa ucheleweshwaji wa malipo ambayo husababisha upotevu wa fedha za Serikali.

**Napendekeza kwa menejiment za miradi husika zifanye tathmini ya kazi ambazo hazijakamilika na kuzijumuisha kwenye bajeti na mpango wa manunuzi ili kuhakikisha miradi inakamilika kwa ufanisi.**

#### **14.1.3 Kutokuwepo kwa makadirio ya gharama za awali**

Mazoea ya kitaalamu yanataka makadirio ya gharama za awali kwa ajili ya bajeti kuandaliwa mapema kabla ya kuanza kwa mradi wowote wa ujenzi. Nilibaini mapungufu yafuatayo kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 56** hapo chini.

## Jedwali Na. 56: Miradi isiyokuwa na makadirio ya gharama za awali

Mradi	Kukosekana kwa makadirio ya gharama za awali	Matokeo
Ujenzi wa Nyumba za Magomeni	Makadirio ya gharama za awali hayakuandaliwa.	Kutokuwepo kwa mwongozo wa gharama/kikomo cha gharama za Usanifu wa mradi
Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya DAWASA Yetu	Hakukuwa na makadirio ya gharama za awali. DAWASA ilidai makadirio ya mwisho yalikuwa Sh. bilioni 37 (bila kodi ya VAT), pasipokuwa na Ushahidi.	Mwongozo wa gharama usioridhisha katika usanifu na utekelezaji wa mradi.
Ujenzi wa Jengo la Biashara la PPF, Ofisi Mpya ya Makao Makuu ya PPF, Ukumbi wa Mkuano wa PPF, na Ghorofa ya Maegesho ya PPF.	Makadirio ya gharama za awali zisizo na uhakika zilizo wasilishwa katika ripoti ya upembuzi yakinifu ya Oktoba 2013. Ripoti hiyo ilionesha makisio mbalimbali yaliyoonesha jumla ya gharama za mradi wa ujenzi kama ilivoelezwa katika Jedwali hapo chini.	Kutokuwepo kwa ufanuzi unaojitosheleza wa makadirio ya jumla ya gharama za mradi wa ujenzi. Kulikuwa hakuna uhakika wa gharama ipi ilikuwa imekusudiwa kutumika na ambayo tayari imetumika kama makadirio ya gharama ya mradi.

**Chanzo:** Nyaraka za mikataba

## Jedwali Na. 57: Kutokuwa na uhakika wa gharama zilizokadiriwa za mradi

Hatua ya Upembuzi Yakinifu	Aya kwenye ripoti	Gharama zilizokadiriwa (Dola za Kimarekani)
Upembuzi yakinifu wa awali wa Oktoba 2013	9.2 -Gharama za kuendeleza mradi	137,592,455
	9.3 - Makadirio ya kifedha	138,022,455
Tathmini ya upembuzi yakinifu ya Aprili, 2016	6.1 - Gharama za kuendeleza mradi	112,444,304
	6.2 - Makadirio ya kifedha	125,086,041
	Kiambatisho 1-ukurasa 18	137,592,455

**Chanzo:** Taarifa ya upembuzi yakinifu wa awali uliofanyika mwezi Oktoba 2013 na tathmini ya upembuzi yakinifu iliyofanyika mwezi Aprili 2016

Vile vile, nilibaini kuwa makadirio ya awali ya gharama za ujenzi wa Jengo la Biashara la PSPF lililopo kwenye Kiwanja Namba 2 na 4 kitalu G, eneo la NCC Manispaa ya Dodoma yaliyotayarishwa na Mshauri Elekezi mnamo mwezi Septemba 2013 yalikuwa ni Sh. 29,540,067,322.79 wakati gharama za mkataba zilikuwa Sh. 36,105,065,863.98. Kiasi hiki kilizidi makadirio kwa Sh. 6,564,998,541.19 (22%). Hii ilisababisha PSPF kutafuta fedha zilizoongezeka ili kutekeleza mradi, hali iliyovuruga mtiririko wao wa kifedha.

Ninapendekeza menejimenti wa DAWASA na PSSSF kuanda na kuidhinisha makadirio ya gharama za awali kabla ya kuanza sanifu wa mradi na kutumia makadirio hayo kama mwongozo wa gharama wakati wote wa Usanifu wa mradi.

#### 14.1.4 Maandalizi yasiyotosheleza ya viwango vya ubora katka ujenzi wa magorofa ya Morocco, Kinondoni yaliyosababisha ongezeko la gharama kwa Sh. 1.73 bilioni

Mradi wa Usanifu na ujenzi wa maghorofa kwa ajili matumizi mbali mbali katika kiwanja namba 1-3 na 44 maeneo ya barabara mpya unajumuisha ujenzi wa maghorofa marefu mawili kwa ajili ya ofisi, ghorofa kwa ajili ya hoteli, ghorofa kwa ajili ya makazi na maduka katika sakafu ya chini hadi sakafu ya tatu.

Hata hivyo, nilibaini hakukuwa na ratiba ya kazi kwa ajili ya umaliziaji wa hoteli, ofisi na maduka hivyo kusababisha Shirika la Nyumba la Taifa kuandika barua tarehe 14 Novemba 2015 kumfahamisha mkandarasi nia ya kubadilisha mawanda ya kazi ikiwa ni pamoja na kuweka nyongeza ya sakafu kwenye majengo ya ofisi na maduka. Ongezeko la gharama kulikosababishwa na ongezeko ya sakafu hadi trehe 11 Aprili 2018 ilikuwa ni Sh. 1,729,540,032.

Hivyo, fedha ambazo zingeweza kutumika kwa kazi zingine zilitumika kufidia ongezeko hili. Pia, muda wa ukamilishaji wa mradi uliathirika kutokana na mabadiliko ya mawanda ya kazi ambayo yangeweza kuepukika endapo viwango vya ubora vingekuwa vimetayarishwa vizuri.

Shirika la Nyumba la Taifa linapaswa kuitia na kujumuisha viwango vya ubora kwenye mikataba kabla ya kusaini mikataba ili kuepuka ongezeko la gharama linaloweza kutokea hapo baadaye. Pia, wanapaswa kuitia mkataba huu ili kubaini usahihi wa nyongeza ya gharama iliyotokana na nyongeza ya sakafu na kuchukua hatua stahiki.

## 14.2 Usimamizi wa ununuzi

### 14.2.1 Ujenzi wa jengo la ofisi ya DAWASA yetu na ununuzi wa samani za ofisi pasipo kushindanisha zabuni

Kanuni ya 203(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inahitaji zabuni zishindanishwe ili kubaini gharama ya chini zaidi katika ununuzi wa kazi za ujenzi.

Sikupata ushahidi wa mchakato wa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya DAWASA Yetu (awali Ofisi ya Waziri), na hivyo kushindwa kubaini ushindani wa Mkataba uliotolewa.

Vile vile, nilibaini kuwa mchakato wa ununuzi haukuatuwa katika ununuzi wa samani za ofisi kwa ajili ya jengo la DAWASA Yetu (Maji House) kwa kuwa hakukuwa na ushindani na pia uwezo wa kisheria wa mkandarasi katika kutoa huduma hii haukutajwa katika nyaraka za ununuzi kinyume na Kifungu cha 64(1) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma, 2011 kinachohitaji Taasisi Nunuzi kushindanisha zabuni kwa kutumia njia zilizowekwa katika kanuni kulingana na aina na thamani ya manununuzi na mzabuni aliyeshinda awe aliyethibitishwa kuwa na uwezo wa kutoa huduma. Hii ilisababisha kazi hii kutolewa kwa bei isiyokuwa na ushindani ya Sh. 2,695,991,004.84.

Ingawa DAWASA ilidai kuwa ununuzi wa dharura ulihitajika kutokana na hitaji la kuondoka katika ofisi zao za awali, hata hivyo hakukuwa na ushahidi wa taratibu zilizofanyika kuthibitisha.

Ninapendekeza kwamba DAWASA (a) ifuate taratibu za ununuzi na kuhakikisha kuwepo kwa nyaraka za michakato ya ununuzi. (b) ihakikishe taratibu za ununuzi zinafuatwa katika kuidhinisha ununuzi wa samani za ofisi zenye thamani ya Sh. 2,695,991,004.84 (isiyo na kodi la ongezeko la thamani).

### **14.3 Usimamizi wa mikataba**

#### **14.3.1 Kukosekana kwa nyaraka za Mikataba kwa ujenzi wa Nyumba za Magomeni**

Kanuni ya 20(1) ya Kanuni za Manunuvi ya Umma ya mwaka 2013, kinataka taasisi nunuzi kuwasilisha nyaraka za kutoa zabuni kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuvi ya Umma ndani ya siku 14 ili kutangazwa kwa umma, pia Kifungu Kanuni ya 115 ya Kanuni za Ununuvi ya Umma ya mwaka 2013 inataka taasisi za umma kufuata taratibu za ununuvi na kuingia mikataba na wazabuni.

Nilibaini hakukuwa na nyaraka za mikataba wa ujenzi wa Nyumba za Magomeni. Maafisa wakuu wa Wakala wa Ujenzi Tanzania walini julisha kuwa Wizara ya Ujenzi na Usafirishaji huwa inaingia mikataba wa Utendaji wa Kila Mwaka na Wakala wa Ujenzi Tanzania kwa ajili ya kufuutilia Utekelezaji ambao unachukuliwa kama mikataba. Hata hivyo, nilibaini kwamba Mkataba wa Utendaji wa Kila Mwaka ultengenezwa kwa ajili ya kufuutilia utendaji wa kila mwaka wa shughuli za Wakala wa Ujenzi Tanzania kulingana na Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Wakala wa Utendaji.

Ukosefu wa nyaraka za mikataba kwa miradi ya ujenzi unazuia uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa ununuvi.

**Ninapendekeza kwamba kwa siku zijazo Wakala wa Ujenzi Tanzania iandae nyaraka za mikataba kwa miradi ya ujenzi iliyokabidhiwa kwao.**

#### **14.3.2 Usimamizi usioridhisha wa muda wa utekelezaji wa mradi**

Mapitio ya Mkataba wa Ujenzi wa Maghorofa ya matumizi mbali mbali ya Morocco kwenye kiwanja Namba 1-3 na 44 uliofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa yalibaini kuwa Mkataba ulisainiwa tarehe 4 Aprili 2014 na ulipaswa kukamilika ifikapo tarehe 17 Aprili 2017.

Muda wa kukamilika kwa mikataba uliongezeka kwa siku 231 kutokana na kuchelewa kupata vibali vya ujenzi na kukamilika kwa muundo wa ramani bila ongezeko la gharama. Hata hivyo, Mkandarasi

alisimamisha shughuli za ujenzi kuanzia tarehe 1 Januari 2019 hadi tarehe 31 Oktoba 2020 kwa siku 669 kutokana na kuchelewa kwa malipo ya hati za mdai. Nilibaini kuwa hadi wakati wa ukaguzi mwezi Novemba 2022, hakukuwa na kazi zilizokamilika, wala muda kutekeleza mkataba haukuwa umeongezwa.

Hii ilichelewesha kufikisha faida za mradi huu kwa walengwa na inaweza kuongeza gharama ya mradi kutokana na ongezeko la bei za bidhaa na huduma hapo baadaye.

**Ninapendekeza kwamba Shirika la Nyumba la Taifa liwe na mkakati wa kuhakikisha mradi wa ujenzi unaendelea na kutoa muda wa uhakika wa kumaliza mradi ili kukidhi lengo la uwekezaji uliotarajiwa.**

#### **14.4 Usimamizi wa fedha**

##### **14.4.1 Kushindwa kudai msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani Sh. 4.27 bilioni**

Mradi wa ujenzi wa Maghorofa ya Mzizima kipande cha 2 na 3 ulikuwa na msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani ya asilimia 45, lakini malipo kwa kwa wakandarasi yalijumuisha kodi ya ongezeko la thamani kutokana na kuchelewa huhuisha msamaha huo kutoka kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania kabla muda wake kuisha. Hii ilisababisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Taifa kushindwa kuokoa gharama za Sh. 4,273,246,087.11 ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani.

Kwa maoni yangu, kiasi cha Sh. 4,273,246,087.11 kingeweza kutumika kwa shughuli nyingine za Taasisi.

Ninapendekeza kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Taifa uanzishe mfumo wa kufuatilia muda wa kumalizika kwa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani.

#### 14.4.2 Riba ya kuchelewesha malipo Sh. bilioni 12.12

Kifungu cha 45.1 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba kinataka Mwajiri kumlipa Mkandarasi kiasi kilichohakikiwa na Meneja wa Mradi ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kutolewa kwa kila hati ya madai. Ikiwa Mwajiri atachelewa kulipa, Mkandarasi atalipwa riba ya kuchelewesha kwenye malipo yanayofuata.

Nilibaini kuwa miradi mitano ya ujenzi kati ya miradi tisa iliyokaguliwa ilikuwa na madai ya riba ya Sh. 12,120,114,011 kutokana na ucheleweshwaji wa kulipa hati za madai ya wakandarasi ndani ya muda uliowekwa katika mikataba husika, hivyo wakandarasi walidai riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa. Ni maoni yangu kuwa, gharama hizo za riba zingeweza kuepukwa au kupunguzwa kwa kuanzisha hatua sahihi za usimamizi wa fedha kwenye miradi. Maelezo ya madai ya riba yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 58** hapo chini:

**Jedwali Na. 58: Uchambuzi wa riba iliyodaiwa**

Na.	Jina la Mradi	Mfadhili	Kiasi cha Riba (Sh.)
1	Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya DAWASA Yetu	DAWASA	2,602,222,751
2	Ujenzi wa Maghorofa ya Mzizima	NSSF	1,534,151,091
3	Ujenzi wa Hoteli ya Kitalii Mwanza	NSSF	4,664,162,217
4	Ujenzi wa Jengo la Biashara	PSPF	531,486,589
5	Mradi wa Ujenzi wa nyumba za Makazi Kawe 711	Mkopo na NHC	2,788,091,363
Jumla			12,120,114,011

Chanzo: Faili za Miradi 2016/17-2021/22

Ninapendekeza menejimenti ya miradi ya ujenzi husika kuhakikisha kwamba malipo ya wakandarasi yanalipwa kwa wakati ili kuepuka gharama za riba.

#### 14.4.3 Kutorejeshwa kwa malipo ya awali Sh. milioni 857.21

Kifungu cha 48.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba No. ME-011/2013-2014/W/01 kwa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya DAWASA YETU kinahitaji malipo ya awali kurejeshwa kwa kukata kiasi kinacholingana na kiasi kilichobaki kutoka kwenye malipo au kufuata ratiba ya asilimia za kazi zilizokamilika kama msingi wa malipo.

Ukaguzi wangu ulibaini Sh. 5,619,498,210 (bila kodi) kililipwa kama malipo ya awali, ambapo kati ya kiasi hicho, Sh. 4,762,286,618 zilirejeshwa na kiasi kilichobaki cha Sh. 857,211,592 hakikurejeshwa. Pia nilibaini hakukuwa na Ushahidi wa dhamana ya malipo hayo ya awali. Kwa hivyo, kuna hatari ya upotevu wa fedha za walipakodi ikitokea mkandarasi ameshindwa kutekeleza majukumu yake ya kimkataba.

**Ninapendekeza menejimenti ya DAWASA kuhakikisha kwamba malipo yote ya awali yanarejeshwa kwa kukatwa kwenye malipo yajayo ya mkandarasi.**

#### 14.4.4 Malipo Zaidi ya Sh. 122.75 milioni kwa huduma maalum kwa mkandarasi mkuu

Makubaliano ya mkataba wa mkandarasi msaidizi kwa ufungaji wa umeme, ufungaji wa mabomba, ufungaji wa vifaa vya uhandisi, ufungaji wa kiyoyozi, ufungaji wa vifaa vya TEHAMA, na ufungaji wa vifaa vya usalama kwa ujenzi wa Hoteli ya Kitalii Mwanza-NSSF yanasema kuwa huduma za mkandarasi mkuu zinakwenda sambamba na huduma zilizotajwa katika vipengele 24.0 hadi 28.0 vya mkataba wa mkandarasi msaidizi.

Mapitio ya hati ya madai No.40 na hesabu za makadirio ya gharama ya kazi yalibaini kuwa mhandisi mshauri aliidhinisha Sh. 122,748,314.70 pamoja na VAT kama malipo ya huduma maalum kwa mkandarasi mkuu kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na. 59.

#### Jedwali Na. 59: Malipo yaliyolipwa zaidi kwa huduma maalum kwa mkandarasi mkuu

Kazi ya mkandarasi msaidizi	Kiasi (Sh.)
Ufungaji wa umeme	39,534,048.82
Kufunga viyoyozi and Mifumo ya uingizaji hewa	23,642,997.65
Kufunga mabomba,miundombinu ya utoaji maji and kufunga vifaa vya kupambana na majanga moto	12,647,188.10
Kufunga vifaa vya kiusalama	7,641,590.45
Kufunga vifaa vya TEHAMA	8,583,693.37
Ufungaji wa lifti	11,974,500.00
<b>Jumla ndogo (Isiyokuwa na VAT)</b>	<b>104,024,018.39</b>
Jumlisha: Asilimia 18% VAT	18,724,323.31
<b>Jumla kubwa (Yenye VAT)</b>	<b>122,748,341.70</b>

Chanzo: Uchambuzi wa BoQ ya mkandarasi mkuu na hati ya madai No. 40, 2022

Hii ilitokana na udhibiti na usimamizi usioridhisha katika mchakato wa malipo, na mshauri hakufanya mapitio kwa usahihi kwa kuzingatia makubaliano ya mkataba wa mkandarasi msaidizi.

**NSSF inashauriwa kurejesha Sh. 122,748,341 zilizolipwa zaidi kwa huduma maalum kwa mkandarasi mkuu.**

**14.4.5 Fedha za zuio zililipwa kabla ya muda wa Kipindi cha matazamio kukamilika Sh. 293.44 milioni**

Katika Mkataba No. PA038/HQ/2014/W/15 kwa ajili ya kusanifu, kujenga na kukarabati Jengo la Biashara la PPF, asilimia 10 ya malipo yalitakiwa yazuiwe kama dhamana, kwa kikomo cha kuzuia asilimia 5 ya kiasi cha mkataba kilichokubaliwa. Nusu ya fedha zilizozuiliwa zilitakiwa kulipwa wakati wa ukamilishaji wa mradi na nusu iliyobaki ilitakiwa ilipwe baada ya marekebisheso ya kasoro zilizojitokeza.

Nilibaini kuwa kiasi chote cha fedha za zuio cha Sh. 11,619,472,993.34 kililipwa kwa mkandarasi baada ya kukamilisha mradi na marekebisheso ya kasoro zilizojitokeza.

Kiasi cha mkataba kilijumuisha kiasi cha matengenezo kwa kipindi cha miaka mitano, na mkandarasi bado alikuwa na jukumu la kufanya matengenezo na gharama ya Sh. 5,868,905,390.48 (pamoja na VAT). Hata hivyo, fedha za zuio kwa kazi za matengenezo ambazo zilikadiriwa kuwa Sh. 293,445,269.52 sawa na Asilimia 5 ya gharama ya kazi za matengenezo katika mkataba ziliwu zimeshalipwa kwa mkandarasi.

Kulipa fedha za zuio kabla ya kazi za matengenezo kukamilika ni kinyume na masharti ya mkataba ambayo yanataka fedha za zuio zitolewe baada ya kukamilika kwa kipindi cha matengenezo na utoaji wa hati ya kufanya marekebisheso ya kasoro. Hii inaweza kuathiri ubora wa kazi za matengenezo na kusababisha hasara ya Sh. 293,445,269.52.

**PSSSF inahimizwa kufuata kikamilifu masharti ya mkataba na kulipa fedha za zuio kama ilivyopangwa ili kulinda maslahi ya mwajiri na kuhakikisha kuwa mkandarasi anatimiza majukumu yake ya kimkataba.**

#### **14.4.6 Makadirio ya gharama yasiyojitoshelesha ya nguzo za kusimikwa ardhini yaliyopelekea malipo zaidi ya Sh. 584.68 milioni**

Kifungu 39.2 cha Masharti ya Kawaida ya Mkataba kati ya Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Taifa na M / s Chongoing International Construction JV M/S Group Six International Co. Ltd kwa ajili ya ujenzi wa maghorofa ya Mzizima kinahitaji makadirio ya gharama za kazi kutumika katika kupata gharama za Mkataba. Mkandarasi atalipwa kwa kazi iliyofanyika kulingana na kiwango katika BOQ kwa kila kipengele.

Mapitio ya makadirio ya gharama na hati za madai kwa kipande cha 3 na kipande cha 2 yilibaini kwamba mkandarasi alilipwa fedha zaidi kuliko gharama za mkataba kwa nguzo za kusimikwa ardhini. Malipo yaliyofanywa yalikuwa Sh. 381,941,036.26 kwa kipande cha 3 na Sh. 225,240,000 kwa kipande cha 2, wakati bei za mkataba zilikuwa Sh. 15,500,000 na Sh. 7,000,000 mtawalia. **Jedwali Na. 60** linaonyesha maelezo.

#### **Jedwali Na. 60: Gharama zilizotumiwa kwa nguzo za kusimikwa ardhini**

Maelezo	Kipimo	Idadi	Kiwango (Sh.)	Kiasi (Sh.)
Kipande cha 3: Hati ya madai No. 50 Gharama za kuweka mitambo kwa ajili ya kusimika nguzo ardhini na kuiondoa kwenye eneo la mradi baada ya kazi kukamilika.	a. Kukodish a mitambo ya kunyanyulia	Kifaa		65,000,000
	b. Kifaa cha kuondoa vumbi	Namba	4	7,800,000
	c. Mashine ya kutindua	Namba	7	3,200,000
	d. Mashine ya umeme ya kutindua	Namba	12	1,900,000
	e. Vingine	Kifaa		8,600,000
	f. Jumla ya gharama ya kusimika nguzo 306 ardhini (Kipande)	Mita	1341	150,000
	Kipande cha 3	Mita za ujazo	592.135	22,000
	h. Kukusanya vifusi na kuiondoa	Mita za ujazo	592.135	30,000
				13,026,976.88
				17,764,059.38

Maelezo	Kipimo	Idadi	Kiwango (Sh.)	Kiasi (Sh.)
	<b>Gharama ya kusimika nguzo ardhini</b>			<b>381,941,036. 26</b>
	<b>Toa: Malipo kwa kifaa</b>			<b>15,500,000</b>
	<b>Malipo zaidi</b>			<b>366,441,036. 26</b>
Kipande cha 2: Hati ya madai No. 47 Gharama za kuweka mitambo ya kukata nguzo za kusimika ardhini na kuiondoa kwenye eneo la mradi baada ya kazi kukamilika.	a. Kukodish a mitambo ya kunyanyulia	Kifaa		40,000,000
	b. Kifaa cha kuondoa vumbi	Namba	2	7,800,000
	c. Mashine ya kutindua	Namba	5	3,200,000
	d. Mashine ya umeme ya kutindua	Namba	10	1,900,000
	e. Vingine	Kifaa		9,400,000
	f. Jumla ya gharama ya kusimika nguzo 168 ardhini (Kipande)	Mita	724	150,000
	g. Kuiondoa mabaki ya zege mitaroni.	Mita za ujazo	320	22,000
	h. Kukusanya vifusi na kuiondoa	Mita za ujazo	320	30,000
	<b>Gharama ya kusimika nguzo ardhini (Pile cutting)</b>			<b>225,240,000</b>
	<b>Ondo: Malipo kwa kila kifaa</b>			<b>7,000,000</b>
	<b>Malipo zaidi kwa kila kifaa</b>			<b>218,240,000</b>
<b>Gharama ilioongezeka (Malipo zaidi kwa kipande cha 2 na 3)</b>				<b>584,681,036</b>

**Chanzo:** Uchambuzi wa wakaguzi na IPC No. 50 kwa kipande cha 3 na No. 47 kwa kipande cha 2

Gharama za nguzo za kusimika zilichukuliwa kama gharama za jumla wakati wa utekelezaji kwa kiasi cha Sh. 607,181,036 (Sh. 381,941,036 + Sh. 225,240,000). Mshauri alidai kwamba mabadiliko hayo yalitokana na idhini kutoka kwa mteja, lakini sikuona ushahidi wa idhini hiyo.

Awali, NSSF ilipanga kuwa kofia za nguzo za kusimika ardhini kuwa mita 8 chini ya usawa wa ardhi, na uchimbaji ulianzia kwenye mita 4., kufuatisha na ripoti ya uchunguzi wa kiufundi ambayo ilionyesha kina cha maji kilikuwa mita 8 chini ya usawa wa ardhi. Hata hivyo, wakati wa wa kusimika nguzo ardhini, maji yalikutwa kwenye mita 2

chini ya usawa wa ardhi, ambayo haikuwa imejumuishwa kwenye ripoti. Hii ilihitaji kubadilisha njia ya uchimbaji nguzo za kusimika ardhini, ambao ulisababisha kuongezeka kwa nguzo za kusikima ardhini, kupunguzwa kwa urefu wa ziada, kuongezeka kwa muda wa kukamilisha mradi, na ongezeko la gharama za mkataba.

**Ninapendekeza menejimenti ya NSSF kuhakikisha kuwa kiasi kilicholipwa zaidi cha Sh. 584,681,036 kinarejeshwa kutoka kwa mkandarasi kutikana na makadirio ya gharama yasiyojitosheleza ya kofia za nguzo za kusimika ardhini.**

#### **14.4.7 Wakandarasi wanne wa mkataba walilipwa malipo ya awali bila kuwepo matakwa ya kimkataba Sh. bilioni 4.83**

Kifungu cha 3.3 (j) cha Mkataba wa Mhandisi Mshauri Mkuu kwa ajili ya Ujenzi wa Hoteli ya Kitalii Mwanza-NSSF kinataka mhandisi mshauri kutoa hati za madaiza mkandarasi.

Hata hivyo, mapitio ya mikataba ya wakandarasi wasaidizi yalibaini kuwa mkataba wa mkandarasi msaidizi mmoja ulijuimisha masharti ya ulipaji wa malipo ya awali, wakati mikataba wa wakandarasi wengine haikuzungumzia malipo ya awali. Licha ya hilo, wakandarasi wanne walilipwa malipo ya awali kulingana na hati ya madai namba 40, ingawa mikataba yao haikuwa na kifungu hicho. **Jedwali Na. 61** linatoa maelezo zaidi.

#### **Jedwali Na. 61: Malipo ya Awali yalilipwa kwa wakandarasi wasaidizi bila makubaliano ya Mkataba**

Huduma ya wakandarasi wasidizi	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Malipo ya awali yaliyolipwa (Sh.)	Maoni ya ukaguzi
Kufunga umeme	11,892,973,666.90	1,783,946,050.04	Haikutajwa kwenye mkataba
Kufunga viyoyozi	9,649,303,359	1,447,395,503.85	Hakuna Mkataba wa mhandisi msaidizi
Kufunga mfumo wa mabomba	8,656,058,618	1,298,408,792.77	Haikutajwa kwenye mkataba
Kufunga vifaa vya usalama	1,997,436,621.54	299,615,493.23	Haikutajwa kwenye mkataba
<b>Jumla</b>	<b>32,195,772,265.44</b>	<b>4,829,365,839.89</b>	

**Chanzo:** Uchambuzi wa mikataba ya mkandarasi msaidizi iliyopitiwa na hati madai namba 40

Hii inaonyesha kwamba mhandisi mshauri aliruhusu malipo haya pasipokuwa na makubaliano ya kimkataba. Ukosefu wa usimamizi sahihi wa fedha unaweza kusababisha upotevu wa fedha za miradi na kupelekea kukosekana kwa fedha katika hatua zijazo za utekelezaji wa mradi.

Ninapendekeza NSSF kufanya mapitio mkataba wa mhandisi mshauri ili kuhakikisha kwamba kuna masharti ya wazi na vipengele vya mtiririko vya fedha za mradi, na kuweka mfumo wa kufuatilia na kudhibiti ili kuidhinisha malipo yoyote yaliyo nje ya mipango ya fedha kuepuka ukosefu wa fedha na kuhakikisha miradi inakamilika kama ilivyopangwa.





## SURA YA KUMI NA TANO



HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## **15.0 Utangulizi**

Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo juu ya masuala muhimu yaliyojitokeza katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2021/22. Lengo ni kuwasilisha ujumbe muhimu na kutoa mapendekezo ya jumla ambayo yanashughulikia mapungufu ambayo yametokea katika sekta mbalimbali.

### **15.1 Hitimisho la Jumla**

Serikali imefanya juhudini kubwa katika kuhakikisha miradi ya maendeleo inayotekelizwa katika sekta mbalimbali inafikia malengo yake ya mwaka. Nimebaini jitihada zilizofanywa na serikali katika kuimarisha uhusiano na washirika wa maendeleo na sekta binafsi kwa kujenga mazingira mazuri katika kuunga mkono bajeti ya serikali, kutoa mikopo nafuu na kuwekeza mtaji katika nchi. Hata hivyo, mbali na juhudini hizi, bado nimebaini kuwa kuna upungufu unaohitaji kuboreshwa katika baadhi ya taasisi za serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyobainika katika ukaguzi uliofanyika wa kifedha na kiufundi. Upungufu huu unahusiana kwa kiasi kikubwa na masuala ya kifedha, ununuzi na usimamizi wa mikataba hususani katika miradi ya ujenzi.

Uchambuzi wangu unaonesha kwamba, zaidi ya asilimia 90 ya miradi imepata hati safi kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2017/18 hadi mwaka 2021/22 ambayo inaleta uaminifu wa taarifa za kifedha za miradi. Hata hivyo uchambuzi wa utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita kwa miaka mitano mfululizo ya kifedha, yaani 2017/18 hadi 2021/22, ni chini ya asilimia 50 kwa hoja zinazojirudia kama ilivyobainishwa katika sura ya pili ya taarifa yangu.

Pia uchambuzi wangu kuhusu ununuzi unaonesha kuwa kwa ujumla watekelezaji wa miradi walifuata Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 wakati wa utekelezaji wa shughuli za miradi katika mwaka wa fedha 2021/22. Hata hivyo nilibaini matukio ya kutotumia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi kwa baadhi ya watakelezaji wa miradi pamoja na mchakato mrefu wa ununuzi uliosababisha kutotekelezwa kwa shughuli ndani ya

wakati uliopangwa na kuongeza hatari ya serikali kulipa gharama za ahadi kwa kiasi ambacho hakijatolewa kwa mujibu wa vigezo na masharti yailiyokubalika katika fursa mbalimbali za mikopo zilizotolewa na Washirika wa Maendeleo.

Mikataba hasa ya miradi yenyeye ugumu katika utekelezaji inahitaji usimamizi mzuri. Usanifu usioridhisha sio tu unahatarisha kuongezeka kwa muda na gharama za miradi bali pia huathiri ubora.

## 15.2 Mapendekezo ya jumla

Kutokana na matokeo ya ukaguzi, yafuatayo ni mapendekezo kwa Serikali ambayo yanakusudia kushughulikia mapungufu ambayo yanaathiri miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali.

- (i) Ofisi ya Uratibu wa Miradi ya Serikali inapaswa kuundwa ili kusaidia na kusimamia utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo nchini.
- (ii) Kubuni na kuunda vipimo muhimu vya utendaji ili kufuutilia utendaji wa miradi katika maeneo mbalimbali, kama vile usimamizi wa fedha na utekelezaji wa mapendekezo ya miaka ya nyuma. Kuchukua hatua muhimu dhidi ya watekelezaji wa miradi ambao hawakidhi mahitaji ya kiwango cha chini cha utendaji.
- (iii) Kubuni mfumo imara wa ufadhili wa miradi ambao utabashiri na kuhakikisha mtiririko wa fedha unaoweza kutegemewa ili kuhakikisha madai ya wakandarasi yaliyothibitishwa yanapewa kipaumbele na kulipwa kwa wakati ili kuzuia migogoro ya baadaye na malipo ya riba kwa madai ya wakandarasi yaliyopita muda wake.
- (iv) Kupunguza hatari zinazohusiana na masuala ya usalama na matatizo ya mazingira ambayo yanaweza kuzuia uendelevu wa miradi iliyotekelozwa.
- (v) Kuhakikisha upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi unafanyika kwa ufanisi na kuidhinishwa kwa usahihi kabla ya kuanza kwa miradi.
- (vi) Kuweka vigezo sahihi kwa ajili ya kugawanya fedha za ujenzi wa miundombini ya shule kwa kuzingatia vigezo halisi kama vile topografia ya ardhi, bei za vifaa katika maeneo mbalimbali na

mambo mengine ili kuhakikisha miradi hii inakamilishwa kama ilivyopangwa.



## VIAMBATISHO

### Kiambatisho I: Muhtasari wa samani na vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano

Na.	Maelezo ya bidhaa	Kiasi	Bei (Sh)	
			Bei kwa kiasi	Jumla
<b>Samani na vifaa</b>				
1	Kiti bora cha ofisi (kinachotengenezwa hapa nchini); Kiti: 50 (U) X 52 (P) X 50 (K) Nyuma: 45 (U) X 70 (K) 4 350,000 1,400,000	4	350,000	1,400,000
2	Viti vya Ofisi (vinavyotengenezwa hapa nchini) Kiti: 50 (U) X 52 (P) X 50 (K) Nyuma: 45 (U) X 70 (K) 5 300,000 1,500,000	5	300,000	1,500,000
3	Viti vya Mkutano/Wageni (vinavyotengenezwa hapa nchini) Kiti: 50 (U) X 45 (P) X 50 (K) Nyuma: 50 (U) X 50 (K) 30 180,000 5,400,000	30	180,000	5,400,000
4	Meza ya Mkutano: (inayotengenezwa hapa nchini); Kipande kuu 140 (U) X 60 (P) X 76 (K) 6 600,000 3,600,000	6	600,000	3,600,000
5	Meza ya Mkutano: (inayotengenezwa hapa nchini) meza ya kawaida: 80 (U) X 60 (P) X 76 (K) 2 550,000 1,100,000	2	550,000	1,100,000
6	Meza ya Mkutano: (inayotengenezwa hapa nchini); vipande vya mkutano vinavyounganishwa; 60 (U) X 60 (P) X 76 (K) 2 450,000 900,000	2	450,000	900,000
7	Meza bora yenyе jedwali moja (170 x 75 x 76cm) 9 850,000 7,650,000	9	850,000	7,650,000
8	Kabati la chuma; linaficha droo nne 4 500,000 2,000,000	4	500,000	2,000,000
9	Mlango mara mbili unaweza kufuliwa - wenye ubao (unatengenezwa hapa nchini) 3 800,000 2,400,000	3	800,000	2,400,000
Jumla ndogo				25,950,000
Vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano				
10	Kompyuta ya mezani 2 2,995,000 5,990,000	2	2,995,000	5,990,000
11	Mashine ya kuchapa 2 1,695,000 3,390,000	2	1,695,000	3,390,000
12	Kifaa cha kudhibitibiti umeme wa kompyuta UPS 750 VA 2 895,000 1,790,000	2	895,000	1,790,000
Jumla ndogo				11,170,000
Jumla kuu				37,120,000

**Chanzo:** Hati za manunuizi, rekodi za manunuizi na faili za mikataba

## Kiambatisho II: Kutokuanza kwa ujenzi na kutonunuliwa kwa vifaa vya shule mpya za sekondari

Na.	Jina la halmashauri	Jina la shule	Na.	Jina la halmashauri	Jina la shule
1	Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro	Shule ya Msingi Ololosokwani	19	Halmashauri ya Wilaya ya Gairo	Shule ya Msingi Rubebo
2	Halmashauri ya Mji wa Kibaha	Shule ya Msingi Kongowe	20	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	Shule ya Msingi Lukobe
3	Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	Shule ya Msingi Mwangia	21	Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	Shule ya Msingi Ufukoni
4	Halmashauri ya Wilaya ya Mafia	Shule ya Msingi Msufini	22	Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	Shule ya Msingi Mnomo
5	Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa	Shule ya Msingi Karume	23	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu	Shule ya Msingi Mangaka
6	Halmashauri ya Mji wa Geita	Shule ya Msingi Nyalubanga	24	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba	Shule ya Msingi Nyamilama
7	Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale	Shule ya Msingi Busolwa	25	Halmashauri ya Wilaya ya Magu	Shule ya Msingi Ilungu
8	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	Shule ya Msingi Msuluti	26	Halmashauri ya Wilaya Sumbawanga	Shule ya Msingi Illemba
9	Halmashauri ya Mji wa Mafinga	Shule ya Msingi Itimbo	27	Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga	Shule ya Msingi Kipapa
10	Halmashauri ya Wilaya ya Mlele	Shule ya Msingi Mgombe	28	Halmashauri ya Wilaya Namtumbo	Shule ya Msingi Sasawala
11	Halmashauri ya Wilaya ya Hai	Shule ya Msingi Kikavu chini	29	Halmashauri ya Wilaya Tunduru	Shule ya Msingi Nanjoka
12	Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'	Shule ya Msingi Waranga	30	Halmashauri ya Manispaa Kahama	Shule ya Msingi Majengo
13	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto	Shule ya Msingi Mbeli	31	Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu	Shule ya Msingi Idukilo
14	Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu	Shule ya Msingi Ngwandakw	32	Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga	Shule ya Msingi Mwalugoye
15	Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali	Shule ya Msingi Uswiswi	33	Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu	Shule ya Msingi Nyamilangono
16	Halmashauri ya Jiji la Mbeya	Shule ya Msingi Inyala	34	Halmashauri ya Wilaya ya Itilima	Shule ya Msingi Senani
17	Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya	Shule ya Msingi Swaya	35	Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi	Shule ya Msingi Matongo
18	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe	Shule ya Msingi Ikuti			

**Chanzo:** Hati za malipo, Nyaraka za mradi na kutembelea miradi

### Kiambatisho III: Shule mpya za sekondari zilizojengwa bila hati miliki za ardhi

No.	Mkoa	Wilaya/Halma	Jina la shule	Fedha iliyopokelewa (Sh.)
1	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa	Shule ya Sekondari Galigali	470,000,000
2	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa	Shule ya Sekondari Iwondo	470,000,000
3	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa	Shule ya Sekondari Nghambi	470,000,000
4	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa	Shule ya Sekondari Lenjulu	470,000,000
5	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	Shule ya Sekondari Nhinihi	470,000,000
6	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	Shule ya Sekondari Zajilwa	470,000,000
7	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Bahi	Shule ya Sekondari Mpinga	470,000,000
8	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Chemba	Shule ya Sekondari Churuku	470,000,000
9	Mtwara	Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	Shule ya Sekondari Lipumburu	470,000,000
10	Mtwara	Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Municipal	Shule ya Sekondari Umoja	470,000,000
11	Mtwara	Halmashauri ya Mji Nanyamba	Shule ya Sekondari Namtumbuka	470,000,000
12	Mtwara	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu	Shule ya Sekondari Nanyumbu	470,000,000
13	Mtwara	Halmashauri ya Wilaya ya Newala	Shule ya Sekondari Nakahako	470,000,000
14	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Illemela	Shule ya Sekondari Buruguza	470,000,000
15	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana	Shule ya Sekondari Kibanda	470,000,000
16	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa	Shule ya Sekondari Irenza	470,000,000
17	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema	Shule ya Sekondari Ibondo	470,000,000
18	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Magu	Shule ya Sekondari Sukuma	470,000,000
19	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi	Shule ya Sekondari Misasi	470,000,000
20	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe	Shule ya Sekondari Bwisya	470,000,000
21	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba	Shule ya Sekondari Kilyaboya	470,000,000
22	Mwanza	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba	Shule ya Sekondari Nkalalo	470,000,000
23	Mbeya	Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	Shule ya Sekondari Bondeni	470,000,000
24	Mbeya	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe	Shule ya Sekondari Msasani	470,000,000
25	Manyara	Halmashauri ya Wilaya ya Babati	Shule ya Sekondari Sarame	470,000,000
26	Manyara	Halmashauri ya Wilaya ya Hanang	Shule ya Sekondari Chief Sarja	470,000,000
27	Lindi	Halmashauri ya Wilaya ya Mtama	Shule ya Sekondari Chiponda	470,000,000

Na. .	Mkoa	Wilaya/Halma	Jina la shule	Fedha iliyopokelewa (Sh.)
28	Lindi	Halmashauri ya Wilaya ya Liwale	Shule ya Sekondari Mangirikiti	470,000,000
29	Lindi	Halmashauri ya Manispaa ya Lindi	Shule ya Sekondari Mingoyo	470,000,000
30	Lindi	Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa	Shule ya Sekondari Nanganga	470,000,000
31	Lindi	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa -Masoko	Shule ya Sekondari Ngome	470,000,000
32	Lindi	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	Shule ya Sekondari Somanga	470,000,000
33	Lindi	Halmashauri ya Manispaa ya Lindi	Shule ya Sekondari Kilangala	470,000,000
34	Lindi	Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa	Shule ya Sekondari Mbwemkuru	470,000,000
35	Lindi	Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea	Shule ya Sekondari Ngunichile	470,000,000
36	Shinyanga	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	Shule ya Sekondari Igalamya	470,000,000
37	Shinyanga	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	Shule ya Sekondari Lubaga	470,000,000
38	Shinyanga	Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu	Shule ya Sekondari Elias Kwandikwa	470,000,000
39	Katavi	Halmashauri ya Wilaya ya Mlele	Shule ya Sekondari Kamsisi	470,000,000
40	Katavi	Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda	Shule ya Sekondari Kawalyowa	470,000,000
41	Katavi	Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda	Shule ya Sekondari Mbugani	470,000,000
42	Katavi	Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe	Shule ya Sekondari Mwamapuli	470,000,000
43	Katavi	Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo	Shule ya Sekondari Kapalala	470,000,000
44	Katavi	Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika	Shule ya Sekondari Majalila	470,000,000
45	Kagera	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	Shule ya Sekondari Rukoma	470,000,000
46	Kagera	Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba	Shule ya Sekondari Kashai	470,000,000
47	Kagera	Halmashauri ya Wilaya ya Misenty	Shule ya Sekondari Kitobo	470,000,000
48	Kagera	Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo	Shule ya Sekondari Nyakahura	470,000,000
49	Kagera	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	Shule ya Sekondari Mushagabo s	470,000,000
50	Kagera	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	Shule ya Sekondari Burigi	470,000,000
51	Kagera	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	Shule ya Sekondari Mafumbo	470,000,000
52	Arusha	Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru	Shule ya Sekondari Amsha	470,000,000
53	Arusha	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	Shule ya Sekondari Ayalabe	470,000,000
54	Arusha	Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro	Shule ya Sekondari Ololosokwani	470,000,000
55	Arusha	Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro	Shule ya Sekondari Oldonyo sambo	470,000,000
56	Arusha	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	Shule ya Sekondari Kiutu	470,000,000

Na. .	Mkoa	Wilaya/Halma	Jina la shule	Fedha iliyopokelewa (Sh.)
57	Mara	Halmashauri ya Mji Tarime	Shule ya Sekondari Gicheri	470,000,000
58	Mara	Halmashauri ya Wilaya ya Tarime	Shule ya Sekondari Bukira	470,000,000
59	Mara	Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti	Shule ya Sekondari Morotonga	470,000,000
60	Mara	Halmashauri ya Wilaya ya Rorya	Shule ya Sekondari Bugendi	470,000,000
61	Mara	Halmashauri ya Wilaya ya Musoma	Shule ya Sekondari Ifulifu	470,000,000
62	Mara	Halmashauri ya Mji Bunda	Shule ya Sekondari Nyamakokoto	470,000,000
63	Dodoma	Halmashauri ya Mji Kondoaa	Shule ya Sekondari Tura	470,000,000
64	Dodoma	Halmashauri ya Wilaya ya Kondoaa	Shule ya Sekondari Bukulu	470,000,000
65	Kigoma	Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza	Shule ya Sekondari Mpeta	470,000,000
66	Kigoma	Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo	Shule ya Sekondari Muhambwae	470,000,000
67	Kigoma	Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko	Shule ya Sekondari Gwanumpuu	470,000,000
68	Morogoro	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	Shule ya Sekondari Lukobe	470,000,000
69	Morogoro	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	Shule ya Sekondari Mindu	470,000,000
70	Iringa	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	Shule ya Sekondari Luhota	470,000,000
71	Iringa	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	Shule ya Sekondari Pawaga	470,000,000
72	Iringa	Halmashauri ya Manispaa ya Iringa	Shule ya Sekondari Mawelewele	470,000,000
73	Iringa	Halmashauri ya Manispaa ya Mafinga	Shule ya Sekondari Changarawee	470,000,000
74	Iringa	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi	Shule ya Sekondari Ifwagi	470,000,000
75	Iringa	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi	Shule ya Sekondari Igowole	470,000,000
76	Daressalam	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke	Shule ya Sekondari Chamanzi	470,000,000
77	Daressalam	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	Shule ya Sekondari Hananasifu	470,000,000
78	Daressalam	Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo	Shule ya Sekondari Msakuzi	470,000,000
79	Daressalam	Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	Shule ya Sekondari Tundwi Songani	470,000,000
80	Daressalam	Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo	Shule ya Sekondari Urafiki	470,000,000
81	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Same	Shule ya Sekondari Kalemawe	470,000,000
82	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Hai	Shule ya Sekondari Mailisita	470,000,000
83	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Same	Shule ya Sekondari Mighareni	470,000,000
84	Kilimanjaro	Halmashauri ya Manispaa ya Moshi	Shule ya Sekondari Moshi Technical	470,000,000
85	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga	Shule ya Sekondari Kifaru	470,000,000

Na. .	Mkoa	Wilaya/Halma	Jina la shule	Fedha iliyopokelewa (Sh.)
86	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Rombo	Shule ya Sekondari Makalema	470,000,000
87	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Siba	Shule ya Sekondari Nuru	470,000,000
88	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Moshi	Shule ya Sekondari Weruweru	470,000,000
89	Kilimanjaro	Halmashauri ya Wilaya ya Moshi	Shule ya Sekondari Muungano	470,000,000
90	Morogoro	Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero	Shule ya Sekondari Homboza	470,000,000
91	Morogoro	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	Shule ya Sekondari Maguha	470,000,000
92	Morogoro	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	Shule ya Sekondari Mhenda	470,000,000
93	Morogoro	Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro	Shule ya Sekondari Mghambi	470,000,000
94	Morogoro	Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi	Shule ya Sekondari Kipingo	470,000,000
95	Morogoro	Halmashauri ya Wilaya ya Ifakara	Shule ya Sekondari Kwashungu	470,000,000
96	Morogoro	Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba	Shule ya Sekondari Mofu	470,000,000
97	Morogoro	Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga	Shule ya Sekondari Vigoi	470,000,000
98	Kigoma	Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu	Shule ya Sekondari Kabagwe	470,000,000
99	Kigoma	Halmashauri ya Mji Kasulu	Shule ya Sekondari Bongwe	470,000,000
100	Kigoma	Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma	Shule ya Sekondari Kagongo	470,000,000
101	Kigoma	Halmashauri ya Mji Kigoma	Shule ya Sekondari Buhanda	470,000,000
				47,470,000,000

**Chanzo:** Hati za malipo, Nyaraka za mradi na kutembelea miradi

#### Kiambatisho IV: Taarifa za mkataba wa mhandisi mshauri

Huduma za ushauri kwa mapitio ya ubunifu na uangalizi wa ujenzi wa BRT awamu ya 2; lot 1: kazi za barabara (20.3 km)	
Namba ya zabuni	AE/001/2015-16/HQ/C/25.
Aina ya ugavi	Ushindanishi wa Zabuni kimataifa
Namba ya mkataba	TRD/HQ/1038/2016/17
Mwajiri	TANROADS
Mshauri	M/S BOTEK Bosphorus Technical Consulting Corporation ya Turkey kwa kushirikiana na M/S Apex Engineering Co. Ltd of Tanzania (mshauri mdogo)
Jina la mkataba	Huduma za Ushauri kwa Mapitio ya Ubunifu na Uangalizi wa Ujenzi wa Mfumo wa Usafiri wa Haraka kwa Basi Dar Es Salaam (BRT) - Awamu ya 2; Lot 1: Kazi za Barabara (20.3 Km) Ikiwa ni pamoja na Daraja 2 na Vituo vya Basi 29 kando ya Barabara ya Kilwa (Kutoka CBD-Kariakoo hadi Mbagala)
Chanzo cha fedha	FedhaBenki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mfuko wa Ukuaji Kimendeleo kwa Pamoja Afrika (AGTF)
Tarehe ya kusaini mkataba	25 Februari 2017
Tarehe ya kuanza kazi	27 Machi 2017
Muda wa awali wa mkataba	Miezi 46
Muda wa mkataba uliorekebishwa	86

Muda uliotumika (Novemba 2022)	Miezi 69
Tarehe ya awali ya kumaliza kazi	5 Januari 2021
Tarehe ya kumaliza kazi iliyorekebishwa	19 Aprili 2024
Thamani ya awali ya mkataba	Dola za Kimarekani 2,434,650 (ikiwa na kodi)
Thamani ya mkataba iliyorekebishwa	Dola za Kimarekani 5,110,312
Mabadiliko	210% <sup>5</sup>
Hali ya utekelezaji (Novemba 2022)	Mradi uko katika utekelezaji wa 80.09%

**Chanzo:** Hati za malipo, IPCs na makabrasha ya mikataba

#### Kiambatisho V: Taarifa za mkataba wa mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya BRT

Ujenzi wa miundombinu ya Dar es Salaam BRT awamu ya 2; lot 1: ujenzi wa barabara (20.3km)	
Namba ya zabuni	AE/001/2017-18/DSM/W/98
Kipindi cha zabuni	Aprili 2018 mpaka 19 Novemba 2018
Namba ya mkataba	TRD/HQ/1047/2018/19
Jina la mkataba	Huduma za Ushauri kwa Mapitio ya Ubunifu na Uangalizi wa Ujenzi wa Mfumo wa Usafiri wa Haraka kwa Basi Dar Es Salaam (BRT) - Awamu ya 2; Lot 1: Kazi za Barabara (20.3 Km) Ikiwa ni pamoja na Daraja 2 na Vituo vyta Basi 29 kando ya Barabara ya Kilwa (Kutoka CBD-Kariakoo hadi Mbagala)
Chanzo cha Fedha	FedhaBenki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mfuko wa Ukuaji Kimaendeleo kwa Pamoja Afrika (AGTF)
Mwajiri	TANROADS
Mkandarasi	M/S Sinohydro Corporation Ltd
Mshauri	M/S BOTEK Bosphorus Technical Consulting Corporation ya Turkey kwa kushirikiana na M/S Apex Engineering Co. Ltd of Tanzania (mshauri mdogo)
Tarehe ya barua ya kukubaliwa	19 Novemba 2018
Tarehe ya kusaini mkataba	10 Desemba 2018
Tarehe ya kuanza mkataba	6 Mei 2019
Tarehe ya awali ya kipindi cha mkataba	Siku 1,095
Tarehe iliyorekebishwa ya kipindi cha mkataba	Siku 1,421
Muda uliotumika (Novemba 2022)	Siku 1,304
Tarehe ya awali ya kumaliza	5 Mei 2022
Tarehe iliyorekebishwa ya kumaliza	27 Machi 2023
Thamani ya awali ya mkataba	Sh. 189,433,784,506.45 (ikiwa na VAT)
Revised <sup>6</sup> Contract Price	Sh. 217,480,899,399.47 (ikiwa na VAT)
Kipindi cha matazamio	Mwaka 1 kwa kazi za barabara

<sup>5</sup> Mabadiliko haya yanatokana na ongezeko Na. 1 la Dola za Kimarekani 135,000; ongezeko Na. 2 la Dola za kimarekani 574,375; ongezeko Na. 3 la Dola za kimarekani 86,687; na ongezeko Na. 4 la Dola za Kimarekani 1,879,600.

<sup>6</sup> The revision of contract price was based on the addendum Number one

	Miaka 3 kwa madaraja ya juu Miaka 5 kwa mfumo wa taa za juu
Kiasi cha thamani ya mkataba kilicholipwa	71.14
Ukamilishaji wa kazi kwa asilimia ya kazi inayoendelea (hadi mwisho wa Novemba 2022)	80.09% (Kulingana na programu ya kazi katika hatua hii, maendeleo yalipaswa kuwa 86.11%)

**Chanzo:** Hati za malipo, IPCs na makabrasha ya mikataba

**Kiambatisho VI: Hati za Malipo pamoja na tozo za riba katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Lusitu - Mawengi kipande cha 2 kwa kiwango cha zege**

Hati ya Mali po Na.	Tarehe ya kuwasilisha	Mwisho wa Malipo	Muda uliochel eweshwa (Siku)	Kiasi cha riba kilichodaiwa katika Hati ya Malipo (Sh.)	Kiasi cha Hati ya Malipo bila Riba (Sh.)	Kiasi cha Riba Kilichodaiwa (Sh.)
1	17 Januari 2018	14 Februari, 2018	268	-	4,820,675,475	170,561,791
2	12 Oktoba 2018	09 Novemba, 2018	68	163,407,127	4,019,652,750	180,465,557
3	12 Oktoba 2018	09 Novemba, 2018	198	127,282,077	5,282,744,024	434,418,704
4	5 Oktoba 2019	02 Agosti 2019	70	1,200,009,606	2,286,629,332	45,198,107
5	13 Septemba 2019	11 Oktoba	27	199,204,928	4,412,644,672	24,412,991
6	10 Oktoba 2019	07 Novemba, 2019	50	-	5,072,919,708	154,162,703
7	29 Novemba 2019	27 Desemba 2019	238	3,684,672	5,072,919,708	57,572,443
8	24 Julai 2020	21 Agosti 2020	60	1,447,253,558	355,150,541	107,088,396
9	22 Septemba 2020	20 Oktoba 2020	41	116,007,480	45,580,209	174,690,421
10	06 Julai 1971	No information	35	58,788,944	3,779,280,054	231,215,543
11	07 Desemba 2020	04 Januari 2021	49	103,475,318	70,146,542,310	262,915,365
12	02/01/2021	22 Februari 2021	229	132,626,936	10624 532 888.39	686,881,828
13	27 Septemba 2021	25 Oktoba 2021	28	3,061,982,664	5622524039 78	113,574,886
14	25 Oktoba 2021	22 Novemba 2021	29	73,859,881	8,075.60 .99833	70,880,838
15	23 Novemba 2021	21 Desemba 2021	30	-	7,763,402	40,356,829
16	23 Desemba 2021	20 Januari 2022	61	165,016,596	82,722,611	51,959,642
17	22 Februari 2022	22 Machi 2022	131	184,440,435	6,793,788,895	205,840,129

Hati ya Malipo Na.	Tarehe ya kuwasilisha	Mwisho wa Malipo	Muda uliochel eweshwa (Siku)	Kiasi cha riba kilichodaiwa katika Hati ya Malipo (Sh.)	Kiasi cha Hati ya Malipo bila Riba (Sh.)	Kiasi cha Riba Kilichodaiwa (Sh.)
	Jumla ndogo		1,612	7,037,040, 222	4,903,861,435	3,012,196, 172
Kiasi cha riba kinachodaiwa (A)				654,759,85 5		
Jumla kuu (Jumla ndogo + A)				7,691,800, 077		

**Chanzo:** Uchambuzi wa wakaguzi kuhusu kumbukumbu za malipo, 2023

